Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Saba – Tarehe 17 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Halmashauri ya Biashara ya Nje kwa Miaka ya Fedha ya 2005/2006 na 2006/2007 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Board of External Trade (BET) for the Financial Years 2005/2006 and 2006/2007).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 65

**Ujenzi wa Barabara za Lami Singida Mjini**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Mkoa wa Singida kwenye Mkutano wa hadhara uliofanyika tarehe 4 Agosti, 2009 aliahidi kuunga mkono juhudi za Manispaa ya Singida Mjini, katika ujenzi wa barabara za lami ndani ya Manispaa.

Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ituatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Mkoa wa Singida tarehe 4 Agosti, 2009 alitoa ahadi ya kuunga mkono juhudi za Manispaa ya Singida katika ujenzi wa barabara za lami.

Katika mwaka 2010/2011 Halmashauri ilituma maombi maalum ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. Hadi sasa shilingi milioni 300 zimetolewa na kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 1.07 na kazi zinazoendelea ni kuimarisha mifereji katika barabara zilizokamilika.

Ufuatiliaji wa fedha shilingi milioni 300 unaendelea ili kuendelea na ujenzi wa barabara kilomita 1 kiwango cha lami ikiwemo barabara ya Salmin na Lumumba iliyoko katika Kata ya Itende. Barabara zilizojengwa ni kama zifuatazo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (i) | Mtaa wa Msikiti | | km. | 0.450 |
| (ii) | Mtaa wa Kanisa Katoliki | | km | 0.310 |
| (iii) | Mtaa wa Mwenge | km | 0.165 | |
| (iv) | Mtaa wa Faraja | | km | 0.145 |
| | **Jumla** | **km** | **1.070** | |

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 Halmashauri ya Manispaa ya Singida imeidhinishiwa shilingi milioni 745 toka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga barabara za Halmashauri, hususan za Manispaa ikiwemo ya Singida kwa kiwango cha lami kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba ombi la Manispaa ilikuwa ni shilingi milioni 600 na wameshatuma shilingi milioni 300. Na kwa kuwa katikati ya Manispaa barabara ni nyingi na Mheshimiwa Mbunge wa jimbo amejitahidi kuweka taa za barabarani mji wote. Na kwa kuwa barabara za lami bado nyingi ambazo hazijatengenezwa mjini kati ili hadhi ya taa hizo ziendane na barabara. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuwaambia wananchi wa Singida Mjini kwamba kupitia Bajeti hii shilingi milioni 300 zilizobakia zitatengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mbunge Dewji kwa kazi

nzuri ambayo ameifanya katika Manispaa ile ya Singida na wenzake wote ambao anashirikiana nao.

Leo asubuhi nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya Paschal Mabiti wananchi wa Singida wenyewe wanasema wanamshukuru sana Rais kwamba ametekeleza ahadi yake kwa maana ya kazi iliyofanyika pale na ndiyo maana tumezungumza hapa. Shilingi milioni 300 ambazo zinadaiwa hakuna ubishi hapa huwezi ku-*debate* hapa maelekezo ya Rais, sina ubavu huo. Hizo fedha tutazitafuta tutazipeleka pale kwenda kumalizia kazi iliyobakia pale. Hapa sisi tunatekeleza maelekezo ya Rais kama ilivyotamkwa.

Kwa hiyo Mheshimiwa Diana Chilolo uwe na amani moyoni mwako. Hii kazi itafanyika, tena itafanyika vizuri mpaka mwenyewe utafurahi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri kuonyesha dhamira ya kufuatilia ahadi za Rais. Kwa kuwa swali la msingi lilitokana na ahadi ya Rais aliyoitoa kwenye Mkutano wa hadhara na kwa kuwa kwa *spirit* hiyo hiyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya kufuatilia kwa karibu ahadi za Mheshimiwa Rais.

Je, Naibu Waziri yuko tayari vile vile kufuatilia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 24 Mei, 2010 aliyoitoa kwenye Mkutano wa hadhara Kimara Mavurunza ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kimara mpaka Segerea kupitia Bonyokwa ambayo iko chini ya Manispaa inayounganisha Manispaa mbili za Kinondoni na Ilala yeye kama Kiongozi wa TAMISEMI?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kabisa kwamba kila akisimamishwa hapa kila mmoja atasema kwamba kuna ahadi za Serikali kwa maana ya Rais. Nimesema na juzi tumejibu tena hapa sisi hapa hatumfuati Rais tukamwambia fedha ziko wapi. Rais ameshapitisha bajeti tumeileta hapa ndiyo hii. Nyie tusaidieni kupitisha bajeti hapa, ndiyo kazi inayotakiwa hapa. Sisi tuna orodha na kitabu kimetengenezwa cha ahadi zote zilizotolewa na Rais nchi nzima. Kama nilivyosema Rais akishatoa ahadi sisi kazi yetu ni kutekeleza ahadi za Rais.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika kama unataka tukitoka hapa twende Ubungo ili unipeleke kwenye hiyo barabara lakini nitakwenda kuangalia kwenye Bajeti yenu nyinyi kama mmeliangalia hili ili tuweze kujua jinsi tutakavyofanya. Lakini nataka nimthibitishie kwamba hatuna tatizo na ahadi yoyote iliyotolewa na Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali lililofuata nalo linaulizwa na Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa tena kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Na. 66

**Mikoa Mipya Kuanza Kazi Rasmi na Wakuu wa Mikoa Kuteuliwa**

**MHE. VICK P. KAMATA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais ameridhia kuanzishwa kwa Mikoa mipya ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Geita; wananchi wa Geita wameupokea uamuzi huo kwa furaha na matumaini makubwa sana.

(a) Je, ni lini Mikoa hiyo itaanza kazi rasmi na Viongozi wa Mikoa kuteuliwa?

(b) Je, Serikali imejiandaa vipi kuiendeleza Miji Mikuu ya Mikoa mipya katika maeneo ya huduma za kijamii, kiuchumi na miundombinu ambayo awali ilikuwa Miji Mikuu ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba wakati Serikali inatangaza kuanzishwa kwa Mikoa na Wilaya mpya ilikuwa ni kusudio la kuanzisha maeneo mapya ya utawala ambayo hatimaye yatawezesha kuanza rasmi kwa Mikoa na Wilaya hizo. Hatua iliyokwishafikiwa ni kuhakiki mipaka ya maeneo yote yanayopendekezwa kuanzishwa ikiwa ni pamoja na wananchi wa maeneo hayo kushirikishwa kuhusu dhamira hiyo ya Serikali.

Hivyo, Mikoa na Wilaya mpya zitaanza rasmi Serikali itakapotoa Tangazo la kuanzishwa kwake *(Government Establishment Notice).* Uteuzi wa Viongozi na watumishi utafanyika zitakapokamilika taratibu za kisheria za uanzishaji Mikoa na Wilaya. Aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa Mheshimiwa Rais Mamlaka na Madaraka ya kuanzisha mamlaka mpya za Wilaya na Mikoa kwa wakati na namna ambavyo atakavyoona inafaa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi huduma za kijamii, kiuchumi na miundombinu katika maeneo yanayohusika, Serikali, Benki ya Dunia pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo imeandaa Mpango wa Muda Mfupi na wa Kati wa uendelezaji wa Majiji 3, Manispaa 15 na Miji Midogo 14 nchini. Geita ni moja ya maeneo ambayo yamefanyiwa maandalizi ya ukuaji wa Miji yenye hadhi ya Makao Makuu ya Mkoa. Shughuli zitakazozingatiwa ni pamoja na upangaji Miji, mazingira na usafi, barabara, mifereji na uboreshaji wa mapato ya Miji hiyo.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa taarifa zisizo rasmi ilikuwa inafahamika kwamba kuanzishwa kwa mikoa hii kunasubiri Bajeti. Je, hiki kigugumizi cha Serikali ni kwa sababu hakuna fungu maalum lililotengwa kwa ajili ya kuanzishwa kwa mikoa hiyo?

Pili, je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Geita waliokuwa na matumaini makubwa sana ya kuanza kupata huduma zao za kimkoa na sasa kumbe uanzishaji wa mikoa hii unasuasua? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nafikiri ujibu tu kwa mikoa yote ambayo inaanzishwa kwa utaratibu huo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama Mbunge mpya wa Viti Maalum anayekuja hapa. Nampongeza kwamba anafuatilia mambo haya kwa karibu sana. Yaani kwa kweli hilo hatuna tatizo nalo tunampongeza kwamba anafuatilia ni Mbunge wetu anatoka kule Geita.

Yeye hakupata nafasi ya kuwa Mbunge wa Viti Maalum ni kwa tiketi ya Geita, sasa huko ni kusuasua. Yaani mkoa ule wa Geita ambao unazungumzwa hapa na ndio umemleta humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Vicky Kamata nataka nikuthibitishie Rais tumemsikia, Waziri Mkuu tumemsikia, Mkuchika tumemsikia sisi wote Taifa zima tumesikia lile lilikuwa ni kusudio linatolewa *notice* yake. Sasa kuna *establishment* ukiingiza voti humu ndani Mheshimiwa Mkulo atakuambia hivi, vipi sasa. Kwa maana yake Rais ndiye mwenye mamlaka na madaraka kama tulivyosema. Sasa sisi tunamsubiri Rais yeye ndio mgawa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hapa maandalizi yote ukishasema kwamba unaanzisha mkoa na Wilaya kama alivyosema hakuna mtu anayebishana hapa tunachokwenda sisi ni kufanya.

Kama ni Waziri wa Fedha anafanya yale yanayomhusu, aliyekuwa TAMISEMI anafanya yale ambayo yanamhusu na wale wengine wote tulioko Serikalini kila moja anajipanga akijua kwamba Rais ametangaza kwamba ana kusudio na kuanzisha mikoa mipya pamoja na Wilaya mpya.

Nataka nilithibitishie Bunge hili kwamba wala msiwe na wasiwasi wala msiwe na hofu sisi tunachosubiri hapa ni mwenyewe mwenye mamlaka na madaraka akishasema tayari mtaona sisi tutakavyokimbiakimbia hapa na nataka niseme *serious* na hali ya juu sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kulieleza kidogo hili baada ya Naibu Waziri kulieleza vizuri tu. Najua ni eneo ambalo bado watu wanaliulizia sana na wengine wanapata hata mashaka pengine Serikali imedanganya, hapana.

Kama alivyosema Naibu Waziri mchakato wa kuanzisha una hatua mbalimbali za kisheria hasa ile ya kwanza ni Rais mwenyewe kuonyesha nia yake njema ya kutaka kuanzisha maeneo mapya. *(Makofi)*

Tunayo hatua ya pili ambayo itatangazwa hivi karibuni hiyo itatoa nafasi kwa wananchi sasa kutoa maoni yao ya mwisho kabla Rais hajaanzisha mkoa wenyewe. Hiyo hatua ni muhimu sana kwa sababu tusingependa kuonekana kwamba tumeshurutisha kuanzishwa kwa eneo lolote na hasa suala la Makao Makuu. Tukishamaliza hatua hiyo basi kinachofuata ni tangazo la mwisho na hilo ndilo linatuwezesha kuanzisha hiyo mikoa.

Sasa suala la lini, nadhani itategemea kwa sehemu kubwa tutapata maoni ya wananchi ndani ya muda mfupi kiasi gani, lakini kawaida huwa ni siku 60.

Kwa hiyo tukipata kabla ya hapo basi mkoa itaanza mapema pamoja kwa ajili ya Wilaya zake. Lakini nataka nimtoe wasiwasi na natoa wasiwasi Watanzania wote Waziri Mkuu mwenyewe naye mdau, kwa hiyo hakuna namna ambavyo tutaliacha hili lisifanyike kwa sababu na mimi ningependa mkoa ule wa Katavi kwa kweli uanze. Kwa hiyo nataka kuwahakikishia kwamba mchakato unaendelea tukimaliza mambo yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Suala la fedha kwa kawaida kwa kuwa ni la kisheria huwezi ukatenga fedha kwa jambo ambalo halijaanzishwa rasmi kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, taratibu zilizofanyika ilikuwa ni kutengeneza mfumo utakaowezesha fedha hizo kubaki ndani ya Wizara ya Fedha yenyewe katika fungu la kawaida kati ya mafungu ya Serikali ili Rais atakapokuwa ameridhia utengenezwe utaratibu sasa wa namna tutakavyoweza kuzitumia fedha hizo kama ilivyokuwa imepangwa.

Sasa kama kutakuwa na ulazima wa kuja Bungen,i sawa, kama hakutakuwa na haja kwa sababu zimeshakuwa *budgeted for* basi na yenyewe itaeleweka baada ya hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu hayo ambayo yametosheleza katika swali hili.

Waheshimiwa Wabunge baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa tutaondoka kwenye swali hilo tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka na linaenda Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Na. 67

**Eneo la Cheju, Kikungwi na Unguja Ukuu**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Licha ya kuwa wananchi wanaishi na kujitafutia riziki katika maeneo ya Cheju, Kikungwi na Unguja Ukuu kuna baadhi ya maeneo yamewekwa mabango ya JWTZ yakionyesha kuwa maeneo hayo ni yao:-

Je, kuna utaratibu gani uliofikiwa kuhusu maisha ya wananchi wanaoishi katika maeneo hayo pamoja na mali zao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Cheju, Kikungwi na Unguja Ukuu ni eneo linalotumika kufanyia mafunzo ya kijeshi kwa *Brigade* ya 101. Eneo hilo lilitolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ili wafanyie mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waliopo karibu na eneo hilo walikuwa wanaomba kuruhusiwa kulima mazao ya muda mfupi kila mwaka. Baadhi ya wananchi walitumia fursa hiyo kujenga vibanda vya kulindia mazao yao na sasa wanataka kuweka makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ hivi sasa limechukua hatua ya kuweka mabango ya ilani katika mipaka ya eneo hilo ili wananchi waweze kuitambua mipaka. Hali hiyo isitafsiriwe na baadhi ya wananchi kuwa wananyang’anywa maeneo kwa vile tu walikuwa wameruhusiwa kulima mazao ya muda mfupi na wameyatumia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi limechukua hatua ya kudhibiti maeneo yake ili kuzuia uvamizi na ujenzi haramu.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwa kuwa maeneo hayo Marehemu Karume baada ya Mapinduzi alituambia wananchi kwamba atafanya mazoezi kwa muda tu. Na kwa kuwa maeneo haya wananchi hivi sasa wana miji yao kama miembe, minazi, miembe isiyopungua miaka 120 hata Marehemu Karume hajazaliwa.

Je, huoni kwamba huu ni ushahidi wa uhakika kwamba wananchi hawa sasa Jeshi limewadhulumu ardhi yao na kuimiliki pasina sababu ya msingi?

(b) Naelewa wazi kwamba Zanzibar hakuna maeneo ya kutosha kwa mazoezi ya kijeshi na wananchi hawa wamekwishatupa nguvu zao na kurithi maeneo haya kwa wazee wao, huoni kwamba sasa na hili siyo lengo la nchi yetu kurejesha wananchi wake nyuma na kwa sababu hii inaonesha wazi kwamba wananchi sasa wanarudishwa nyuma kimaendeleo.

Je huoni kwamba hii ni kuwadhalilisha Wananchi wa Chejo, Kikungwi, Unguja Ukuu, kwa Jeshi kuchukua eneo hili?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapotoa eneo kulipatia Jeshi haitoi kwa muda. Inaipa Jeshi kwa madhumuni yaliyokusudiwa ya mazoezi, mazoezi hayawezi yakawa yanafanyika kwa muda, Isipokuwa tu utaratibu ni kwamba Jeshi linapopewa eneo la wananchi taratibu za kufidia wananchi wale hufanyika. Kwa hivyo ninachoweza kusema hapa ni kwamba tutaangalia endapo wananchi waliopo pale walifidiwa na kama hawajafidiwa basi taratibu za kuanza utaratibu wa kuwafidia zitafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwadhalilishi wananchi hawa, Jeshi lipo pale kwa manufaa ya wananchi kwa sababu linatoa ulinzi wa Taifa na kwa maana hiyo ningeomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuwaelimisha wananchi kwamba majeshi yetu yapo katika maeneo mbalimbali ya nchi hii kwa madhumuni ya kutoa ulinzi wa Taifa letu na hakuna dalili ya kwamba Serikali inataka kuwadhulumu wananchi na kila mara endapo maeneo ya wananchi yanachukuliwa basi ni wajibu wa Serikali kulipa fidia na hilo litafanyika.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kunipa nafasi, naomba kumwuliza Waziri kama ifuatavyo:-

Kwa sababu maeneo ya Majeshi sasa yamekuwa karibu sana na wananchi na kutokana na uzoefu wa milipuko iliyotokea Mbagala na maeneo mengine ya Tanzania;

Je, haoni sasa vituo vya Jeshi vilivyopo karibu na wananchi kama kile cha Mtwara Mjini kikahamishiwa mbali na mazingira ya wananchi ili kupunguza matatizo yeyote yanayoweza kutokea kama milipuko ya mabomu yaliyotokea Mbagala na kwingineko? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi linaweka vikosi vyake katika maeneo ambayo ni *strategic* kiulinzi. Maeneo haya hayawekwi tu kwa sababu yapo, yanawekwa pale kwa sababu maalum za kiulinzi.

Lakini lipo swali ambalo linaulizwa katika Mkutano huu wa Bunge ambalo litalijibu kwa kina ni mipango gani iliyopo kuhusu suala hili la makambi kuwa karibu na wananchi. Ninachoweza kusema ni kwamba mara nyingi wananchi ndiyo wamekaribia

kambi siyo kinyume chake na kiutaratibu inatakiwa wananchi wawe angalau kilomita moja kutoka Kambi za Jeshi zilipo, hiyo ndiyo inaitwa *buffer zone*.

Kwa hiyo taratibu zitachukuliwa ili kuhakikisha kwamba suala hili sasa linarekebishwa kutokana na uzoefu ambao umepatikana wa athari zinazoweza kutokea wananchi wakikaribia sana makambi haya.

Na. 68

**Uvamizi wa Maharamia.**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza**:-**

Kuna ongezeko kubwa la maharamia wa Kisomali katika mwambao wa Bahari ya Hindi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujilindaa na maharamia hao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maharamia wa Kisomali wamekuwa wakifanya mashambulizi kwa meli za biashara na uvuvi mfululizo katika mwambao wa Tanzania kwa muda mrefu sasa. *(Makofi)*

Hivyo JWTZ likiwa walinzi wa mipaka ya nchi yetu linaendelea na operesheni ya kuwasaka na kuwakamata maharamia wanaojihusisha na matukio ya utekaji meli katika mwambao wa Tanzania, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujilinda na maharamia, JWTZ linatekeleza yafuatayo; linafanya doria baharini kwa kutumia meli za kivita, linaimarisha ulinzi baharini katika maeneo ya vitalu vya utafiti wa gesi na mafuta na linafanya kazi ya kusindikiza meli za biashara pindi zinapoingia katika eneo letu pale linapoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ linashirikiana na nchi jirani za ukanda wa bahari ya Hindi kama Kenya, Msumbiji, na Afrika Kusini katika ubadilishaji wa habari kuhusu maharamia. Aidha, Jeshi limeanzisha mawasiliano na nchi rafiki ili kukamilisha mpango wa kuzitambua meli *automatic identification system* (*AIS*) katika mwambao wetu ili kufuatilia nyendo za maharamia baharini. Mchakato wa uwekaji wa mitambo hiyo upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ linashirikiana pia na mataifa yenye meli za kivita katika ghuba ya Aden yapatayo takribani 27 ambayo yanaendesha operesheni maalum ya mapambano dhidi ya uharamia kwenye pembe ya Afrika (Operesheni ATLANTA). Ushirikiano huo unahusu kutoa mafunzo na mbinu za kupambana na maharamia baharini.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni meli ngapi ambazo zimewahi kutekwa katika mwambao wa bahari yetu, na kama kuna meli ziliwahi kutekwa;

Je, maharamia hawa walipatikana na walipewa adhabu gani?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi operesheni zimeanza maharamia wamefanya majaribio ya kuteka meli 30, kati ya hayo matano yalifanikiwa na 25 yalizuiliwa.

Maharamia waliokamatwa ni kumi na mbili na kesi zilizopo mahakamani mpaka sasa ni tano. Bado hakuna kesi ambayo imemalizika.

Na. 69

**Kiwanda cha Korosho-Lindi**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Kiwanda cha Korosho cha Lindi kiliuzwa kwa Kampuni ya *BUCCO* lakini hadi leo hakifanyi kazi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukirejesha Serikalini na kutafuta mwekezaji mwingine atakayeanzisha uzalishaji na kutoa ajira kwa wakazi wa Lindi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *BUCO Investment Holdings* (T) iliuziwa viwanda viwili vya korosho, kiwanda cha Lindi na cha Masasi mwaka 2005. Taarifa tulizonanzo ni kwamba kampuni ya *BUCO Investment Holdings (T)* ina kesi mahakamani

kufuatia mgogoro wake na benki ya *CRDB* kutokana na mkopo uliokuwa umetolewa na benki hiyo kwa ajili ya uwekezaji katika kiwanda cha Masasi na kiwanda cha Lindi ziliwekwa kama dhamana. Hali hiyo imeikwamisha kampuni ya *BUCO Investment Holdings (T)* kuendelea kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafuatilia kwa karibu mwenendo wa mgogoro wa *BUCO Investment Holdings (T)* ulioko mahakamani na kwamba maamuzi ya kisheria ya mahakama kuhusiana na mgogoro huo yataiwezesha Serikali kuchukua hatua muafaka dhidi ya kampuni ya *BUCO Investment Holdings (T)* kuhusiana na kiwanda cha Lindi.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema ikafahamika kwamba kesi hiyo ipo Mahakamani kwa muda gani sasa?

(b) Kwa kuzingatia uchumi wa Taifa na maslahi ya Umma, Je, hakuna kipengele chochote cha sheria ambacho hali kama hii inapotokea kuna jambo gani ambalo linapaswa kufanyika ili kuweza kufanya hali ya uchumi na wakazi wa Lindi wakaendelea kupata ajira?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikumbuki tarehe kamili ambayo kesi imepelekwa mahakamani nitamtafutia tarehe hiyo, lakini najua kesi ipo mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipengele kinachoweza kuingia hapa, naomba niseme kwamba si rahisi kwa kweli. Mhimili mmoja kuingilia mhimili mwingine, kwa sababu kesi ile iko mahakamani itakuwa ni kinyume cha sheria Serikali sasa kuanza kuzungumzia habari zilizopo mahakamani na kutengua, mpaka mahakama itakapokuwa imetoa uamuzi, baada ya hapo tutachukua hatua ambazo zinastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tutakazochukua ni kwamba tunacho chombo cha *Consolidated Holding Cooperation* ambacho kitakwenda kukagua kiwanda kile kama matumizi yanayoendelea sasa hivi ni yale ambayo yaliyokusudiwa, ninaelewa kabisa kwamba malalamiko ya wananchi wale ni kwamba kiwanda sasa kimesimama walikuwa wanatarajia kupata ajira na sasa hawapati, lakini si rahisi kwa kweli kuingilia muhimili ambao unafanya kazi wa mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi ukitoka Serikali nayo itaanza kuchukua hatua. *(Makofi)*

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti matatizo yaliyotokea Lindi kwa kiwanda kuuzwa kwa kampuni ya *BUCO* yametokea pia Mkoa wa Kilimanjaro ambacho kiwanda cha magunia kiliuzwa kwa mwekezaji binafsi. Kiwanda cha *Machine Tools* nacho kimefungwa, kiwanda cha ngozi nacho hakifanyi kazi kwa kiwango cha kutosha.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kumpa Mwekezaji mwenye uwezo kwa ajili ya kuweza kuzalisha ajira kwa ajili ya vijana wetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anavyosema Mheshimiwa Betty Machangu ni kweli kwamba kuna baadhi ya Viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa vikapewa baadhi ya Wawekezaji, wengine wamefanya vizuri na wengine wamefanya kwa wastani lakini kuna wengine ambao hawajafanya vizuri kama vile ambavyo ameainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti Wizara yangu imefanya tathmini na taarifa kamili imepatikana, lakini tumerudi pale pale ambapo Naibu Waziri wa Kilimo alikuwa anazungumza sasa hivi kwamba baada ya taarifa ile kukamilika tumeupeleka kwa *Consolidated Holdings Company* ambao ni warithi wa *PSRC* ambayo ndiyo waliingia mkataba nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wawekezaji wote hawa, ambao wanaweza wakaangalia vipengele vya sheria vyote ambavyo vimekiukwa kama kuna ambavyo vimefuatwa wanaweza wakaviangalia, baadaye sasa kuona kama kuwapeleka mahakamani au kurudisha Serikalini kwa ajili ya taratibu za kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawasubiri *PSRC*, tunawashukuru kwamba Waziri wa Fedha ametangaza kwamba *CHC* wanaongezewa muda wa kuendelea kufanya kazi ili wakamilishe pamoja na kazi hii ambayo tunaitegemea ya kutoa tathmini ya kisheria kuhusu viwanda hivi ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa havijafanya kazi sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwa na subira. *(Makofi)*

Na. 70

**Agizo la Kupunguza bei ya Sukari –Kagera**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mkoa wa Kagera mwezi Machi mwaka huu 2011, aliagiza pamoja na mambo mengine hatua Fulani zichukuliwe ili bei ya sukari ipunguzwe iwe chini au sawa na maeneo ambapo sukari haizalishwi.

(a) Je, hatua hizo ni zipi na je, zimechukuliwa?

(b) Je, bei ya sukari Kagera imepangwa kiasi cha kulingana na bei ya maeneo mengine au chini zaidi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu la kutaka bei ya sukari katika maeneo yanayozunguka viwanda vya sukari iwe chini au sawa na maeneo mengine, kiwanda cha sukari cha Kagera kimeanzisha utaratibu mzuri wa kujenga mahusiano na Wafanyabiashara wa sukari wanaozunguka Kiwanda hicho na kuwauzia wafanyabiashara wa sukari kwa shilingi elfu sabini na mbili (72,000) kwa mfuko wa kilo hamsini sawa na shilingi 1,440 kwa kila kilo moja.

Hali hiyo inawezesha wafanyabiashara wa rejareja kuuza kwa bei ya chini ya shilingi 1700 kwa kilo ambayo ndiyo kiwango cha juu kilichokubalika baina ya wazalishaji, wasambazaji na Serikali, na hivyo kuwezesha jamii zilizo jirani na kiwanda kupata sukari kwa bei ya chini. Aidha, kiwanda kimeweka utaratibu wa kuwagawia wafanyakazi wake wote kilo tatu za sukari kila mwezi na tumeruhusu wafanyakazi hao kununua sukari kilo mbili zaidi kila mwezi kiwandani kwa bei ya shilingi 1400 kwa kilo. Kutokana na utaratibu huo, jamii yote inayozunguka kiwanda inakuwa na uhakika wa kupata sukari na kunufaika na punguzo hilo la bei. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na agizo la Serikali kuhusu bei elekezi ya sukari ya shilingi 1,700 kwa kilo, Mikoa yote ikiwemo Mkoa wa Kagera haitakiwi kuuza kwa bei inayozidi kiwango hicho ambacho ni cha juu. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara yangu imekua inakusanya taarifa za bei mbalimbali za bidhaa muhimu ikiwemo sukari. Kwa mujibu wa taarifa za bei tunazokusanya, bei ya sukari katika Mkoa wa Kagera imezingatia agizo hilo na wafanyabiashara walio wengi wamekuwa wakiuza sukari kwa bei isiyozidi shilingi 1700 kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zinaendelea kufanyika kati ya Serikali na wadau mbalimbali wa sekta ya sukari, ili kusaidia kuongeza uzalishaji wenye tija katika viwanda ili bei ya sukari iendelee kushuka na kuwawezesha wananchi wa kawaida wa Mkoa wa Kagera na Mikoa mingine ya Tanzania kuweza kumudu kununua bidhaa hiyo muhimu. *(Makofi)*

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri yanatia matumaini kwa wananchi, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, bei ya sukari ilipanda kutokana na hujuma za walanguzi kuhodhi sukari na kupandisha bei isivyo halali, na wakifanya hivyo kulikuwa na vyombo vya Serikali Mikoani , kuna Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakurunguzi kuna Afisa Biashara walikuwa wapi kudhibiti hali hii isijitokeze na wamechukua hatua gani kwamba hali hii isijitokeze.

(b) Ni hatua gani zinachukuliwa sasa kuhakikisha kwamba sukari inaingia katika orodha ya bidhaa zilizopo katika wakala wa Taifa wa chakula *National Food Reserve Agency* ili bei ya sukari idhibitiwe na isipande tena?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili la Walanguzi ningependa kwa ufupi tu niseme tu kwamba kilichofanya bei ya sukari ikapanda mwaka huu kuliko miaka mingine ni kuongezeka kwa bei ya sukari katika soko la dunia. *(Makofi)*

Bei ya sukari kutoka soko la dunia imeongezeka kutoka dola mia mbili na thelathini na tano kwa tani hadi dola mia nane na hamsini mpaka mia tisa kwa tani. Mafuriko yaliyotokea Pakstani na Brazil ndiyo yamesababisha bei hiyo kupanda. Na kwa sababu hapa nchini kwetu viwanda vina utaratibu wa kuacha kuzalisha sukari kuanzia mwezi wa kumi na mbili mpaka mwezi wa sita wale wenye vianda na wasambazaji wakubwa walipoona kwamba bei ya sukari kutoka Nje ni kubwa wakaona kwamba kuna umuhimu wa kulimbikiza ile sukari ili wakati huu ambapo hakuna nyingi waweze kujipatia faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo Serikali ililiona Waziri Mkuu akaitisha mkutano wa wadau wote wazalishaji na wasambazaji na Wizara husika na Bodi ya Sukari na katika Mkutano ule ndipo ambapo ilikubaliwa kwamba suala la kuhodhi sukari halitakiwi, na wale ambao walikuwa wamehodhi sukari wakakubali kuisambaza na Serikali ikatoa vibali vya msamaha mkubwa kwa wale ambao wangeweza kuingiza sukari ambazo ni tani elfu hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya sukari ile kuanza kuingia tukaona kwamba mabadiliko makubwa yametokea kwa wenye viwanda, kwa wasambazaji wakubwa lakini tukapata changamoto kwa *retailers,* wale wafanyabiashara wadogowadogo katika mitaa yetu na katika vijiji vyetu.

Waziri Mkuu alitoa agizo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri zetu waanze kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanakiuka bei hiyo elekezi wanachukuliwa hatua katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na kunyang’anywa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Wizara ni kwamba walio wengi wameweza kufanya lakini bado kuna changamoto kwamba kuna wafanyabiashara wadogo wadogo wengine ambao hawajaweza kufikia kile kiwango.

Serikali inaendelea kuwaomba Wakurugenzi na nitumie fursa hii kuwaomba Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Mikoa kama ambavyo Waziri Mkuu ameagiza wasimamie kwa makini suala hili.

Tunafahamu hapa Bungeni kwamba Halmashauri zetu kuna zingine ambazo zinafanya kazi vizuri sana, kuna zingine ambazo kidogo kuna changamoto. Mimi naomba

Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane sote sasa tuhakikishe kwamba kwa kweli utekelezaji wa suala hili katika Halmashauri zetu unafanyika.

Tuko Bungeni hapa lakini tuko na Madiwani wetu tunawasiliana nao kwa vizuri, tuko na Wakurugenzi wetu tuhakikishe kwamba ingawa *by laws* zinapitishwa kuhakikisha hili linatekelezwa.

Sasa hili la kuingiza sukari katika bidhaa muhimu kama vile vyakula muhimu ni wazo zuri na Wizara yangu kwa kweli inatafakari namna gani ya kushauri Baraza la Mawaziri tuone kama kuna umuhimu au kuna uwezekano wa kuliingiza kama bidhaa muhimu ambayo itakuwa inadhibitiwa kama vile mafuta au kama vile bidhaa hizi za mawasiliano kwa maana ya simu. Sasa ufumbuzi wa kudumu kabisa wa suala hili kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na uzalishaji wa kutosha sukari ikishakuwa nyingi katika nchi yetu na bei itashuka hakutakuwa na sababu za kuingilia kwa maana za kiutawala. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee majibu yamekuwa marefu sana na niwaomba Waheshimiwa Mawaziri angalau majibu yawe mafupi tupata maswali ya nyongeza mengi.

Na. 71

**Mgogoro wa Mpaka Kati ya Hifadhi ya Saadani na Vijiji Vinavyoizunguka Hifadhi Hiyo**

**MHE. SALEH AHMED PAMBA** aliuliza:-

Serikali imeanzisha Hifadhi ya Saadani, kwa madhumuni ya kuhifadhi wanyamapori ili kukuza utalii na maendeleo ya Wilaya ya Pangani kwa ujumla, lakini kumekuwepo na migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vya Mkalamo, Boza na Mahunguru.

Je, Serikali iko tayari kuangalia upya mipaka kati ya hifadhi na vijiji tajwa hapo juu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Hifadhi ya Taifa ya Saadani ipo katika Mikoa ya Tanga Wilaya ya Pangani na Handeni na Mkoa wa Pwani Wilaya ya Bagamoyo. Hifadhi hii ilianzishwa tarehe 16 Septemba, 2005 baada ya kupandisha hadhi eneo la pori la akiba *(Game Reserve)* la Saadani. Katika Wilaya ya Pangani, hifadhi hii inapakana na Vijiji vya Mkalamo, Mbulizaga, Bunyuni, Mkwaja, Mikocheni na Sange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya Hifadhi ya Saadani kwenye Kijiji cha Mkalamo, ni ile ile iliyokuwa mipaka ya Pori la Akiba la Saadani na *Mkwaja Ranch*. Hakuna mabadiliko yaliyofanywa kwenye mipaka ya zamani ya maeneo haya wakati wa kuanzisha Hifadhi ya Saadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara haijawahi kupata kwa njia ya maandishi au kwa njia nyingine ikiwemo kupitia vikao malalamiko yoyote kuhusu tatizo la mpaka kati ya hifadhi na Kijiji cha Mkalamo, pamoja na vitongoji vyake vya Boza na Mahunguru. Vikao vya Ujirani Mwema hufanyika mara kwa mara Kati ya Hifadhi na kijiji hiki kujadili masuala mbalimbali ya kijamii pamoja na uhifadhi. Kikao cha mwisho kati ya Kijiji cha Mkalamo kilifanyika tarehe 30 Machi, 2011. Aidha, kwenye kikao hicho cha mwisho hakuna hoja yoyote iliyojitokeza juu ya mgogoro wa mpaka kati ya kijiji hicho na Hifadhi. Hata hivyo kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge, anatembelea wananchi wake na hili ni jambo jema sana nampongeza na yawezekana kabisa kwamba amepata na wananchi uwepo wa tatizo hili basi Wizara yangu inahakikisha tu kwamba haina tatizo la kuzungumza naye na wananchi katika ule mfumo tulionao wa ujirani mwema ambao tunafanya vikao mara kwa mara kuhakikisha kwamba tunapata ufumbuzi wa majadiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pamba hukusimama nimeshamtaja Mheshimiwa Akunaay, Mheshimiwa Salehe Pamba. Waheshimiwa Wabunge, suala likishajibiwa kama mwenye swali la msingi ana swali la nyongeza, anatakiwa kusimama papo hapo.

**MHE. SALEH AHMED PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunihurumia. Kwa kuwa jibu la Mheshimiwa Waziri, halifanani na hali halisi na kwa misingi hiyo ndiyo sababu nimeuliza swali namba 71 na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali kukutana na wana vijiji ambao wana matatizo ya mipaka na hifadhi hiyo.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri ataifanya ziara hiyo lini?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa idadi ya tembo katika hifadhi ya Saadani imeongezeka sana na hivyo kuvuka mipaka na kuleta uharibifu wa mali na mazao ya wana vijiji na kwa kuwa kumekuwa na madai ya kifuta machozi tangu mwaka 2005 kwa wanavijiji wanaozunguka hifadhi hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri atatoa kauli gani kuhusu madai haya ya muda mrefu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Pamba kwa kuwa kiungo kizuri sana katika Wizara yangu na wananchi wa jimbo lake. Ikumbukwe kwamba Mheshimiwa Pamba amekuwa kwenye Wizara yetu na hivyo anajua vizuri na hata mchakato huu anaujua vizuri jinsi ulivyokwenda. Kama nilivyosema kwamba tunakusudia kutatua migogoro yote ya mipaka kwa kushirikiana na wananchi kwa mazungumzo.

Kwa kuwa kuna shughuli zinazoendelea hapa Bungeni basi nimwombe Mheshimiwa Mbunge, mwenzangu kwamba tutakapokuwa tumemaliza kikao hiki

nitatafuta nafasi niweze kutembelea Mkoa wa Tanga na Wilaya ya Pangani kuzungumza na wananchi kuhusu tatizo hili.

Lakini hata hivyo nimwahidi tu kwamba hata kabla mimi sijaenda huko wakati kipindi hiki cha Bunge kinaendelea nitaongea na wenzangu wa Hifadhi ya Taifa *TANAPA* ili waweze kwenda kwenye kijiji hicho kuzungumza na kuanza kupata ufumbuzi wa awali kabla mimi kwenda huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vile vile kwamba kumekuwepo matatizo ya wanyama hawa kuharibu mazao ya wananchi kwenye maeneo mengi sana kwenye nchi yetu na siyo Pangani peke yake.

Kuna matatizo hata hivi tunavyozungumza kuna tembo wamevamia maeneo ya Bukoba Vijijini wanyama hawa wameharibu mazao Wilaya ya Rombo, Wilaya ya Bunda, hata hapa tu jirani Wilayani ya Kondoa. Kwa kujua tatizo hili kwa upande wetu sisi tumeongeza fedha kwa upande wa askari wanaofanya shughuli za kutoa wanyama hawa kwenye maeneo hayo.

Kwenye madai ambayo ni ya zamani tuliyapokea mwaka 2007 kwa bahati mbaya taarifa zilikuwa siyo kamilifu sana na kwa sheria ya wakati ule ilikuwa inalipa kwa ekari inayozidi ekari moja. Tulikuwa tunazidi *a fixed sum*, tulilipa shilingi milioni 2,400,000 kwa maeneo ambayo yalikuwa na sifa za kulipwa kwa vigezo vya wakati huo. Kwa sasa hivi kanuni zimeboreshwa kupitia sheria namba 5 ya mwaka 2009 tutakuwa tunalipa viwango tofauti zaidi.

Kwa hiyo, niombe tu kwamba Mheshimiwa Mbunge kwa hayo madai ya zamani kwa upande wetu ni kwamba tuliyalipa mwaka 2008 japo ni kiasi kidogo sana kwa sheria ya wakati ule lakini tuli-*settle*.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Niombe kwa lugha ya Bunge hapa ndani hawa tembo wanaitwa ndovu. Basi baada ya kutoa mwongozo wa jina hilo naomba sasa tuendelee na swali linalofuata.

Na. 72

**Migogoro ya Mipaka Kati ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na Wananchi**

**MHE. ROSE KAMILI SUKUM** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwepo na migogoro ya mipaka kati ya mamlaka za Hifadhi za Taifa na wananchi wa vijiji vinavyopakana na hifadhi hizo kutokana na mamlaka hizo kuvamia kwa nguvu maeneo ya wakazi wa vijiji hivyo vinavyopakana na Hifadhi hizo na kusababisha wakazi hao kupigwa na kujeruhiwa na wengine kufungwa jela bila kuwa na makosa.

Baadhi ya vijiji hivyo ni pamoja na Nyansorori, Buchungu, Twamchanga, Mbikiri vilivyopo Wilayani Serengeti na Hifadhi za Akiba za Ikorongo/Grumet ambazo zimesababisha baadhi ya wafugaji kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu baada ya kupigwa risasi na Askari wanaolinda hifadhi hizo.

Je, Serikali inalimbia nini Bunge kuhusiana na migogoro hiyo inayowanyima wananchi haki zao za msingi na ina mpango gani endelevu ya kumaliza tofauti hizo na kuwapa wananchi haki zao za msingi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kabisa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa vijiji alivyovitaja vipo Wilaya ya Serengeti na vinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambayo imeanzishwa kwa sheria ya Serikali namba 235 la tarehe 21 Juni, 1968 na kubainisha bayana mipaka ya maeneo yote ya hifadhi. Pia ni kweli kwamba kumekuwepo na migogoro mbalimbali ambayo inaendelea kujitokeza kati ya mamlaka ya Hifadhi za Taifa na wananchi wanaoishi kuzunguka maeneo hayo ya Hifadhi. Migogoro hiyo inasababishwa kwa kiasi kikubwa na wananchi wenyewe kutotambua mipaka halisi ya hifadhi na kutozingatia sheria ya Hifadhi za Taifa, jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kuendelea kutokea kwa migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008 Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Halmashauri za Wilaya ya Ngorongoro Meatu, Bunda, Bariadi Magu, Serengeti na Tarime iliendesha zoezi la uhakiki wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ili kila mdau aweze kuelewa mipaka halisi chini ya ardhi. Zoezi hilo lilifanywa baada ya kutolewa elimu kwa wananchi.

Kwa upande wa Wilaya ya Serengeti, Vijiji vya Bonchugu, Rwamchanga, Mbirikiri, Miseke, Merenga, Bisalala, Mbalimbali, Machochwe, Nyamakendo, Robanda na Nyasurura vilishiriki katika zoezi la utoaji elimu. Baada ya elimu kutolewa la uhakiki lilifanyika kwa kushirikisha viongozi wa vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya zoezi hilo maeneo yaliyokuwa nje ya Hifadhi yalirudishwa kwa wananchi. Uthamini na mazungumzo yanaendelea kwa kwa maeneo ambayo yapo ndani ya Hifadhi ili fidia iweze kutolewa na eneo liweze kuwa hifadhini. Wizara yangu imekuwa ikiwasisitiza wafanyakazi wakiwemo Askari kufuata sheria katika kutekeleza majukumu yao.

Inapotokea askari kavunja sheria hana kinga yoyote hatua za kinidhamu huwa zinachukuliwa. Aidha, wananchi wanaruhusiwa kutoa malalamiko yao ikiwemo kuwafungulia mashitaka pale ambapo askari wanakuwa wamekiuka sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi zetu na vijiji vinavyozunguka hifadhi, Serikali imetenga Bajeti maalum kwa ajili ya kufanya zoezi la uhakiki wa mipaka na kuweka alama za kudumu katika maeneo yote yanayozunguka hifadhi zetu katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Hivyo, namshauri sana Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kushirikiana na taasisi ya *TANAPA* pamoja na Wizara yetu ili kuweza kuweka mipaka hii na kuiheshimu.

**MHE. ROSE KAMILI SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba afahamu kwamba yeye alitoa semina kuhusu mipaka lakini mimi nimeuliza maswali ya msingi kwa hii migogoro imeanza siku nyingi kwa maana kwamba Serikali ilikuwa haitambui au haikuwashirikisha wananchi wanaohusika ili kuweka hiyo mipaka.

(a)Je, ni lini wananchi hao walishirikishwa kwenye mpango huo kabla ya kuweka hiyo mipaka wa mwaka 1968?

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwaeleza kwamba Serikali Kuu inaingiza mipango hiyo bila kuwashirikisha wananchi kwa mfano Ushoroba inapoanza kuweka wananchi hao hawakushirikishwa wale kupewa fursa yoyote wakati wananchi wanategemea kupeleka malisho yao wakati wa kiangazi kwenye maeneo hayo.

Je, Serikali inaingizaje mpango bila kushirikisha wananchi kwa kutumia sheria ya ardhi namba 4 na namba 5? Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa heshima kabisa nimjibu Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, suala kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika uainishaji wa mipaka. Niseme kwamba sheria anayoisema ya vijiji ni ya mwaka 1999. Hifadhi ya Serengeti ilianzishwa mwaka 1969 utaratibu wa wakati huo ulifuatwa vizuri kabisa.

Sasa hivi matatizo yameongezeka sana baada ya kuwa wananchi wameongezeka na shughuli za kibinadamu zikawa zimeongezeka. Lakini pia *description* ya mipaka ya wakati ule ilikuwa inatumia *land marks* kwamba mlima fulani, bwawa fulani. Sasa unaposema mlima, mlima unaweza ukawa na mteremko upande huu kilomita tatu na upande huu kilomita tatu. Kwa hiyo, *specific area* kwenye ule mlima inakuwa haijabainishwa. Kwa hiyo, tunachokifanya sasa ni kutengeneza mipaka kwa kutumia vipimo vya kisasa vya *GPS* na tunazungumza na wananchi kwamba mpaka tunaomba uwe hapa.

Kwa kweli kuna maeneo mengi ambayo dhahiri yanaonekana kwamba yako kwenye vijiji vya wananchi tunayarudisha. Mfano, mzuri ni eneo la Maharaka kwenye Jimbo la Mvomero kwa rafiki yangu Mheshimiwa Makala. Eneo lile lilikuwa likijulikana kwamba liko hifadhini sasa hivi tumeshawaambia wananchi kwamba liko kwenye eneo lao na waendelee na shughuli zao. Kwa hiyo, tunashirikiana vizuri katika kuweka vizuri mipaka hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge swali la msingi liliulizwa na Rose Kirigini, basi tumpe Rose Kirigini aulize swali la nyongeza. (*Makofi*)

**MHE. ROSE K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijiji vilivyotajwa katika swali la msingi vya Nyasololi, Buchungu, Rwamchanga, Mbikili nikiongezea na kijiji cha Pakinyigoti, migogoro hii imekuwa ni ya muda mrefu sana na pori la akiba la Gurumeti. Na kwa kuwa mimi binafsi kwa takribani miaka mitano nimekuwa nikifuatilia kwa karibu sana migogoro hii na kwa kuwa Wizara husika imekuwa ikitekeleza migogoro hii kupata ufumbuzi lakini suala lililobakia sasa ni kuunganisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi.

Je, Waziri yuko tayari kuiunganisha Wizara hii ili kuhakikisha migogoro hii inatatuliwa kwa haraka? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu kwamba kwa dhahiri kabisa Wizara kwenye maeneo ya ardhi tumekuwa tukishirikiana na Wizara ya Ardhi, tumekuwa tukifanya hivyo kwenye maeneo yote ambayo tumesema mazoezi ya uhakiki wa mipaka yanafanyika.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekuwa tukifanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo.

Na. 73

**Wananchi Kutozielewa haki zao na Sheria za Nchi**

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI** aliuliza:-

Ni haki ya kila mwananchi kujua na kuzitambua sheria na haki zao kwa ujumla:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu kwa umma ili wananchi waweze kuzielewa sheria za nchi pamoja na haki zao kwa ujumla?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa kila mwananchi kuzijua na kuzitambua sheria za nchi. Kwa kujua na kuzitambua sheria za nchi, mwananchi anakuwa katika nafasi ya kutovunja sheria za nchi na pia kujua haki zake.

Mheshimiwa Spika, Serikali kila mara imekuwa ikitoa elimu kwa Umma kuhusu sheria mbalimbali na shughuli zinazofanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara mbalimbali kupitia vyombo vya habari kwa mfano vipindi vya televisheni na radio.

Mathalan katika mwaka huu wa fedha, Wizara ya Katiba na Sheria imeendesha jumla ya vipindi 24 vya Televisheni na vipindi 23 vya Radio vinavyoelimisha sheria mbalimbali na haki za watu. Sanjari na hilo, Wizara yangu iliandaa na kusambaza vipeperushi vinavyoelimisha haki mbalimbali za raia. Aidha, Wizara ya Katiba na Sheria imekuwa ikishiriki katika maonyesha mbalimbali ambapo hutumia fursa hiyo kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kisheria. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara ya Katiba na Sheria, ilishiriki katika maonyesho ya Nane Nane yaliyofanyika Mkoani Dodoma ambapo wananchi walipata fursa ya kuelimishwa masuala mbalimbali ya kisheria na haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Katiba na Sheria imeandaa Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliana uliofadhiliwa na Mpango wa Maboresho wa sekta ya sheria. Mkakati huu utaanza mwaka ujao wa fedha 2011/2012. Ni imani yangu kuwa kupitia mpango huu wananchi watapata fursa pana ya kujua mengi kuhusu sheria za nchi na haki zao.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutambua mchango wa Chama cha Wanasheria wa Tanzania Bara, Chama cha Wanasheria Wanawake wa Tanzania na Asasi zingine zisizo za Kiserikali kwa kuunga mkono juhudi za Serikali za kuwaelimisha wananchi masuala mbalimbali kuhusu haki zao.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa njia zitumikazo kutolea taarifa hii haiwafikii walengwa ipasavyo kwa kutokufuatilia vyema vipindi vya radio na televisheni.

Je, Serikali iko tayari kuanzisha mtaala wa somo hili mashuleni? (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mitaala ya shule za msingi na sekondari na vYuo pamoja na Vyuo vikuu masomo haya yanatolewa. Kwa hiyo, tunategemea kwamba elimu hii inatolewa kwa njia hiyo. Lakini njia nyingine ni kwenye Halmashauri za wananchi na ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha wananchi kuhusu mambo mbalimbali hasa sheria ambazo zinawahusu zaidi wananchi ikiwa ni pamoja na Katiba.

Kwa msingi kwamba katika Ibara ya 26 ya Katiba ambayo inamtaka kila mwananchi kutii sheria za nchi. Kwa hiyo, kwa njia hiyo basin a ninyi pia mtakuwa mmetoa msaada mkubwa kwa kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mwanasheria Mkuu amesema kujua sheria ni kutii na kuwa katika Bunge lililopita, Serikali iliahidi kuleta marekebisho ya sheria ya ndoa ya mwaka 1971 hadi leo haijaletwa na kwa kuwa sheria hiyo inalinda maslahi ya wanawake kupunguza manyanyaso, kujua haki zake na hasa ukizingatia ile shilingi mia moja ya kutunza mtoto baba anapomtoroka mama inakuwa inaongeza idadi ya watoto wa mitaani.

Je, Serikali inasemaje katika Bunge hili?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliahidi kuleta hiyo sheria hapa Bungeni kama anavyosema Mheshimiwa Zaynab Vulu. Tukubaliane kwamba mchakato wa sheria ya ndoa pamoja na sheria ya mtoto, pamoja na mahakama za kazi ni jambo ambalo linapaswa kujadiliana kwa pamoja.

Kwa hiyo, wakati muafaka sheria hiyo italetwa Bungeni na ni wazi kwamba sheria ya ndoa ni muhimu sana katika jamii yetu na mimi mwenyewe ni mdau katika sheria hiyo. Kwa hiyo, wakati muafaka utakapofika sheria hiyo itakuja.

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mwanasheria Mkuu, lakini sio wewe mwenyewe tu ni wewe na mke wako wote ni wadau wa sheria hiyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge lakini hata hivyo, naomba tukumbushane kwamba sheria ya mtoto tayari tumeshaipitisha ndani ya Bunge hili na hilo suala la matunzo ya mtoto limeshashughulikiwa ndani ya sheria hiyo tuliyoipitisha Bunge lililopita la malezi bora kwa mtoto.

Kwa hiyo, tuwaelimishe wanawake wote wajaribu kufuatilia sheria hii, sasa hivi watoto wetu wanalindwa, ile shilingi mia moja haipo tena.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Swali Namba 74 kwa maelekezo ya Mheshimiwa Namelock Edward Sokoine, hayupo ameniagiza swali lake liulizwe na Mheshimiwa Livingston Lusinde.

Na. 74

**Uhusinao kati ya Tanzania na Israel**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE (K.n.y. MHE. NAMELOCK E. M. SOKOINE)** aliuliza:-

Tanzania iliwahi kuwa na mahusiano na nchi ya Israel ambayo ilitoa mafunzo kwa vijana wetu na JKT na kuwezesha kuanza shughuli za uzalishaji katika kilimo:-

(a) Je, ni nini kilisababisha uhusiano huo kuvunjika?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufaanya mazungumzo na israel ili kurejesha uhusiano uliopo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kumjibu Mheshimiwa Namelock Moringe Sokoine, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatia vita ya siku sita iliyotokea kati ya Israel na Misri mwezi Juni,1967 na kuiwezesha Israel kushinda vita hiyo na kuteka ardhi ya Misri ikijumuisha eneo la ukanda wa Gaza na Sinai Peninsula, Tanzania pamoja na nchi nyingine za umoja wa nchi huru za Kiafrika (OAU) zilivunja uhusiano na Israel, baada ya Rais Gamel Abdel Nasser wa Misri kuziomba nchi za Afrika kufanya hivyo.

Israel iliendelea kukalia maeneo hayo kwa ubabe kwa kipindi cha miaka 10 hadi Israel na Misri zilipowekeana mkataba wa amani uliosimamiwa na Marekani maarufu kama *Camp David Accord,* Septemba, 1978. Katika mkataba huo, Israel ilikubali kuondoka kwenye maeneo walioyokuwa wameyateka ya ukanda wa Gaza na Sinai Peninsula, na kwa upande mwingine Misri pamoja na nchi nyingine za kiarabu hasa Jordan na Syria zikatambua rasmi kuwepo kwa Taifa la Israel.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya suluhisho hilo, nchi nyingi za Afrika zilirejesha uhusiano wake na Israel. Tanzania ilirejesha uhusiano wake na Israel tarehe 23 Februari, 1995. Balozi wetu Misri ndiye anayewakilisha nchi yetu nchini Israel, na Israel inawakilishwa Tanzania na Balozi wa Israel nchini Kenya. Uhusiano wetu ni mzuri na unatawaliwa na misingi ya kuheshimiana na uhuru.

Uhusiano wetu na Israel haufuti uhusiano wetu na Palestina, na tunaendelea kuunga mkono madai ya Palestina ya kuwa nchi huru na kamili katika maazimio yote ya Umoja wa Mataifa.

Wizara mbalimbali za Serikali ikiwemo Wizara ya Kilimo zimekuwa na mawasiliano na Israel. Milango iko wazi kwa watu binafsi, mashirika yasiyo ya Kiserikali na taasisi za umma kuendeleza mahusiano haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante, swali la nyongeza Mheshimiwa Livingstone Lusinde a.k.a Bajaji.

**MHE. LIVINGSTON J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba uhusiano huo ulivunjika na sasa umerudi na kwamba Balozi wetu wa Misri ndiyo anaetuwakilisha Israel na Balozi wa Israel wa Kenya ndiye anaewakilisha Israel hapa Tanzania. Haoni kwamba ushirikiano huo bado wa mashaka?

Katika swali la msingi, Mheshimiwa Namelock alitaka kujua vijana wa JKT waliokuwa wakipelekwa mafunzoni Israel na kuja hapa kuja kujenga nchi yao vizuri kwa kujitegemea.

Je, Serikali haioni sasa kwamba vijana wanaomaliza JKT wakiachwa tu wazungunge mitaani ni hatari wengine wasiokuwa na imani wanaweza kujiingiza kwenye vitendo vya ujambazi? Wapatiwe kazi ikiwepo kuajiriwa katika kampuni mbalimbali za ulinzi. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza kwa nchi yetu kuwakilishwa Israel na Balozi wetu alioko Misri na kwamba Israel inawakilishwa na Balozi wake aliopo Kenya, hakuonyeshi kusuasua kwa uhusiano ni jambo la kawaida kwa sababu hakuna nchi hata moja ambayo inaweza kuwa na Mabalozi wake katika kila nchi, ni utaratibu wa kawaida kwa nchi kuwa na Balozi ambaye ana-*cover* eneo kubwa na anakuwepo katika *capital* katika eneo lile.

Kwa hiyo, Balozi wetu wa Misri ana-*cover* katika maeneo mengi kama zilivyo Balozi nyingine nyingine zinakuwa zinatuwakilisha katika nchi zaidi ya moja. Kwa hiyo, bado ni uhusiano mzuri na tayari kuna mahusiano ya Kibalozi na utaratibu kwamba anaku- *accredited to Tanzania* kama huyo Balozi wa Kenya. Kwa hiyo, ni Balozi wa Israel nchini Tanzania pia kama ambavyo Balozi wetu wa Misri ni Balozi wetu nchini Israel ingawa yuko Misri.

Kuhusiana na suala la vijana wetu kupelekwa Israel, suala halikuwa hilo, nafikiri suala lilikuwa ni kwamba wakati huo Israel ilikuwa inaunga mkono na kusaidia Kambi zetu za JKT, tumesema kwamba mahusiano yamerejeshwa na milango iko wazi, na hizi sasa kuna majadiliano ambayo yameanza kwa nchi zetu mbili kushirikiana katika maeneo ya ulinzi, lakini kuna taratibu amabazo zinafuatwa kwanza.

Kwa hiyo, inawezekana baadaye ikapelekea mahusiano hayo pia yakifikia kuendelea kutusaidia katika kambi za JKT, ahsante.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita, lakini ninaomba tumalize swali lililobakia moja ili tuweze kulikamilisha. Kwa hiyo, naomba tu turuhusu Mheshimiwa Ali Khasim Seif, Mbunge wa Mkoani aulize swali ambalo ni la mwisho katika siku hii ya leo. *(Makofi)*

Na. 75

**Ujenzi wa Maabara**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Miongoni mwa changamoto za walimu ufundishaji wa somo la Sayansi katika shule zetu.

Je, katika kipindi cha mwaka 2005-2010 zimejengwa Maabara ngapi na kupatiwa vifaa kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wahisani imefanikiwa kujenga jumla ya Maabara 419 ambapo Maabara 311 zilijengwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari awamu ya kwanza (MMES I) na Maabara 108 zilijengwa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Maabara 419 zilizojengwa ni Maabara 108 ambazo zilipatiwa vifaa kikamilifu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jawabu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kati ya Maabara 419 ni Maabara 108 yaliyopatiwa vifaa. Je, hizi Maabara 311 zitapatiwa vifaa lini?

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyooneka wanafunzi wengi siku hizi hawapendelei kusoma masomo ya Sayansi.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kupata Walimu bora katika masomo haya ya Sayansi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kutoka Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa anauliza maabara zilizokamilika na zile ambazo hazijakamilika kwamba zitapatiwa lini vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kwa kutumia mikakati yake ambaye imejiwekea kupata vifaa kwenye shule na maabara, hivi karibuni shirika la *URESCO* tumepata *micro science kit,* yaani Kiswahili maana yake vivunge zilizotolewa na shirika hilo ambazo zinalenga kuzipatia

shule mia moja themani (180) katika nchi yetu ya Tanzania kwa baadhi ya Mikoa, Kagera, Dodoma, Kilimanajro, Mwanza, Mbeya, Morogoro, Shinyanga na Tanga. Kila shule watapata *package* hiyo. Kwa hiyo, kwa ajili ya masomo ya Sayansi ambayo unaweza kufanya majaribio ya ndani pamoja na majaribio ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuna hakika baada ya miaka miwili tutaendelea kusambaza hizi package kwa ajili ya masomo ya Sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge angependa kujua mikakati ya Serikali katika kupata Walimu wa masomo ya *physics*, *chemistry* na *biology* yaani maana yake Walimu wa Sayansi. Kwa sababu vijana wengi siku hizi wanapenda kusoma masomo ya *Arts.* Lakini Serikali kwa kutumia mikakati mbalimbali tumeweza angalu mwaka huu kufanikiwa kuwapata vijana 35,450 waliojiunga Kidato cha Tano, lakini miongoni mwa hao, vijana 16,105 wanasoma masomo ya Sayansi yaani *combination* za *PCM,PCB,CBG,CBA* na kadhalika.

Vilevile ili kutouwa kada hii ya Diploma, mwaka huu Serikali imefanya mpango mkakati ambapo tumetafuta vituo vinne kwa ajili ya kwenda kuwapa pre-entry program vijana hawa ambao wanataka kujiunga kada ya ualimu kwa masomo ya sayansi na masomo mengine. Vituo vya Tukuyu, Morogoro, Kisuru na Butimba ambapo mimi mwenyewe nitakwenda kufungua mafunzo hayo Butimba huko Mwanza na wameanza masomo haya tarehe 1 Juni, 2011. *(Makofi)*

Masomo haya yanataka kuanzishwa miezi mitatu hii, kabla hawajaanza masomo ya Diploma kwa ajili ya masomo ya Sayansi na masomo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge nimewaomba radhi sana, muda wa maswali kwa kweli umepita na tumeufidia kidogo kwa sababu ya zile taarifa ambazo zilitolewa mwanzo nikaona ni suala la busara kama tutamaliza maswali yote.

Kwa hiyo, kabla hatujaendelea hapa nina matangazo machache, labda kabla sijatangaza Waheshimiwa Wabunge niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao wataanza kuchangia ajenda itakayofuata baada ya matangazo ili kama wako nje ya ukumbi waweze kurejea ndani.

Tutaanza na Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, tutafuatiwa na Mchungaji Msigwa, tutafuatiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono halafu tutaendelea na wengine. Kwa hiyo, kama hawapo ndani, ningeomba waanze kujianda kurudi ukumbuni.

Tangazo langu la pili, kwa mujibu wa Kanuni Namba 98 (1) (2) kinahusu utaratibu wa kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Serikali, sasa kifungu kile cha 2 ndiyo ninachotaka kukisema hapa, uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.

Sasa naomba niwatangazie kwamba tarehe 21 Juni,2011 siku ya Jumanne ndiyo itakuwa siku ya kuhitimisha Bajeti hiyo kwa kupiga kwa kutamka jina la Mbunge mmoja mmoja, nafahamu Waheshimiwa wengi *weekend* wangependa kurudi kwenye Majimbo yao na kufanya kazi zao za Kibunge kwa mujibu wa Katiba, lakini tafadhali sana kila Mbunge ajue kwamba siku hiyo ni siku muhimu sana kwa kila Mbunge kuwepo hapa Bungeni kwa ajili ya kuhitimisha shughuli hiyo ya Kikatiba. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo, naomba nitoe matangazo ya kikazi, nina taarifa za mikutano ya Kamati hapa. Kwanza kabisa kikao cha Kamati ya kudumu ya fedha na uchumi. Tafadhali naomba uwatangazie Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya fedha na uchumi kuwa leo tarehe 17Juni, 2011 mara baada ya Kuahirisha Kikao cha Bunge.

Sio baada ya kuhairisha Mheshimiwa Mwenyekiti ni kusitisha Kikao hiki cha Bunge mchana huu tunasitisha hatuhairishi. Mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa nane kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo na kitafanyika Ukumbi Namba 219, gorofa ya pili jengo la Utawala.

Tafadhali sana Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo mhudhurie katika kikao hicho muhimu sana.

Halafu nina taarifa ya Mkutano wa Chama cha Kibunge cha Maendeleo ya Idadi ya watu. Tafadhali naomba uwatangazie Wabunge Wote kuwa leo tarehe 17 Juni, 2011 saa saba mchana katika Ukumbi wa *basement* kutakuwa na Mkutano wa Wabunge wanaopenda kujiunga na Chama cha Kibunge na Maendeleo na Idadi ya watu (*Tanzania Parliamentary Association on Population and Development).*

Pia Mkutano huo utafanya Uchaguzi wa Viongozi wa Chama hicho. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenye *interest* na Chama hicho mnaombwa kukusanyika katika Ukumbi huo.

Lakini ninayo matangazo mengine hapa, tunao wageni wafuatao. Kwanza kabisa tuna wanafunzi ishirini na Walimu wawili kutoka shule ya sekondari ya Gonja, Wilayani Same Mkoani Kilimanjaro, ningeomba wasimame wanafunzi kutoka Gonja sekondari, karibuni sana katika Bunge letu.

Vilevile tunao Walimu nane kutoka shule ya msingi Kibamba iliyopo Dar es Salaam, naomba wale Walimu nane wasimame. Karibu sana Walimu na tunawashukuru kwa kazi yenu nzuri katika Taifa letu. Vilevile tunao wanafunzi thelathini na sita na Walimu saba kutoka kituo cha huduma ya mtoto cha Kanisa la Anglican Manyoni Mashariki wakiongozwa na Mchungaji Benjamin Mbango. Naomba hao wanafunzi, Mchungaji na hao watoto wasimame, karibuni sana na Mheshimiwa Mchungaji tunaomba uendelee kuliombea Bunge letu pamoja na kuja kututembelea.

Halafu vilevile ninao wanafunzi kumi kutoka Hijira Seminary, Shule ya Sekondari iliyopo Dodoma. Naomba wanafunzi wa Hijira, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo lingine la mwaliko. Umoja wa wanavyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu wa CCM Mkoa wa Dodoma unachukua fursa hii kuwaalika Wabunge wote wa CCM katika maafali ya kwanza ya kuwaaga wanavyuo wanachama wa CCM itakayofanyika tarehe 18 Juni, 2011 siku ya Jumamosi katika Ukumbi wa *Royal Village* kuanzia saa nne asubuhi, Mgeni rasmi atakuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Ndugu Wilson Mukama na Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi mnaalikwa sana kwa heshima kubwa kushirikiana na wanafunzi hao kwenye siku yao hiyo muhimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo jingine hapa la mwisho. Lakini sio kwa umuhimu, Waheshimiwa Wabunge leo tumetembelewa na wasanii wa filamu, *Bongo Movie* wapato thelathini, wamekuja kucheza mechi ya kirafiki na Waheshimiwa Wabunge kwa timu ya netibali na timu ya *football.*

Sasa kabla sijawataja hawa wageni wetu hapa, ningeomba sana Kamati ya Ufundi leo isilale, kwa sababu kwa kweli kesho tutakuwa na shughuli nzito sana. Sasa nasikitika tu hapa Mheshimiwa Ngonyani simwoni sasa sijui ana kaimu nani, aah! Ana kaimu Mheshimiwa Hawa Ghasia. Kwa hiyo, tunakuomba sana Mheshimiwa Hawa Ghasia leo kwa kweli usilale uchukue nafasi hiyo vizuri. *(Makofi)*

Wasanii hao wamefuatana na Viongozi wao wafuatao:-

Ndugu Hatiman Mbilinyi, ambaye ni Mwenyekiti wa hiyo *Club* yao. Tunaomba Mbilinyi asimame. Ndugu Jacob Stephen, J.B., yeye ni Makamu Mwenyekiti na Ndugu Chiki Mchoma, yeye ni Katibu wa hiyo Klabu. Sasa kwa sababu orodha yao ni ndefu na muda wetu wa shughuli unazidi kwenda, ningeomba sasa wasanii wote wasimame kwa ujumla wao ili Bunge liweze kuwatambua. *(Makofi)*

Karibuni sana, Kiti kinaomba mjitayarishe kwa sababu kesho mtapata maumivu makubwa sana. Waheshimiwa Wabunge, nitoe pia mwongozo. Tunashukuru, ninaomba mkae.

Nitoe mwongozo kwa Waheshimiwa Mawaziri, wakati wa kujibu maswali kama katika Kiti amekaa Mwenyekiti, ninaomba mji-*address* kwa Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa mujibu wa utaratibu, akikaa Mwenyekiti siyo Spika, kwa uhakika ni Mwenyekiti mwenye dhamana ya kuongoza Kikao; kuna Mwenyekiti, kuna Naibu Spika na kuna Mheshimiwa Spika.

Kwa hiyo, baada ya kutambua hilo, ninaomba sasa nimwite Katibu tuendelee na ajenda inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano ya hoja hiyo yanaendelea na kama nilivyosema, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, atafuatiwa na Mchungaji Msigwa. Mheshimiwa Nyambari.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Ninakushuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Jina langu ni Nyambari Chacha Mariba Nyangwine. Kabla ya yote, nichukue nafasi niishukuru Serikali ambayo imeandaa Bajeti ambayo nitaichangia kwa mara ya kwanza tangu nilipochaguliwa na Wananchi wa Tarime kuwa Mbunge wao kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Pongezi hizo azipokee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Waziri wa Fedha. Kabla sijaendelea kuchangia kuhusu Bajeti hii, ninaomba nitumie nafasi hii, kwanza, kuelezea *situation* halisi katika Wilaya ya Tarime. Leo ninaomba Wana-Tarime wafahamu kwa hakika kabisa kwamba, tunawatetea na nitakuwa mstari wa mbele kuwapigania kama nilivyokwishawaahidi. Sisi tumeshaunda Tume inayochunguza kwa kina mauaji yaliyotokea katika Mgodi wa Nyamongo. Hiyo Tume inafanya kazi na niliahidi kwamba, tutachukua hatua za kisheria na kali zaidi kwa yeyote aliyehusika kusababisha mauaji hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninawaombeni Wana-Tarime mfahamu hilo na mjue kabisa kwamba, nitalisimamia kwa dhati, waache wanasiasa mcharuko wanaokimbia kufanya mambo ambayo hayana maana Tarime.

Baada ya kuyasema hayo, ninaomba nirudi kwenye Bajeti ya Serikali. Mimi ninaamini kabisa kwamba, Watanzania tukiamua tunaweza, tuamue sasa. Bajeti ya Serikali imejikita katika mambo mengi sana; kwanza, imedhamiria kupunguza hali ngumu ya maisha ya Mtanzania wa kawaida; ni Bajeti inayomjali mkulima; imegusia kila Idara. Imegusia elimu, afya na hata ajira na kwamba, itapunguza matumizi ya Serikali. Hilo ninaamini kwamba ni jambo ambalo litawezekana, Watanzania wawe na imani kwa sababu kupanga ni kuchagua.

Tumepanga hiyo bajeti lazima tutaisimamia na sisi tutakuwa mstari wa mbele kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba, inatekeleza kile kilichopangwa katika Bajeti yetu. Nichukue nafasi hii nimnukuu Mheshimiwa Zitto Kabwe, ambaye ni kijana mwenzangu, tulisoma wote. Katika kuwasilisha Bajeti ya Upinzani, mwasilishaji amesema, kila mtu akitimiza wajibu wake tunaweza. Tukiacha kuwa Taifa la walalamikaji tunaweza. Tukiendeleza Umoja wa Kitaifa, mshikamano na kulinda haki za raia, tunaweza. Ninaamini tunaweza. Mimi ninaongeza kwamba, tukiamua tunaweza. *(Makofi)*

Mheshmiwa Mwenyekiti, Taifa letu limekuwa la walalamishi na kitu wanachokilalamikia hakina maana. Mimi ninawaombeni wanasiasa tusitumie nafasi hii

kuwapotosha Watanzania kuhusu ukweli unaoandaliwa na Serikali. Hakuna Serikali katika dunia hii ambayo ni ya kitapeli. Wanasiasa wanasema kwamba, Serikali inatapeli Wananchi; jamani hakuna. Wanasema kwamba, miaka 50 hatujafanya lolote katika Nchi ya Tanzania, hata kuitukana Serikali na kutoa uhuru kupita kiasi, hayo ni maendeleo. *(Makofi)*

Kutoa uhuru wa kusema mambo ambayo mengine ni ya kuudhi na kuchukiza watu, hayo yote ni maendeleo. Kwa hiyo, Watanzania tumetoka mbali na ninajua kabisa kwamba, tunakwenda mbali lakini tuamue kuanzia sasa. Ninaishauri Serikali kwa kiasi kikubwa ikusanye ushuru na mapato ya kutosha ili tuweze kusimamia matumizi ya ndani yatokane na kodi zetu. Hela za kutoka nje za misaada pamoja na mikopo ya nje na ya ndani, itumike kujenga barabara na kujenga miundombinu. Zaidi ninaishauri Wizara ya Uchukuzi ihakikishe kwamba, Bandari yetu ya Dar es Salaam inafanya kazi na inajiendesha kibiashara na siyo kwa hasara. Hili ninaamini kabisa kwamba, tutafanikisha kama tutaamua.

Tusitumie nafasi hii kuwaleta Wawekezaji ambao wanatuletea Mikataba mibovu na matokeo yake bandari inashindwa kujiendesha. Tunataka Bandari ya Dar es Salaam ijiendeshe kwa faida. Hakuna haja ya kuwapatia watu kuchukua mizigo inayotoka bandarini kuitunza katika *Warehouse* za raia pasipo kusimamiwa na Serikali. Ikifika pale, watu wanapokwenda kuchukua ile mizigo, inawawea vigumu sana kuikomboa, kama imechukua siku tano au kumi, wanalipishwa hela nyingi sana. Hizo hela zingelipishwa na Serikali, ninaamini Bandari ya Dar es Salaam ingeweza kuchangia sehemu kubwa sana ya Pato la Taifa.

Vilevile Serikali itumie fedha za kutosha kuhakikisha kwamba, ndege zetu za ATC hata kama ni mbili zinafanya safari; kwa sababu zile ndege ndizo zinazotambulisha Taifa la Tanzania. Sasa wageni wanapokuja wakikuta ni ndege binafsi zinaruka lakini ndege ya Taifa hairuki, kwa kweli hili jambo inabidi tukae tulifikirie na zaidi tuhakikishe kwamba, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam na viwanja vya ndege vyote vilivyoko Tanzania tuviendeshe kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaegemea zaidi kuhusu Tarime katika kuchangia Bajeti hii. Nianze na miundombinu katika Wilaya ya Tarime. Ninaomba kwa mara nyingine, Serikali ihakikishe kwamba, barabara ambazo zipo chini ya *TANROAD*, ambazo ni mbili ziwekewe lami. Moja ni Barabara ya Nywamwaga inayotoka Tarime, Nyamwaga, kwenda mpaka Serengeti iwekewe lami. Hii itasaidia sana kupunguza msongamano usiokuwa wa lazima wakati mvua zinaponyesha katika Wilaya ya Tarime na itaongeza kipato kwa Wana-Tarime; na vilevile Security Road inayotoka Susuni inapita Kubiterere, Gwitiryo, Borega, Nyansincha, Muriba mpaka Kegonga nayo ninaomba iwekewe lami; kwa kuwa barabara hii ipo mpakani, itasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha maisha ya Wana-Tarime. Ninakuhakikishia kwamba, Serikali ikifanya hivyo, Tarime yenye neema tele itawezekana.

Vilevile madaraja; Daraja la Mto Mori pamoja na Daraja la Kyoruba imekuwa ni kero sana kwa maendeleo ya Wana-Tarime, ambayo kupitia Bunge hili Serikali ifanye uamuzi wa dhati kabisa wa kuiendeleza Wilaya yetu ya Tarime.

Tumebahatika kupata Uwanja wa Ndege wa Magena, ambao hivi sasa unatumika kwa kiasi kikubwa kusafirisha watalii kutoka nchi jirani ya Kenya. Ninaiomba Serikali itumie fursa hii kuhakikisha Uwanja wa Magena unaendelezwa kwa sababu ndege zinatua mara mbili kwa wiki. Tukifanya hivyo tutaweza kukusanya mapato kupitia Uwanja huu na vilevile tutafanikiwa kuwasafirisha watalii kutoka Tarime mpaka Serengeti. Hali kadhalika, iende sambamba na kununua gari la zimamoto katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

Sekta ya Kilimo: Ni ukweli usiopingika kuwa, katika Nchi ya Tanzania na katika Wilaya ya Tarime, kilimo kwa kiasi kikubwa kinatoa ajira kubwa sana kwa watu binafsi na ndicho kinaongeza kipato. Bahati nzuri katika Wilaya yetu tumebahatika kupata ardhi yenye rutuba na mvua mara mbili kwa mwaka, mazao mengi yanastawi; kahawa, chai na hata bangi inastawi kinyume cha sheria. Tuhakikishe tunaisaidia Wilaya yetu ipate mafanikio ya kilimo hasa kutoa pembejeo za kilimo na kuwawezesha Wananchi wapate sehemu ya kuuza mazao yao, licha ya kutegemea kuuza katika Nchi ya Kenya, ambapo inakuwa ni kero; polisi wanawaandama siku hadi siku. Tusaidie kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia kusisitiza mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba, wamiliki wa Mgodi wa North Mara, watekeleze yote waliyoahidi Wananchi; kama hawatatekeleza ipo siku tutawafukuza. Tutakuwa wakali sana, watekeleze ahadi walizoahidi kwamba, wataimarisha huduma za jamii kama maji, barabara, elimu, afya na umeme. Ninawaomba watekeleze, wasipotekeleza tutachukua hatua kali sana na Wananchi wa Tarime ninawaombeni nitalisimamia hilo na kuhakikisha linatekelezwa.

Umeme wa *REA;* kwanza, ninaishukuru Serikali kwa kuliona hilo, imeanza kupeleka umeme vijijini. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ahakikishe Vijiji vya Nyamwigura, Rozana, Nyamwaga, Keisangura, Tagare, Kumwika, Kobori, Itiryo, Mangucha, Kegonga, Masanga, Susuni, Kubiterere, Borega, Kimusi na vijiji vingine vyote vipatiwe umeme; hiyo itawezekana. *(Makofi)*

Tutumie vilevile umeme wa Mgodi wa Nyamongo kuhakikisha unawanufaisha Wananchi; maana Wananchi wasiambulie kuona nyaya tu zinapita. Ninaiomba Wizara tushirikiane kwa Wamiliki wa Mgodi, kwa sababu tukifanya hivyo, vijiji katika Kata za Komaswa, Manga, Kibasuka hadi Nyamongo, vitahakikisha vinapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta nyingine ambayo ninapenda kuichangia ni elimu na katika elimu mengi yamezungumzwa. Ninapenda ni-*declare interest* kwamba, mimi ni mchapishaji wa vitabu. Ninawaombeni wachapishaji wa ndani wawezeshwe ili waweze kuchapisha vitabu ambavyo vinaendana na hali halisi ya mazingira ya Mtanzania, badala ya Wizara kuwekea mkazo vitabu vya kutoka nje ya nchi, ambavyo havioneshi uzalendo, ambavyo vinasisitiza tamaduni za nje. Ninaomba tutumie nafasi hii

kuwasaidia wachapishaji wazalendo ili waweze kuchapisha vitabu ambavyo vinaendana na mahitaji ya Tanzania.

Maji ni muhimu sana, nimeshaiomba Serikali ihakikishe inapeleka huduma za maji katika Jimbo la Tarime na sehemu nyingine za Tanzania.

Ajira imeongelewa, lakini mimi ninaamini kwamba, mmomonyoko wa maadili toka ngazi ya familia mpaka Taifa, umechangia sana vijana wengi kubaki vijiweni na kulalamika. Tutumie nafasi hii kuwaomba vijana wenzangu kwamba, tukiamua tutaweza, tufuate ushauri wa Serikali tutajitahidi kuwawezesha lakini na wao wafanye kazi, wasikae kulalamika tu kila wakati. Hilo litawezekana kama tutaamua.

Vilevile ninaiomba Idara ya Mapato *(TRA)*, iangalie ushuru wa waendesha pikipiki. Hivi sasa hapa Tanzania vijana wamejiajiri kuendesha pikipiki. Utakuta wanatozwa kodi ya mapato kuanzia shilingi 90,000 mpaka laki moja. Ninaomba Idara ya Fedha au Wizara ya Fedha, ihakikishe waendesha pikipiki hasa wa Wilaya ya Tarime, wasitozwe zaidi ya shilingi 30,000, hii itawasaidia sana kujiajiri na kuajiri watu wengine.

Mwisho, nichangie kuhusu njaa katika Wilaya ya Tarime. Nimeshamwomba Waziri wa Kilimo, aangalie katika Ukanda wa Tarime Magharibi hasa katika Kata za Komaswa, Manga, Kibasuka, Nyangoto, Kemambo, Nyarukoba na Gorong’a, kuna njaa. Ninaiomba Serikali itoe msaada wa haraka ili Wananchi wa Tarime wasiendelee kuumia. Ninafikiri Wananchi wa Tarime wakila wakashiba watafanya mambo makubwa sana katika nchi hii.

Ninaamini kwa dhati kwamba, kwa Tanzania hii tukiamua tutaweza. Sasa tumeamua kwamba, tunafanya kazi kwa bidii na hasa katika Jimbo langu la Tarime, vijana wamejiari kwa kiasi kikubwa na akina mama wamejiweka katika vikundi mbalimbali vya uzalishaji. Tutaomba Benki ya Wanawake iwasaidie waweze kupata mikopo ya kuwasaidia kujiendeleza ili watoe mchango mkubwa sana wa maendeleo katika Wilaya yetu. Nitawaomba wale ambao watakuwa na mawazo mazuri ya kutusaidia kuendelea, ninawakaribisha Tarime. Ninamwomba Mchungaji wangu yule pale wa CHADEMA, karibu Tarime utuombee, tudumishe amani. Atakayekuja kuleta fujo, ninarudia kusema kwamba, wazee wameamua hatuwezi kukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ninaunga mkono Bajeti hii ipite kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana. Katika kipengele kimoja tu, Serikali itasaidia mazao yote, lakini hata kama bangi inastawi huko, hiyo haitasaidiwa na Serikali. Kwa hiyo, mazao mengine yote yatasaidiwa na Serikali yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Ninaomba nimwite Mchungaji Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini na Mheshimiwa Nimrod Mkono, atafuatia.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami pia ninaungana na wenzangu kusema kwamba, kabla sijaendelea kuchangia, siiungi mkono Bajeti hii mpaka baadhi ya mambo fulani labda Waziri ayatolee ufafanuzi vizuri.

Kabla ya kuingia kwenye mada yangu, ninachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kwa mapenzi makubwa, Wananchi wote wa Nyanda za Juu Kusini, hususan Wananchi wa Iringa Mjini, kwa kujitokeza kwa wingi sana pale ambapo tulipita tukifanya maandamano ya kudai haki na ukombozi wa Mtanzania katika nchi hii. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nchi yetu ina matatizo ya Utawala Bora na Sheria; na ningependa nizungumzie kwa kifupi kidogo. Wachina wana methali moja wanasema, nitainukuu: *"It is not economical to go to bed early and save all the candles if the result is twins."* Siyo jambo la kiuchumi kwenda kulala mapema ukatunza mishumaa, matokeo yake unazaa mapacha. Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imekuwa ikijaribu kuwakandamiza na kuwapiga watu ambao wanadai haki zao, kwa kuamini kwamba, inatunza amani, kumbe matokeo yake tutakuja tutabanana ... *(Kicheko)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Kanuni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(a). Mheshimiwa anayechangia hivi sasa anasema, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inapiga watu, inaua watu; sasa mimi ninafikiri, kwanza, kwa mujibu wa Kanuni hii, Mbunge yeyote hatakiwi kuzungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala. *(Makofi)*

Pili, ningependa Kiti chako, mimi kama sehemu ya Serikali, Mheshimiwa Mbunge anithibitishie tu ni mahali gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo hayo. Atoe uthibitisho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, umeunganisha Kanuni hiyo kwa Kifungu (a) na (b). Suala unalolisema haliko kwenye mjadala ni kweli suala hilo la kupiga watu ambalo unalizungumzia katika hoja yako ya msingi ya ajenda ya fedha, sasa sijui unaunganishaje hiyo na ajenda hii ya fedha? Vilevile umeombwa uthibitishe ni kwa kiasi gani Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kazi yake ni kuua watu na kupiga watu.

Sasa Mchungaji Msigwa, ninaomba ufanye mawili; ama ukubali unao uhakika wa kuthibitisha hilo; na ukinikubalia kuwa, unao uhakika wa kuthibitisha hilo, nichukue maamuzi ya Kikanuni ya kukufanya uthibitishe hilo au vinginevyo uondoe kauli yako hiyo.

Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaamini na muda huu utanifidia ili niweze kuzungumza niliyokusudia kuzungumza.

**MWENYEKITI:** Ninaomba uende kwenye majibu yangu ili tuweze kuendelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Serikali imeuwa watu Arusha, imeuwa watu Nyamongo na sasa ninapozungumza, kuna wanafunzi waliopigwa *UDOM* wamelazwa hospitali. Kwa hiyo, siongei mambo ambayo hayana kina, ni Serikali imewauwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili.

**MWENYEKITI:** Ninaomba ukae Mchungaji Msigwa. Kwa maana hiyo, unataka kuthibitisha Serikali imeuwa watu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa utaratibu huo, Ofisi yangu itachukua utaratibu unaotakiwa, ulete uthibitisho maalum na kama uthibitisho huo hautajitosheleza, basi Kanuni nazo zitachukua mkondo wake katika kushughulikia suala hilo unalolizungumza. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya, ninaomba uendelee; na ajenda hiyo kwa kuwa nimeishaifanyia maamuzi, nisingependa ijitokeze kwenye mjadala wako tena.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuhusu mambo ambayo hayajadiliwi katika utaratibu, tumeona watu wakizungumza masuala ya maandamano hapa, hawachukuliwi hatua!

**MWENYEKITI:** Mchungaji Msigwa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ngoja nirudi kwenye hoja, samahani.

**MWENYEKITI:** Ninaomba ukae chini. Nikishafanya maamuzi, nimemaliza kufanya maamuzi, unaporudia kuyarudia maamuzi ya Kiti, Mchungaji Msigwa, sasa unahamisha mjadala kati yako wewe na Kiti. Kiti kinao uwezo wa Kikanuni wa kuamua jambo lingine. Nimeshasema mjadala huu nimeufunga baada ya kufanya maamuzi na ni mwiko kwa mujibu wa Kanuni, kurudia kitu ambacho kimeshafanyiwa maamuzi.

Sasa ninaomba uendelee, lakini kama huna hoja ya kuendelea hoja yako bado ni hiyo, ninadhani nimwite mtu mwingine aendelee.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ngoja niende kwenye hoja moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza kuhusu maendeleo ya Taifa letu na kwamba nchi yetu imekuwa huru kwa kipindi cha miaka 50, hakuna anayesema kwamba, nchi hii haijafanya kitu chochote; ni watu wanaojaribu kufitini uhalisia. Tunachozungumza ni sawa na ukiwa na mtoto wa miaka kumi anayekuwa na tabia za mtoto wa miaka miwili; Bajeti ya Mheshimiwa Mkulo, imetuwekea vipaumbele. Taifa letu tuna umri wa miaka 50, nusu karne, wengine wamezungumza hapa, kama Kambi ya Upinzani tunasema kwamba, tabia za Serikali yetu hazilingani na umri wa mtu ambaye amekomaa, ndipo ugomvi unapoanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto mchanga ana tabia za kulialia, anataka abadilishwe nepi, anataka apewe maziwa, lakini mtu mzima anawajibika kulingana na umri wake. Hoja tunayoizungumza hapa ni umri tulionao na maendeleo ambayo hayalingani na umri tulionao, saa zote tunazungumza vitu ambavyo ni *basic.* Ninakumbuka tunazungumza kuhusu kubana matumizi na Wabunge wenzangu wengi sana wamemsifu hapa Waziri Mkuu, kwa hatua yake ya kukataa *VX* na kutumia *GX,* lakini mimi *with due respect, ni*naomba nikuseme kidogo Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninadhani nitakuwa rafiki yako mzuri kuliko wengine wote wanaokusifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji, Kanuni zetu zinasema unapoongea, unaongea na Kiti. Kwa mujibu wa Kanuni unaongea na Kiti, hum-*address* mtu yeyote ndani ya Bunge. Bunge hili ni Mwenyekiti, Spika, Naibu Spika na Mzungumzaji. Sasa kama kila Mbunge hapa akisimama anam-*address* Mbunge mwenzake ndani ya Bunge, eeh, itakuwa ni kazi kubwa sana.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zimewekwa ili tufuate utaratibu, wewe niambie mimi; mambo yako yote niambie mimi usimtaje Mbunge mwingine humu ndani. Huu ndiyo utaratibu wa maongezi yetu yote ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mchungaji, haya endelea. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuja Iringa nikiwa bado siyo Mbunge na nilisema nitakapokuwa nimekuja Bungeni ni lazima hili nitali-*address; k*wa kubana matumizi Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulikuja na ndege mbili, ulikuwa na msafara wa magari karibu 50, njia zilizibwa magari kutoka Dar es Salaam na Mbeya, yalikuwa hayaingii wala kutoka Iringa kwa saa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo dalili nzuri ya kubana matumizi. Uchumi uli-*freeze* karibu saa tano kuingia na kutoka Iringa. Kwa hiyo, tunapozungumza kubana matumizi, hebu tubane matumizi kwa vitendo ili hata watoto hawa ambao wanadai haki zao, waone watendaji wa Serikali tunafanya kazi zetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja kwenye vipaumbele, Mheshimiwa Mkulo, umezungumza Mipango mizuri ya Viwanja vya Ndege, kwa maana ya miundombinu.

Pale Iringa, tuna kiwanja kizuri sana cha ndege ambacho kama kingeingizwa kwenye utaratibu mzuri, kingeweza kukuza uchumi, kwa sababu tuna mbuga nzuri ya wanyama ambapo kama ingejengwa barabara ya lami kwenda Mbuga za Wanyama, *National Park*, uchumi wetu ungeweza kuongezeka. Vilevile tuna barabara inayotoka Chimala kwenda Kitulo, ambako kuna Mbuga ya Kitulo, hii ni Mbuga nzuri lakini nayo haijawekwa kwenye Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wakati analizindua Bunge hili, alizungumza jinsi gani ambavyo Sekta ya Utalii inaleta pato kubwa kwa Taifa letu. Kama kweli tunaithamini Sekta ya Utalii, maeneo haya ambayo yanaonesha kwamba, yanaweza yakaleta watalii wengi, yangetiliwa maanani. Vile vile Mbunge mwenzangu wa Mufindi, alizungumza kuhusu barabara; tuna mbao nzuri sana kutoka kule *SAO Hill*, ambazo zinasambazwa karibu Tanzania nzima, lakini barabara ile haijawekewa kipaumbele kwa kiwango cha lami. Ningesihi, ili tuwe na uwiano wa mgawanyo wa uchumi tulionao, maeneo hayo; Nduli Kiwanja cha Ndege; barabara nzuri ya kwenda kwenye Mbuga za Wanyama ambako ni Jimbo la Mheshimiwa Lukuvi; barabara nzuri zitengenezwe katika eneo la Bwana Lutengano, ambaye ni Mbunge wa CCM*;* hata kwa Mheshimiwa Anna Makinda, ambaye ni Mbunge pekee wa kwanza mwanamke, Kiwanja cha Ndege nacho kimeachwa tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba hayo mawazo yote yatiliwe maanani kusudi maeneo hayo yaweze kuleta maendeleo katika maeneo yanayohusika. Katika kitabu chako, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ukurasa wa kwanza; ningeomba unifafanulie vizuri; hivi *what is the legitimacy of SUMATRA getting cut from fuel importation?* Kuna umuhimu gani *SUMATRA* wanakatwa? Ningepata ufafanuzi hapo.

Ukurasa wa 10, Serikali imekuwa ikiwashauri Wananchi kutumia vyanzo mbadala badala ya umeme na hili limetolewa ambapo Wananchi wamejitahidi kuitikia mwito; lakini tatizo kubwa ni gesi ya LP tunayoitumia, gesi hii imekuwa na bei kubwa kwa sababu inatokana na mafuta. Kwa kuwa nchi yetu ina akiba ya gesi asilia, yaani *natural gas,* Serikali ina mpango gani au *strategies* gani za kuwa-*encourage* watu wa sekta binafsi kuanza kuingiza nchini vifaa vitakavyotumia nishati hiyo? Ningeomba nipate ufafanuzi katika maeneo hayo. Aidha, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha nishati hii ya gesi asilia inasambazwa nchi nzima ili kuvutia Sekta Binafsi kuanza kuingiza vifaa vitakavyohitaji gesi hiyo asilia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa kumi huo huo; Hifadhi ya Chakula, *NFLA*, kutumika kupunguza bei ya chakula nchini kama ulivyoeleza; tatizo kubwa ni usambazaji wa chakula kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Kwa kuwa tunafahamu kuwa wanaosambaza chakula hiki ni Sekta Binafsi, Serikali inaposema itasambaza chakula hiki kwa bei nafuu; je, inaweza kutuambia ni *strategies* za namna gani zitakazotumika kuhakikisha tunapata chakula hicho katika maeneo mengi ambayo Wananchi wa kawaida hawawezi kumudu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 11 wa Bajeti unasema; kuongeza ajira, mpango wa kuleta mapinduzi ya kilimo. Hili ningemwomba Mheshimiwa Waziri atupe *Action Plan*, la sivyo ni kupeana ahadi ambazo hazitekelezeki; *what is your Action Plan?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 13, Kifungu (c), Serikali imeweka utaratibu mzuri, *data* zipo kusaidia watu wangapi? Utaratibu huu umefanikisha wajasiriamali wangapi? *What was the estimate numerical goals?* Ulikuwa na malengo yepi *before? So far, what percentage has been achieved?* Ukitupa majibu hayo, nitafurahi kuiunga mkono Bajeti yako. Hatuwezi kusema tuna Mpango mzuri tu, upi; una malengo yepi? Majibu haya tumeyapata kwa Mawaziri wengi, wanasema tuna *Vision* hii, hata ukienda kwenye Manispaa nyingi wanasema, tuna *Vision* hivi na hivi, lakini ukiwaambia mpaka sasa tuko wapi kwenye *graph* hiyo ninaomba nipate majibu, hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *kipengele (d)*, unasema kuharakisha maboresho! *Time line*, unaharakishaje? *For how long* tutaharakisha hayo maboresho? Serikali imekuwa ikituambia *the same for few years already! It is time we start demanding actionable points. We need tangible goals with time lines now. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 16, kuongezeka kwa kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani, hilo ninakupongeza. Kugharimia mafuta ya kuendesha mitambo ya kufufua umeme *IPTL*, lakini *this is the wastage of money!* Kumekuwa na mipango ya kubadilisha mitambo hii iwe inatumia *natural gas* kwa miaka zaidi ya minne sasa; *when will this mitambo be converted to start using gas?* Utaanza lini kui-*convert* mitambo hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 25 – 26, inaonesha kwamba, malengo yote ya ukusanyaji kodi kwa vipindi viwili mfululizo, hayakufikiwa! Unaweza ukatueleza ni kwa nini hayakufikiwa na kwa nini hayatafikiwa tena ikiwezekana mwaka huu? Udhibiti wa fedha za umma, mashirika kushindwa kujiendesha kibiashara; mashirika haya yamekuwa yaki-*suffer* kutokana na kuingiliwa kiutawala na kiutendaji, matokeo ni kwa mashirika haya kuendeshwa kisiasa zaidi kuliko kibiashara.

Je, Serikali inaweza kutuambia nini kuhusu kuruhusu mashirika haya kujiendesha yenyewe bila ya kuingiliwa na Viongozi mbalimbali na Wizara za Serikali? Je, Serikali haioni muda umefika kuangalia upya Sheria inayosimamia Uundwaji wa Bodi za Mashirika haya na kutafuta namna salama ya kutoa uhuru zaidi wa mashirika kujiundia bodi zao wenyewe kutegemea mahitaji yao ya kiutawala na kiufundi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nitafurahi kama utanipa majibu mazuri katika hayo ili niweze kuiunga mkono Bajeti yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa mafanikio katika kuongeza idadi ya Vyama vya *SACCOS* na Vikoba na idadi ya Wanachama. Kwa kuwa vyama hivi vinatunza jasho la watu wengi na kuwa kama msemo unaosema, kwenye msafara wa mamba na kenge nao wamo na hujihudhurisha, je, Serikali ina mpango wowote wa kuweka sheria itakayovilazimisha vyama hivi kufanyiwa *auditing* japo mara moja kwa mwaka ili tuweze kudhibiti wale ambao ni wezi katika vikundi hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa au kama Wabunge, tumefurahia sana huu usemi unaosema, *yes we can.* Ninaweza nikasema ni usemi ambao tumeu-*copy* na kuu-*paste* kutoka Marekani, lakini wenzetu hawa wameji-*commit*, wana uzalendo, wanaipenda nchi yao; ukienda kwa Wamarekani, karibu kila mtu ana Bendera ya Taifa nje inapepea. Kwenye mafriji yao kuna nyimbo za Taifa, wako *commited* na kazi kuliko kusema *yes we can,* lakini kama hatujaji-*commit,* haya mambo hayawezekani. Tunahitaji *commitment* za Mawaziri, za Viongozi wa Serikali na Wabunge kwa pamoja, tuache *blah blah,* tufanye kazi ambayo Wananchi wametutuma. Tuji-*commit* kwa pamoja, tushikamane, ndipo tunaweza tukasema kwa pamoja *yes we can.* Vinginevyo, tutachukua semi hizi, *yes we can,* tunakuwa kama kasuku kama hatutaji-*commit. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wengi majibu wanayoyatoa hapa ni sawa na tukiwa kwenye Kamati, hayana *details,* wakija Bungeni kwa sababu ya muda, yanakuwa yana *details.* Ninaomba tuji-*commit* kwa pamoja, *yes we can,* tukishikamana kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWONGOZO WA MWENYEKITI**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7), nikirejea Kanuni ya 64, Fasili ya 1(f) na (g).

**MWENYEKITI:** Ninaomba uisome.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano Katika Bunge, Mbunge:-

(f) hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote.

(g) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaheshimu sana na kumheshimu Mheshimiwa Mbunge mwenzangu na Mchungaji wangu Msigwa, lakini alipokuwa akichangia hapa aliifananisha Serikali ya Tanzania na mtoto wa umri wa miaka kumi, lakini anayetenda sawasawa na mtoto wa miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania imeongozwa na Mheshimiwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mtu anayeheshimika Duniani kote. Serikali ya Tanzania imeongozwa na Mzee Ali Hassan Mwinyi, Mzee Mkapa na sasa Mzee Kikwete. Serikali ya Tanzania, sisi sote tulioko hapa ni sehemu na Serikali hii, haijawahi kufananishwa na mtoto wa miaka miwili. Tumetoa Magwiji na Mabingwa wa Uongozi katika Umoja wa Mataifa na katika Bara zima la Afrika. Tunaiongoza nchi hii kwa viwango ambavyo Dunia nzima inaridhika. Mheshimiwa ni sehemu ya mafanikio hayo kama Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema lugha hii inaudhi na siyo tu inamdhalilisha Mtanzania mmoja mmoja kama Fasili ya 1(g) inavyosema, hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine; lakini ninamwomba sana Baba Mchungaji, ukiishusha hadhi ya Serikali yako na kuifananisha na umri wa miaka miwili, siyo jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ukipata muda, ulitolee maelekezo ili tuendelee kurejea kwenye Lugha ya Kibunge kuliko kuidhalilisha Serikali yetu, kana kwamba sisi siyo sehemu yake. Hatufurahishwi kama watu binafsi na siyo hadhi ya Bunge letu kuja hapa kutumia jukwaa na fedha za walipa kodi wa Tanzania, kuitukana nchi yetu na kuwatukana Watanzania mmoja mmoja. Serikali hii haijajileta yenyewe madarakani, imeletwa na kura za Watanzania kwa kuridhika jinsi inavyofanya kazi kwa viwango vya kisasa na vya kupigiwa mfano Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Sendeka. Katika utoaji wa hoja yake, ameliomba Bunge sasa lifanye utaratibu wa kutoa maelekezo kwa kina kwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Ole-Sendeka, kwa sababu sasa hivi Bunge hili tumeanza sasa kuligeuza kuwa ni Bunge ambalo halina ustaarabu. Waheshimiwa Wabunge, tumeanza sasa kutumia maneno ambayo mimi ninaweza kukubali mtu anaweza kuwa na hoja inayomkera, lakini unapoijumuisha Serikali hii toka ilipopata uhuru, kwa sababu hauko *specific* katika eneo gani; sasa unapoihusisha Serikali hii toka ilipopigania uhuru, ambao uhuru ule tunao wote mpaka sasa na kujumuisha Serikali hiyo yote kwa lugha ya kuudhi, iko kama mtoto, akiwemo na Marehemu Baba wa Taifa anayeheshimiwa katika Ulimwengu mzima; ninadhani nikubaliane na Mheshimiwa Ole-Sendeka, tumwombe Mheshimiwa Spika na kwa kuwa sasa hivi tunafanya marejesho mapya ya kanuni zetu, ifike mahali kuwe na kifungu ambacho kitaweza kutusaidia kuondoa hii tabia ya kuwa na maneno ya kuudhi, yasiyokuwa na utaratibu ili Bunge letu libaki na heshima na liendelee kuwa sifa, lionekane kwamba hata sisi Wabunge tunajiheshimu wenyewe na hata kama mtu anatoa hoja apingane na hoja kwa hoja na siyo kwa lugha ambazo zimekuwa wakati mwingine zinatudhalilisha katika Bunge.

Kwa hiyo, nipokee huo mwongozo na ninaomba nipokee hiyo taarifa yako, ninadhani kuna umuhimu wa kufanya hivyo ili kulifanya Bunge letu liendelee kuwa la heshima. *(Makofi)*

## KUHUSU UTARATIBU

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge). Kanuni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ile ile ya 64(1), ninataka kuzungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Nilitaka Mheshimiwa rafiki yangu, Mchungaji, Mbunge mwenzangu wa Iringa, kwa sababu na Wabunge wa Iringa wanamsikia, nisimsimamishe tena mara ya pili, amalizie hotuba yake; katika hotuba yake anasema Mheshimiwa Waziri Mkuu na bahati njema ulimsimamisha mapema, maana alikuwa anamtaja na kumuonesha kwamba, Mheshimiwa Waziri alikwenda Iringa; yeye mwenyewe Waziri alitumia ndege mbili za Serikali, lakini msafara wake huyu Mheshimiwa Waziri Mkuu alipanda magari 50; na Mheshimiwa Waziri Mkuu huyu alisimamisha misafara kutoka Dar es Salaam, Morogoro na Mbeya kwa saa tano; bahati nzuri na Hansard ninayo, tayari vijana wangu wameshaniletea.

Sasa ningependa Mchungaji, kwa sababu katumia ushahidi wa Iringa na mahali popote ulipo; tungependa tujue huyo ni Waziri Mkuu gani unayemsema; ni huyu wa Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye anaweza kusafiri kwa ndege mbili za Serikali mara moja na magari 50; haya sijui anayaweka kwenye ndege anakuwa nayo wapi; anatoka nayo wapi? Jambo hilo limetokea lini Iringa kama ulivyosema? Wakati gani ambapo magari yalisimamishwa kutoka Dar es Salaam, Mbeya na Morogoro kwa saa tano nchi ilisimama? Hilo nalo ni jambo ambalo ningependa Mheshimiwa Mchungaji, mimi zamani nilifikiri Mchungaji maana yake ni Mchungaji wa Kondoo, sasa sijui huyu ni Mchungaji gani; lakini ningependa Mchungaji Msigwa athibitishe hapa.

Mimi nina-*declare interest;* ninakaa Iringa lakini sisemi hapa kwa sababu ninatoka Iringa ila nilitaka tu kuliomba Bunge lako Tukufu likubali Mheshimiwa huyu atoe uthibitisho. Kauli kama hizi zikiendelea, tutaendelea kuliacha Bunge hili lizungumzie masuala ya Alinacha badala ya kuzungumzia masuala ya kero za Wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninashukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, baada ya kuyasema hayo, nirudi tena kwa Mheshimiwa Mchungaji; unapotakiwa kuthibitisha jambo ambalo halina ukweli, ninakuomba yale yale mawili; una uhakika na ulichokisema kama huna uhakika ufute kauli yako, kama huna uhakika basi mimi nitaendelea na kanuni yangu ili kuweza kulihitimisha jambo hili.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, ninaomba unilinde. Sijafurahishwa sana na Mheshimiwa Waziri kuniita Mchungaji gani; hiyo ni kashifa, ni dharau, kwa sababu mimi sichungi kanisa lake, ninaomba aniheshimu, hii kazi sikuipata kwa ku-*apply*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order*.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ninaomba hilo alifute kabisa, kwa sababu akiniita Mchungaji gani, kuna watu ninaowachunga wananiheshimu, inawezekana simchungi yeye.

Pili, nilivyosema …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji, wewe hilo nalo kama limekuudhi utalileta kwa utaratibu wake. Ninaomba mnisikilize Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Mchungaji amepewa mwongozo na Kiti, sasa aanze kujibu ya Kiti, halafu hoja hiyo nyingine nayo itafuata kwa utaratibu wake. (*Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. ZAINABU M. VULLU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Hakuna taarifa mpaka nimalize taarifa ambayo iko mbele yangu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuhusu magari anayoyazungumza na ndege, hii ni akili ya kawaida; mtu hawezi kupanda ndege mbili mbili, mimi ninazungumza ndege zilikuja mbili Iringa na magari yalikuwa 50 na mimi nilikuwepo kwenye msafara, tulikuwa tunazindua Barabara ya kutoka Iyovi kwenda mpaka Iringa Mjini. Sasa ukiniambia mtu anapanda ndege mbili mbili, hata kwa kawaida haiwezakani; utapandaje ndege mbili, ila ndege zilikuja mbili Iringa na magari 50 na gari langu likiwa kwenye msafara kama Mwenyekiti wa CHADEMA, nilikwenda kufungua ile barabara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji, wala hatuna mgogoro, ninakubaliana na wewe, ndege zilikuja, magari yalikuja, yaani wala sina mgogoro na wewe; mimi ninaomba uniambie tu kwamba, ninathibitisha kauli yangu hiyo ni ya kweli.

Subiri, wala hakuna mgogoro, Mheshimiwa Msigwa wewe unasema vitu vyako ambavyo unavifahamu vizuri, umevi- *witness* vizuri na Bunge hili lina taratibu, wala hatugombani. Wewe ulishashuhudia hayo uliyoyasema na bahati nzuri hayo yote uliyoyasema yamerekodiwa na *Hansard*, kwa maana hiyo wala hatuna mgogoro.

Mchungaji, unasimama kutetea hoja yako na mimi ninakubaliana na wewe na ninakulinda katika hoja yako hiyo na kama ni hoja ya ukweli, yenye msingi, ninailinda kwa nguvu yangu yote katika Kiti; ndiyo maana nimekwambia jambo ni dogo tu; uniambie Mheshimiwa Mwenyekiti ninathibitisha hayo niliyoyasema ni ya kweli. Utapata tu muda mzuri wa kuyasema hayo vizuri kabisa na kuyathibitisha wala haina tatizo. Kama siyo ya kweli, unasema Mheshimiwa Mwenyekiti sina uhakika na hayo niliyoyasema, kwa hiyo, ninaomba kufuta kauli yangu hiyo; ndiyo Kanuni Mheshimiwa Msigwa, wala hatuna matatizo, tunapeana nafasi kila mtu atathibitisha mambo anayoyasema Bungeni, hayana matatizo wala halina neno. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ninathibitisha niliyoyasema ni ya kweli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru, tunaendelea. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zitafuata utaratibu wake.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Sijampa mtu nafasi, Mheshimiwa Zaynab Vullu.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuhusu taarifa, kifungu namba 68(8).

Mheshimiwa Mchungaji, alipokuwa akichangia alisema Mbunge wa Kwanza Mwanamke ni Mheshimiwa Anne Makinda. Kwa kuwa hili ni Bunge Tukufu na sisi sote tunapoingia hapa tunaapa kwamba, tutasema ukweli na kwa kuwa *Hansard* zinachukua taarifa, ninaomba nimwarifu kwamba, Mbunge wa Kwanza si Mama Anne Makinda; wako akina Bibi Titi na wengineo. Inawezekana Mchungaji wakati anaingia kwenye siasa, hajasoma vizuri, aangalie; na kwa kuwa yeye ni Mchungaji ninamwomba awe makini anapotoa taarifa ili kondoo wake wasije wakamponyoka.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninafikiri hiyo ni taarifa tu, ambayo Mheshimiwa Mbunge unataka kumsahihisha Mchungaji. Inawezekana Mchungaji yeye katika kuangalia suala hili, anafahamu Mbunge wa kwanza ni Mheshimiwa Mama Anne Makinda; ninadhani kwa kuchukulia kwamba, Mkoa wa Iringa, Mbunge wa Kwanza wa Jimbo ni Mheshimiwa Mama Anne Makinda. *(Makofi)*

Mchungaji upate tu taarifa kwamba, Mama Anne Makinda siyo Mbunge wa Kwanza Mwanamke katika Nchi hii ya Tanzania. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, ninaposema kwa Mkoa wa Iringa, ninataka kujua Mchungaji Msigwa inawezekana alifikiri hivyo, lakini kwenye *statement* yake alisema Mbunge wa Kwanza bila kusema ni wa mahali gani; kwa hiyo, taarifa hii na *Hansard* ninaomba irekodi kwamba, Mbunge wa Kwanza Mwanamke katika nchi hii siyo Mama Anne Makinda, naomba *Hansard* muiweke vizuri. Kwa mkoa wa Iringa, Mbunge wa Kwanza ni Mama Anne Makinda.

Baada ya kusema hayo, ninafunga taarifa zote, ninaendelea na mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Mkono.

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**TAARIFA**

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba mimi.

**MWENYEKITI:** Ninaomba tuendelee. Waheshimiwa Wabunge, tusitumie huu muda wetu vibaya, hebu tuendelee kuwawakilisha Wananchi. Mheshimiwa Mkono. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkono, husikiki vizuri hapo.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja hii muhimu, ambayo ni Bajeti. Bajeti hii inahusiana na mapato na matumizi ambayo Serikali inakusudia kwa kipindi cha miezi kumi na mbili. Kabla sijaanza kuchangia, nichukue nafasi hii pekee, nami niungane na wenzangu walionitangulia, kutoa rambirambi zangu za dhati kwa kifo cha Mama yetu Mpendwa, aliyekuwa Mama wa Spika wetu wa Bunge, Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, ningependa kusema machache kuhusu Wananchi walionichagua huko Musoma Vijijini; wamenichagua kwa miaka mitatu mfululuzo ilikuwa ni vipindi vitatu mfululizo, ninadhani nitakuwa nimekosa heshima bila kuwakumbuka na kuwashukuru sana kwa kunipitisha kwa kipindi hiki tena. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue hii nafasi kuwapongeza Wabunge wapya na wa zamani, kwa kuweza kuingia kwenye Ukumbi huu kama Wabunge, baada ya kupitia mchakato mkubwa uliofanywa wakati wa Uchaguzi Mkuu; hongereni sana ndugu zangu Waheshimiwa mliopo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Wapiga kura wote wa Musoma Vijijini, Bajeti hii ninaiunga mkono mia kwa mia. Ninapenda kuwaambia wanaonisikiliza, kwa upande wa Musoma Vijijini, hatukupata faida na bajeti hii kwa kuwa kero zetu kubwa ambazo tulikuwa tumeiomba Serikali itusaidie, zimebaki pale pale hazikuongezwa kwenye Bajeti hii. Ninasema kero kubwa kwetu ni barabara; barabara moja ambayo imezungumzwa kwa miaka mingi ni ya kutoka Mkutano, inapitia Butiama, inakwenda Ikizu, Fort Ikoma, haipo kwenye Bajeti hii. Nitalizungumza jambo hili wakati Waziri mhusika atakapowasilisha hoja yake, lakini ninasema Bajeti haina mwelekeo wa kutusaidia kwa kero hii.

Sehemu ya pili ni Uwanja wa Ndege, ambao tulidhani ungeingizwa kwenye Bajeti hii. Pale Musoma, upo Uwanja wa Ndege mdogo sana, tulidhani kwamba kwa kuwa tumeahidiwa miaka ya iliyopita, Uwanja ungejengwa karibu na Nyasurula; pia haupo katika Bajeti hii.

Sehemu ya tatu ni jambo sugu sana la Buhemba; *Buhemba Mine* imekuwa inanisumbua mimi kama Mbunge wao kwa miaka 11 sasa. Serikali kila wakati inaniahidi

itafanya kitu kuhusu Buhemba, sasa ule mgodi umebaki pale unaachama tu Watu wa Kenya ndiyo wanafaidika, lakini sisi Wananchi wa Tanzania hatupati lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameniahidi mara nyingi atakuja pale hajafika. Kwa hiyo, ninasubiri, ninatoa tu tangulizi kwamba; ifikapo Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini, ninakusudia kutoa shilingi kutoka kwake mpaka mtakapokwenda kuwaambia Watu wa Buhemba kulikoni, Buhemba ni ya nani na kama kweli ni ya Wanajeshi, basi hilo siyo Jeshi la Ulinzi ni Jeshi la Wizi. Sitaki kufikia huko, lakini ninatoa kauli kuwa, siamini kama Bajeti hii inawafanyia Watu wangu Musoma Vijijini vyema, kuwa na Pori pale Buhemba kwa miaka yote tangu MEREMETA kukimbia pale mpaka sasa hakuna kinachoendelea.

Tatizo langu la tatu ni malambo makubwa niliyoahidiwa miaka kumi sasa. Niliambiwa malambo kumi yatajengwa pale ama yatakarabatiwa, malambo hayo mawili yapo Kiagata, hali yake ni mbaya kabisa na sioni mwelekeo kwa Bajeti hii kwamba lolote litafanyika pale Kiagata wala Kyalano.

Huko nyuma, Waziri Mkuu aliyotangulia, aliwahi kuniletea Mawaziri watatu kuja kuona hali halisi ya Buhemba, Kyalano na hali halisi ya malambo matatu, nikaahidiwa kwamba, kitafanyika kitu. Ninasikitika kuona hata ndugu zangu Wapinzani wakija Musoma hawaendi Buhemba, maana wanaogopa, sijui wanapewa nini pale, mimi sijui; ningependa kujua kulikoni huko Serikali na upande wa Upinzani pia. *(Makofi)*

Haya malambo mengine niliyoyasema ya Kyarano na kule pia muhoji, lipo upande wa Nyanza, yako katika hali mbaya na sioni fungu lolote kwenye Bajeti la kunisaidia kule. Pamoja na kusema hivyo, kwa kigugumizi nitaiunga mkono hoja hii, iwapo mtawaambia Watanzania wenzangu hasa wanaoishi Musoma Vijijini, mtatusaidia kuondoa kero hizo.

Sasa ninakuja kwenye lingine muhimu sana, ambalo ni kuhusu makadirio yenyewe ya mapato na matumizi. Kwa mwelekeo wangu, ninaona Serikali imekwama kuongeza Pato la Taifa. Ninarudia tena; Pato la Taifa limebaki dhaifu kwa kipindi kirefu sana, sioni Bajeti hii kwa kweli ina lengo la kuongeza mapato. Katika mapato ya ndani ya Serikali, kubwa zaidi ambalo linaingiza mapato mengi ni Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*, *rate* yake mpaka sasa ni asilimia 18, ilipunguzwa kutoka 20 mpaka 18, lakini ukiona *rate* ya Kodi ya Mapato, utaona kwamba, imebaki *standly* ni asilimia 30. Tangu tupate Uhuru mpaka leo, kodi hiyo imebaki kuwa ni *rate* ya *30.* Kiwango hiki ni cha juu sana kuliko sehemu nyingi duniani.

*Tendency* leo ni kupunguza *income tax.* Hata sisi Wabunge, fedha tunazopata hapa kiwango kikubwa, *30 percent,* inakwenda kwenye Kodi ya Mapato. Mapendekezo yangu ni hivi; kwa kuwa ulimwengu unapunguza Kodi ya Mapato, Uingereza wamepunguza mpaka asilimia 26. Je, Mheshimiwa Spika, unaonaje iwapo tukifanya *balancing* kati ya Kodi ya Mapato na *VAT?* Hiyo ndiyo *consumption tax.* *Tendency* kubwa katika ulimwengu wa leo ni kwamba, wanaotozwa fedha zaidi ni wenye mapato makubwa. Asilimia 80 ya Kodi ya Mapato hulipwa na watu 400 tu, yaani *large tax*

*payers.* Sehemu ambayo ni *Informal Sector* kama Tanzania, yaani biashara ya chini chini ama biashara ya magendo ambayo ndiyo kubwa zaidi, wao hawalipi mapato. Kwa hiyo, kama tukiongeza *VAT* na tupunguze Kodi ya Mapato, ninasema *balance* iwe namna hii; Kodi ya Mapato iteremke mpaka 24 na Kodi ya Ongezeko la Thamani ipande kutoka 18 mpaka 21, *balance* yake itakuwa nzuri sana. Serikali itapata kodi zaidi.

Ukiona leo Ufaransa, ambayo ndiyo ilikuwa nchi ya kwanza kabisa kubuni Kodi ya Ongezeko la Thamani, wao wanafanya *balancing*; sioni ni kwa nini sisi tusifanye? Ninaamini tukifanya hivyo, tutaongeza Kodi ya Mapato angalau *one third* kuliko tunayokusanya leo. Sioni mapendekezo ya Upinzani wala ya Serikali kuonesha kwamba, kweli tutaongeza Kodi ya Mapato kuweza kutukwamua kwa tatizo hili la kupata maendeleo.

Sehemu ya tatu, ambayo ninapenda kuchangia ni kuhusu *Public Private Partnership.* Ninachukua nafasi hii ya pekee, kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya, kuleta Muswada wa *PPP* mwaka jana na ninapozungumza, zile Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ziko tayari. Ninawapongeza sana na ndiyo wakati sasa watu binafsi wanaweza kuungana na Serikali kuongeza bidii ya maendeleo kwa Miradi mikubwa kama ifuatayo:-

Miradi ya Kuzalisha Umeme na Kusambaza Umeme Nchini na Miradi ya Barabara, maana kila mwaka Serikali inatenga fedha nyingi sana kuwekeza katika miundombinu. Serikali yenyewe haiwezi, lakini kwa kupitia Sheria hii, ninadhani Watu Binafsi wataungana mkono na Serikali ili waweze kuzalisha na pia kuongeza Mapato ya Taifa.

Ninatoa onyo na kuna changamoto nyingi za kufanya, mimi ninapendekeza kwamba, zile *units* mbili ambazo Serikali imesema *unit* moja ya kutoa mapendekezo ya uzalishaji, ninadhani wanasema *advertisement* na ile *investment incentive* ziende *TIC,* hapo sina tatizo. Tatizo kubwa ni kwamba, kitengo kingine kinakwenda Wizara ya Fedha, ninasema Wizara ya Fedha haiwezi kufanya tathmini nzuri ya kibiashara, maana kama tunavyoielewa, imeshindwa kuendesha *ATC* na hata imeshindwa kutoa fedha kwenda kwa vijana katika Bodi ya Mikopo *on time*. Siamini kama kweli inaweza kufanya kazi hii ya kuchambua; nani atafanya hizi *PPP?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, turudi nyuma tufanye ile *unit* ambayo ni *Technical* irudi *PSRC* ya zamani, ambayo leo tunaiita *Consolidated Holding.* Ukifanya hivyo, utakuwa umefanya wale wataalamu waweze ku-*analyze* mahitaji ya *Public Private Partnership* kitaalamu kabisa. Wao wana uzoefu mkubwa na ninadhani wanaweza kutusaidia kuliko kurundika jambo kubwa kama hili kwenye *bureaucracy* ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba utusaidie Miradi hii mizuri kama ya Elimu iweze kuungana na Miradi iliyo chini ya *PPP* ili tuweze kujenga sehemu kubwa ya mahitaji yetu kule Musoma Vijijini; kwa mfano, Hospitali ya Kwangwa ilikuwa inasuasua ninadhani kwa kipindi cha miaka 50, hakuna lolote linaloendelea pale.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hii ni kengele ya pili. Tunaendelea na msemaji anayefuata ni Mheshimiwa Kheri Ali Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hiyo, ninasema ahsante sana.

**MHE. KHERI ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, kwanza, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa mmoja kati ya Wabunge wanaoshiriki katika Bunge la Kumi.

Ninaomba niwashukuru Wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura Zanzibar, kwa kunipa ridhaa ya kuwawakilisha katika Bunge hili. Pia ninaomba niwashukuru Wana-CCM pamoja na Chama cha Mapinduzi, kwa kunipa nafasi ya kugombea nafasi ya Ubunge katika Jimbo la Kwamtipura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Rais wa Tanzania, Dkt. Jakaya Kikwete na Makamu wake, kwa ushindi walioupata wa kuliongoza Taifa hili katika Awamu ya Nne ya Uongozi wa Nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili, pamoja na Watendaji wake wote, kwa kutengeneza bajeti ambayo imegusa maeneo yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia sehemu ya Nishati na Umeme. Kwa mujibu wa Bajeti yetu ya Mwaka 2011/2012, tumeambiwa kwamba, tatizo la umeme linaweza likapungua kwa kiasi kikubwa, baada ya kupitishwa kwa Sheria ya *PPP* na kutengenezwa kwa *regulations* zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na mazoea huko nyuma kusikia vitu kama hivi kwa lugha nyingine kwamba, kina cha maji kipo chini, kwa hiyo, umeme hauwezi kupatikana wa kutosha. Sasa hii isije kuwa ni kubadilisha lugha tu kutoka kina cha chini cha maji kwenda kwenye kutekeleza Sheria ya *PPP* na *Regulations*. Ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba, hili pendekezo waliloweka hapa linafanyiwa kazi, kwa sababu hili ndiyo tatizo letu kubwa, kwani tunaweka mapendekezo lakini katika utekelezaji inakuwa ni kwa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa yameainishwa maeneo hapa ambayo yanaonekana kwamba, umeme utazalishwa, maeneo hayo ni kama Mtwara, Mpanga,

Tanga, Kilimanjaro na sehemu nyingine, ninadhani tungeangalia na maeneo mengine ambayo pia yana uwezo wa kuzalisha umeme. Kwa mfano, nilipata bahati ya kwenda Mchuchuma, kuna Makaa ya Mawe na Makaa ya Mawe ninaweza kusema ni *multipurpose* kwa sababu, kwanza, yanatumiwa katika viwanda na wakati huo huo yanazalisha umeme. Kwa hiyo, tukichimba yale Makaa ya Mawe, tutakuwa tumefanya kazi mbili kwa wakati mmoja.

Tanzania tuna viwanda lakini vinatumia makaa yanayoagizwa kutoka nje kwa fedha za kigeni. Kama makaa yale yatachimbwa, nina hakika matumizi ya hizi fedha za kigeni yatapungua. Kwa mujibu wa taarifa tulizozipata wakati tulipotembelea sehemu ya machimbo, tuliambiwa kwamba, makaa haya yalipelekwa Afrika Kusini baada ya kuchorongwa ili kupima *quality* yake. Watu wa Afrika Kusini kwa sababu ni nchi pekee inayofanya hivyo, yaani kuchunguza makaa, walisema Makaa ya Tanzania ni ya *first class*.

Hivi sasa makampuni ya hapa Tanzania yananunua makaa Afrika Kusini, lakini ni ya *low quality*. Sasa tukipata makaa haya, tuna hakika viwanda vyetu vitatumia makaa mazuri na vilevile tutaokoa fedha za kigeni badala ya kuzipeleka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huohuo tutapata umeme ambao tutausambaza, kuondoa tatizo la umeme hapa Tanzania, ambalo sasa hivi limekuwa kubwa sana katika nchi yetu na sote tunafahamu umuhimu wa umeme katika Uchumi wa Taifa. Kwa sababu hata Zanzibar pia tunatumia umeme wa TANESCO, kwa hiyo, tatizo la umeme linapotokea kama ni mgawo au kama umeme haupatikani, basi na sisi Zanzibar tunaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia sehemu ya umeme, ninaomba sasa niende sehemu ya pili ya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mashirika ya Umma, tumeambiwa kwamba, Kitengo cha *TR*, yaani *Treasury Registrar*, kinaimarishwa ili kusimamia vizuri mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua nchi yetu ni ya ujamaa na kujitegemea na moja kati ya misingi ya ujamaa na kujitegemea ni kuweka uchumi mikononi mwa Wananchi. Njia moja ya kuweka uchumi katika mikono ya Wananchi kwa nchi maskini kama yetu, ambayo watu wengi hawana mitaji ni kuunda Mashirika ya Umma ili kudhibiti hizo njia za uchumi. Sasa mashirika mengi yameundwa, lakini kama ilivyoelezwa kwenye Kitabu cha Bajeti ni kwamba, hayajiendeshi na hayatengenezi faida. Sasa ni vizuri tunapoyakabidhi haya Mashirika kwa Hazina, tuwe tumewakabidhi pamoja na uwezo, kwa sababu katika moja ya mambo tuliyogundua katika Kamati wakati tunayaita Mashirika ni kwamba, mambo yanapofanywa na Mashirika inatakiwa Hazina waarifiwe au watoe ushauri, lakini hawaarifiwi wala ushauri wao hautolewi.

Kwa hiyo, hiki Kitengo cha Hazina ni vizuri Sheria yake ikawekwa na wakatungiwa na *Regulations* zake katika kusimamia Mashirika pamoja na Wakala. Bila

kufanya hivyo, hawatakuwa na uwezo wa kufanya kitu chochote; ni sawa na kama ni Kitengo cha Ushauri tu, waende pale waangalie Shirika linafanya nini, warudi halafu basi. Tukiwapa Sheria na *Regulations* zao na tukiwapa uwezo wa kusimamia vizuri Mashirika yote, ninaamini Mashirika yote ambayo yanapata hasara yatapata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo na Serikali iache kuyaingilia sana Mashirika, kama Mheshimiwa Rais alivyotoa kauli kuiagiza Serikali kwamba, sasa iache kuyaingilia Mashirika, Mashirika yaachiwe Bodi za Wakurugenzi pamoja na Bodi za Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mzuri; moja ya Mamlaka ambayo imetungiwa Sheria na kupewa *Regulations* ni *TIRA. TIRA* ni *Tanzania Insurance Regulatory Authority*. Ilipoundwa ilitungiwa Sheria na Bunge mwaka 1996 na ikatungiwa na *Regulations* zake. *TIRA* inasimamia Mashirika yote ya Bima Tanzania. Mashirika yote ya Bima Tanzania yanajua kwamba, yakifanya kosa fulani hukumu yake ni fulani. Sasa Mashirika yetu mengi hapa Tanzania tukiondoa Bima, hayajui wanajifanyia mambo wanavyotaka wenyewe, wanajua kwamba, hakuna lolote. Leo Shirika la Bima limeelezwa waziwazi kwamba, likifanya kosa Fulani, Shirika lenyewe litalipa faini kiasi fulani na *Chief Executive Officer* atalipa kiasi fulani. Sasa kama *Chief Executive Officer* haguswi katika ku-*fail* kwa Shirika, Shirika halitakwenda. Lazima *TR* tuwaundie *Regulations,* pamoja na meno ya kuweza kuitumia hii Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yamezungumzwa katika usimamiaji wa Mashirika ya Umma, ambayo *TR* inatakiwa iyashughulikie. Ninadhani kwa vile nilizungumzia *Regulations,* basi baadhi yake yangefaa yakawa katika hizo *Regulations*. Kwa mfano, kama suala la kutekeleza ukaguzi wa kimenejimenti kwa Wakala, Taasisi na Mashirika, kuandaa mfumo wa mperembaji, mhakiki, hayo yote yataingizwa katika *Regulations* ili kumwezesha *TR* kusimamia vizuri haya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni ya uboreshaji wa mfumo wa kodi na tozo na hatua nyingine za mapato. Miongoni mwa maeneo ambayo yameguswa katika kipengele hiki ni Sekta Isiyo Rasmi kama eneo la kuingizwa katika Mfumo wa Kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kusema kwamba, ilipotajwa Sekta Isiyo Rasmi, haikuwekewa ufafanuzi kwa sababu sekta isiyo rasmi ni pana sana, inahusisha eneo kubwa sana na inahusika na watu wengi sana. Sasa nina wasiwasi na ninaomba Serikali iwe makini sana katika eneo hili, kwa sababu lisije likatokea tatizo la kuleta vurugu. Sekta Isiyo Rasmi iangaliwe kwa umakini na ingekuwa vizuri kama ingekuwa imechanganuliwa ili kueleza itahusisha eneo fulani na Fulani, lakini hapa imewekwa *in general*, yaani Sekta nzima.

Tunajua kwamba, katika Sekta hii kuna Sekta nyingine ambayo sisi wenyewe Wabunge humu tunaisaidia, kwa sababu hali zao ni za chini; hawana uwezo, tuwasaiadie wainuke. Sasa leo ukisema unawaingiza katika kodi, maana yake unataka uwanyang'anye ule mtaji ambao siyo mkubwa. Hata hivyo, ni mtaji ambao labda

unatokana na posho za Waheshimiwa Wabunge kuweza kuwasaidia kujiendesha kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni nia ya kuongeza mapato ya Serikali, ninadhani kuna maeneo tungeyaangalia sana. Kuna maeneo ambayo tunayabuni kama ni vyanzo vya mapato, lakini baadaye tunayaacha. Uzuri wa kubuni maeneo ya vianzo vya kimapato ni kwamba, uvianzishe vile vyanzo, uvisimamie na baadaye kuviboresha ili vizalishe zaidi. Ukisema tuvianzishe vyanzo tu halafu baadaye tunakaa, leo umepata milioni moja mwaka unaofuata unapata laki tano, kwa kweli hicho chanzo kinakuwa hakileti faida. Tuviimarishe vyanzo vyetu vya mapato tulivyonavyo ili tuhakikishe kwamba, mapato kila mwaka yanaongezeka kwa vyanzo vilevile na wakati huo huo tunabuni vyanzo vipya ili kuvijazia katika vyanzo tulivyonavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kusema kwamba, kuna maeneo ambayo tumeyaweka kama ni ya kutuingizia mapato; kwa mfano, kuna wawekezaji ambao wapo hapa nchini, kuna wawekezaji wanakuja hapa walisha-*plan* kabisa; kwa mfano, tulipotembelea Mradi wa Liganga, tuliwauliza wawekezaji kwamba, wanategemea kwamba *pay back period* ya *investments* zao ni miaka mingapi? Mmoja akasema ni miaka saba, lakini mwingine akasema hapana ni miaka miwili.

Sasa nina wasiwasi kwamba, katika eneo hili inawezekana huyu mwekezaji akakaa miaka miwili akisharejesha *capital outlay* yake aliyowekeza, atauza hisa zake na atapata *super profit* ataondoka nchini, kwa sababu sheria zetu ni dhaifu hasa katika suala la ongezeko la mitaji, yaani *capital gains.*

Kwa hiyo, ningeshauri Wataalamu wetu tuwape ujuzi zaidi wa kutengeneza sheria, ambayo itawabana wawekezaji, kwa sababu hapa kwetu hawalipi *capital gains,* lakini kwa nchi za wenzetu wanalipa.

Sasa labda wataalamu wetu wangekwenda kule kusoma sheria zao zikoje na zetu zikoje, hata ikawa kule wanalipa na hapa hawalipi.

Vilevile tukajua kwamba, sasa hivi wanapokuja wawekezaji basi tunajua kwamba, tutapata kipato fulani baada ya miaka fulani. Kama hilo haliwezekani, tuwe na *Tax Agreement* katika nchi wanazotoka wale wawekezaji, tukae na nchi zile tukubaliane utaratibu wa kulipa kodi kwa wawekezaji ambao wanakuja hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani kwa kufanya hivyo, mapato yetu yatainuka na tatizo la uchumi katika nchi yetu linaweza kuondoka. Nchi yetu ni tajiri sana, kwa sababu wakati tulipotembelea kule Ludewa, tulisikitika sana sisi wengine; mimi ninatoka Zanzibar lakini nilipokuta hali ya Ludewa Liganga ilivyo, nilisikitika sana kwa sababu kule hakuna jiwe, kila jiwe unalolishika ni chuma na mengine yameshaweka kutu …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. KHERI ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Kheri Ali Khamis, kwa mchango wako. Ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay.

**MHE. MUSTAPHA BOAY AKUNAAY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba niungane na wenzangu, kumtakia Rehma Marehemu Mama yake Spika wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, ninataka kuwasalimia wapiga kura wangu wa Wilaya ya Mbulu; kwamba, tuko Bungeni kwenye Bajeti na Bajeti ndiyo kama inavyosomwa na mikiki ni kama hivi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wenzangu wengi wameshazungumzia mapato yaliyopo na matumizi yalivyopangwa, labda nianze na mapato ambayo yameachwa nje ya kapu, yaani mapato ambayo Serikali haijatoza kodi mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika Kitabu cha Bajeti, vyanzo vya ndani, 53% ya bajeti nzima; hiki ni kiasi kidogo sana na ni cha hatari, kwa sababu iwapo kiasi ambacho kinategemewa kutoka nje kama hakijapatikana kwa sababu yoyote ile ambayo itatokea duniani, basi ina maana Bajeti yetu itakuwa imekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo ambavyo Serikali ilitakiwa ivitazame na vya hakika ni kupanua wigo wa Kodi ya Mapato. Kodi kubwa ya mapato haikusanywi, kwa mfano, Kodi ya Mapato kwenye *Super Markets; Super Markets* kubwa zinalipa shilingi 291,000 kama *presumptive tax*, lakini hiyo ni hela ndogo ukilinganisha na mfanyakazi wa Serikali ambaye ni wa kima cha kati, anayepata shilingi milioni kama mbili yeye analipa shilingi laki tano kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo ambavyo Serikali ilitakiwa ivitazame na vya hakika ni kupanua wigo wa kodi ya mapato. Kodi kubwa ya mapato haichukuliwi. Kwa mfano, kodi ya mapato ya *Super Markets*. *Super Markets* kubwa zinalipa Sh. 291,000/= kama *presumptive tax,* lakini hiyo ni hela ndogo ukilinganisha na mfanyakazi wa Serikali ambaye ni wa kima cha kati anayepata shilingi milioni kama mbili, yeye analipa laki tano kwa mwezi. Ina maana kwa mwaka ni kama shilingi milioni sita. Kwa hiyo, kama hizo *presumptive tax* hao watu wa *presecutive* wangefuatwa zaidi na wakalipa kodi ambazo zinastahili badala ya sasa hivi wanapolipa *provisional tax* za Sh. 70,000/= kwa kila miezi mitatu na kuacha pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutegemea *taffic notification* kama kianzio cha kodi cha mapato kama trafiki anayomtoza mtu Sh. 50,000/= barabarani, hiki ni kitendo cha hatari sana, kwa sababu tunatengeneza kosa litendeke ili tupate mapato badala ya kuwashauri watu wasitende makosa. Tunawategemea watende kosa ili pesa ipatikane.

Eneo hili ni hatari kwa sababu watu wengi wanaoendesha pikipiki, magari yaliyozeeka ambayo ni ya wakulima wetu watakamatwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwarejeshe kwenye kumbukumbu kwanini kulianzishwa *traffic notification*. *Traffic notification* ilianzishwa ni kuzuia kesi nyingi zisiende Mahakamani kwa ajili ya makosa madogo madogo barabarani ambayo mkosaji atakubali kosa hilo apigwe faini pale Sh. 5000/= au Sh. 10,000/= na mwisho kabisa iwe Sh. 20,000/=. Sasa ikiongezwa kwenda Sh. 50,000/=, basi watu wengi wataamua kwenda Mahakamani wasilipe na wadai ushahidi uje. Kwa hiyo, badala ya kulipa hizo wanazolipa pale barabarani tutajaza tena Mahakama kesi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wanafahamu njiani magari yanavyosimamishwa na matrafiki. Sasa trafiki wataanza ku-*negotiate*, ama wataanza kupatana, kama huwezi kutoa Sh. 50,000/=, basi lipa Sh. 20,000/=. Kwa hiyo, ile Sh. 20,000/= ndiyo itahalalishwa kuwa ndiyo pesa zinazopotea njiani. Sijasema trafiki wanachukua rushwa, lakini ninasema zitapotea njiani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuzungumzia kuhusu mapato ambayo yameachwa nje. Katika Sekta ya Utalii kama msemaji mmoja alivyozungumza, tungekuwa na ndege inayomilikiwa au ambayo inakuwa na usajili hapa Tanzania na kusafiri kwenda sehemu ambazo watalii wanatoka, tungekuwa na mapato mengi sana. Kwa mfano, mwaka 2009 katika utalii wa kimataifa, Tanzania ilipata shilingi trilioni moja na nusu (trilioni 1.5) ambayo ni robo tu ya mapato ya ndani ya sasa. Hiyo ni kwa sababu hatuna ndege ya kwetu, '*National carrier*.' Kutokuwa na *National carrier* tunakosa asilimia 60. Asilimia 60 inatumika katika usafiri. Kwa lugha ya utaalamu wa kiuchumi, wanasema kuna *leakage of income.* Sasa *leakage* ya asilimia 60 ungeizuia na kupata mapato hayo iwapo ungeamua kuwekeza katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa katika utalii wa hapo hapo kuna utalii hapa ndani ambao unaitwa utalii wa kiutamaduni ambao hauhitaji mtaji mkubwa huu ni *pro-poor tourism* ambayo Serikali imeiweka kwenye *policy* yake kwamba kuwe na utalii wa kitamaduni ili watu wetu wawekeze huko. Sasa kama Serikali ingewekeza zaidi katika usalama kwa ajili ya utalii huu, basi tungepata pesa zaidi kuliko kutegemea zaidi pesa za trafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu *skilled development levy (SDL)*. Ni jambo la busara kuongeza mfuko wa mkopo wa vijana wetu wanaosoma Vyuo Vikuu, lakini tukumbuke kwamba hii *SDL* makusudio yake mwanzoni kabisa ilikuwa ni pesa za kusaidia kuwe na watu ambao ni *skilled* hapa Tanzania, ndiyo maana ikaitwa *vocational training levy.* Sasa hii inategemea kama waajiri wataajiri watu wengi na kulipa asilimia sita ya mshahara wote wa mwezi. Sasa kutokana na hali ya umeme kupungua, hali ya mazingira ya uzalishaji kutokuwa nzuri, wafanyakazi wakipunguzwa, mishahara itapungua. Ina maana basi, hiyo *SDL* nayo itapungua. Basi siyo sehemu nzuri ya kutegemea kwa ajili ya Mfuko wa Elimu kwa sababu mfuko utayumba.

Kwa hiyo hapo mimi ningeshauri kwamba Serikali ingeanzisha kodi nyingine ambayo italipwa na watu wote. Hii *SDL* inalipwa tu na waajiri ambao nao sasa hivi wana malumbano na Serikali kwamba wao wanapolipa hii kodi inawasaidia vipi? Wanadai hii kodi wapate sehemu ambayo wao watapata kwa wafanyakazi wao mafunzo kwa sababu sasa hivi *ZDL* inapelekwa yote kwenye *training institutions* ambazo zinatoa *skills training*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye *East African Federation - monetary union* na tunahitaji wataalam, na wataalamu hawatakuwa ni *academicians,* ni watu ambao watatokana na vyuo vinavyofundisha *skills*. Iwapo tutapunguza hizi pesa zikaenda kwenye Vyuo Vikuu bila kurejesha kiasi fulani, huku itakuwa hatujafanya vizuri. Kwa hiyo, hapo mimi ningeshauri kwamba Serikali itafute kodi nyingine ambayo itajaza huo mfuko wa kodi badala ya kutegemea *skills development levy* kugawanywa hiyo asilimia sita ambayo waajiriwa hapa Tanzania ni wachache, waajiri ni hao *private sector* ambao uchumi ukiyumba na wao wanafanya *retrenchments*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa ningependa nizungumzie juu ya kuboresha viwanda. Viwanda vikiboreshwa siyo vya mjini tu, viboreshwe pamoja na umeme katika vijiji, kwani msingi wa bajeti hii ni kukuza uchumi na kuondoa umasikini. Sasa ili uondoe umasikini, lazima utazame hawa wakulima na wanaokaa vijijini.

Kwa hiyo, suala la umeme vijijini limeangaliwa katika sehemu ambayo madini na nishati wamepewa pesa, wamepewa pesa ndogo sana. Kwa ajili hiyo hali ya kumwezesha Mtanzania kukua kiuchumi bado itakuwa ni ya kusikitisha. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba Serikali itazame upya eneo hili kuwezesha wananchi walioko mashambani waweze kuongezewa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni miundombinu. Nimeona Wizara ya Ujenzi inapata shilingi trilioni 1.5. Kwa hiyo, barabara ambazo zinahitaji zitazamwe zaidi ni zile ambazo zinatoka sehemu za mazao ya biashara, hasa maeneo ya Mbulu, Mwanza, Hanang, Rombo, Iringa, na kadhalika sehemu ambazo kahawa inalimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hapo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mustapha Akunaay, naona hoja yako ya mwisho imeungwa mkono karibu na Wabunge wote. Kwa hiyo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Vita Kawawa, halafu Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu ajiandae.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami nitoe mchango wangu katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru wananchi wa Namtumbo walionipa fursa hii tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano kuja kuwawakilisha. Naomba niwahakikishie kwamba sitawaangusha, nitawawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuiwasilisha vyema hotuba yake Bungeni, lakini pia Watendaji waliosaidia kuandaa bajeti hii. Ili bajeti iweze kutoa majibu yaliyokusudiwa, lazima tujielekeze katika utekelezaji wa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rita Mlaki, unavunja utaratibu.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujielekeze katika yale yaliyokusudiwa na kuwasilishwa Bungeni na kupata idhini ya Bunge na kwenda kufanyiwa kazi inavyotakiwa. Sina budi kutoa ushauri kwamba lazima tushirikiane, kila mtu katika sekta yake. Katika eneo lake la kazi kila mtu afanye kwa bidii ili kukuza fursa hii tuliyonayo ya kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alieleza kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia MKUKUTA II, hasa katika vipaumbele vinavyogusa wananchi walio wengi. MKUKUTA II umejikita katika maeneo muhimu ya miundombinu, kilimo, sekta ya viwanda yenye lengo la kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi hasa za ndani, lakini ya kilimo na mengine dhana ya sekta ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya MKUKUTA II ni vipaumbele ambavyo viko pia katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi wa haraka kama alivyosema Waziri katika hotuba yake aya ya 92 ukurasa wa 50 (6) akiwasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi na malengo ya uchumi katika kipindi hiki cha mwaka 2011/2012 – 2015/2016 alisema kwamba raslimali zote zitaelekezwa kwenye maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali katika eneo hili kwa kutambua hilo, imeweka bajeti katika kilimo Sh. 926,200,000,000/= na itaendelea kuongeza usambazaji wa pembejeo za kilimo na zana bora kwa wakulima zaidi ili kuongeza tija na uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ni muhimu sana hasa tukichukulia maanani kwamba zaidi ya asilimia 75 ya wananchi wa Tanzania ndio wamejiajiri katika eneo hili. Naiomba Serikali tuelekeze raslimali kama tulivyokusudia kukuza uchumi. Nitatoa mfano. Kuna sekta ndogo tu ya kilimo ambayo inachochea sana ukuaji wa uchumi kwa haraka. Kwa takwimu za haraka nilizonazo, sekta hiyo ndogo naitilia mkazo na kutoa takwimu zake ili Serikali iiangalie sana iweze kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mwaka 2006 sekta hii iliingizia wakulima Sh. 60,976,000,000/= lakini iliuza nje kwa dola za Kimarekani milioni 65 mauzo ya nje. Mwaka 2007 ilipanda tena ikawaongezea wakulima shilingi bilioni 75, lakini iliuza mauzo yake nje kwa fedha za

kigeni shilingi milioni 87. Mwaka 2008 ilikwenda mara mbili ya hapo, wakulima waliingiza fedha shilingi bilioni 170.393 na mauzo ya nje yakafikia dola milioni 176. Mwaka 2009/2010 wakulima hao waliuza kwa shilingi bilioni 317, lakini mauzo ya nje yalifikia dola milioni 232. Mwaka 2010 kati ya mauzo ya dola milioni 500 ya mazao makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikiendelea zaidi, kodi ya ndani katika sekta hii ndogo mwaka 2006 ilichangia tozo la kodi shilingi bilioni 65; mwaka 2007, shilingi bilioni 80; mwaka 2008, shilingi bilioni 93; mwaka 2009, shilingi bilioni 98 na mwaka 2010, shilingi bilioni 110. Katika mapato ya Halmashauri, sekta hii ilichangia shilingi bilioni tatu mwaka 2006; Sh. 3,600,000,000/= mwaka 2007; mwaka 2008, shilingi bilioni nane na mwaka 2009, shilingi bilioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii naomba ku-*declare interest* kwa mujibu wa Kanuni ya 61 kwamba ni Sekta ya Tumbaku na mimi ni Mwenyekiti wake. Naiomba Serikali iiangalie kwa kina sekta hii kwa jinsi gani inavyochochea ukuaji wa uchumi wa haraka kwa wananchi wake na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye chakula, jana nilisikitika kusikia kwa wenzetu, Mheshimiwa Masele jana wakati anatoa hotuba yake alisema watani wetu kule wanapewa mahindi Shinyanga mpaka Kahama kule kilo 10 kwa kaya. Iliniuma sana kwa sababu sisi Mkoa wa Ruvuma mwaka jana Serikali imenunua kwenye Hifadhi ya Taifa tani zaidi ya 50,000 na tunacho chakula hicho kwenye maghala. Serikali imetoa tani 10,000 tu na sasa hivi ziko zaidi ya tani 40,000 kwenye maghala yetu na mwaka huu tunategemea zaidi ya tani 120,000 wakulima wetu watavuna. Mvua zimekwenda vizuri, mbolea Serikali ilisambaza vizuri sana na tunategemea tani 120,000 za chakula na kwenye maghala ziko tani 40,000. Tunaomba Serikali mje mwondoe kile chakula muwapelekee watani wetu wale. Iramba nao nimeambiwa wana njaa, tunaomba muwapelee chakula hicho ili sisi chakula tunachokivuna sasa hivi kiweze kuingia kwenye maghala yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali katika eneo lingine la miundombinu. Kwetu kule barabara ya kutoka Peramiho kwenda Mbinga inajengwa. Barabara kutoka Songea kuja Namtumbo inajengwa, zote kwa kiwango cha lami, lakini pia barabara kutoka Namtumbo kwenda Tunduru mkandarasi ameshapewa na yuko katika *mobilisation stage*. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali katika kuona umuhimu wa eneo letu lile ambalo lazima tulifungue ili chakula kiweze kuletwa kwa haraka katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niishukuru Serikali kwamba mwaka jana Namtumbo na Songea Mjini tulitengewa fedha katika bajeti iliyokwisha, mwaka huu kulileteawa majenereta ya umeme. Tunashukuru sana, mkandarasi yuko katika *site* Songea Mjini akiweka kitako cha kuweka majenereta hayo, na nimeambiwa kwamba akimaliza kuweka kitako pale, anakuja Namtumbo na Mheshimiwa Waziri amenihakikishia mwezi Desemba umeme utawaka Namtumbo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie eneo hili la mafuta. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuona ipo haja ya kupitia na kukokotoa tozo zinazotozwa na mamlaka mbalimbali kwa lengo la kuzipunguza ili kupunguza mzigo wa bei ya mafuta. Lakini ukitazama kwa watozaji, yaani zile mamlaka zinazotoza tozo mbalimbali za mafuta, zipo kisheria na zilitungwa na Bunge letu humu ndani zifanye kazi gani. Lakini juu ya yote wana toza tozo nane na tozo hizi kwa ujumla wake ni asilimia 2.6 au ni wastani wa Sh. 47.76 na kuna tozo nyingine zinatozwa na makampuni ya mafuta asilimia 2.09. Lakini pia malipo ya wasambazaji asilimia 8.98 na kodi ya Serikali asilimia 18.58 lakini pia kwa wastani wa mafuta yote yanayoingizwa kwa maana ya dizeli, petroli na mafuta ya taa. Pia kuna gharama hizi za tozo 13, gharama ya manunuzi ni asilimia 67.72.

Ushauri wangu ni kwamba, naomba sana wataalamu wawe makini sana hapa wanapofanya mapitio ya zoezi hili, ili waje na majibu yatakayoleta *impact* katika kupunguza mfumko wa bei. Naiomba Serikali ielekeze vizuri wataalamu waangalie yale maeneo yanayotozwa kwa asilimia na hapo hapo kwa dola. Haya maeneo nayo yanaumiza sana au yanaongeza sana tozo katika bei ya mafuta. Naomba Wizara iangalie sana maeneo haya tozo linapotozwa kwenye asilimia, lakini kwenye dola. Dola inapopanda bei vile vile bei ile inapanda. Kwa hiyo lazima tuangalie na tuwe na *flat rate* kama tunajua ni Sh. 200/= kwa tani, basi tunajua hela ya Kitanzania ni Sh. 200/= kwa tani. Naiomba Serikali iangalie pia eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali pia iangalie eneo lile la *ceiling addition* ambalo linawapa mwanya wafanyabiashara kuongeza bei la asilimia 7.5. Eneo hili linaweza kuangalia na kupunguzwa, nalo linaweza likatusaidia. Lakini pia tuangalie ile tofauti ya *fuel levy* ya mafuta ya taa na dizeli. Naomba Serikali nayo iangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Serikali kwa uamuzi wake wa kuamua kuweka utaratibu wa ile *bulky consignment* au *bulky procurement* ya mafuta. Naomba kuitahadharisha Serikali katika utaratibu huu, sehemu ile ya kuhifadhia mafuta *out storage facility* iwe asilimia 100 ili imilikiwe na Serikali tusije tukadanganywa kuingia ubia katika eneo hili. Naiomba sana Serikali, hili ni kwa ajili ya Usalama wa Taifa pia.

Leo hii kwenye hifadhi ya chakula hatuingiliani, hatuna ubia na Serikali. Kwenye hifadhi ya mafuta pia kuwe kwa ajili ya Serikali. Huo ndiyo ushauri wangu. Lakini sio kwamba nazuia, Makampuni binafsi wasiendelee na utaratibu huo waendelee nao wa *bulky consignment*, waendelee nao kwa utaratibu wao waliojiwekea, lakini pia Serikali sasa hivi imeanza katika utaratibu huu, utaratibu wa kujenga boya kule *out anchorage*, ambalo litakuwa linapokelea yale mafuta. Lakini pia eneo lile naomba Serikali kwa ushauri wangu limilikiwe kwa asilimia mia moja na Serikali. Wafanyabiashara kama wao wana utaratibu wao wa *bulky consignment* au kufyonza mafuta yao waweke *pipeline* zao kutoka pale. Hii ni kwa ajili ya ku-*control,* lakini pia *income* kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ulikuwa huo. Naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa kwa mchango wako na hasa kwa kweli kwa kuhimiza chakula kibebwe kule Kusini wapelekewe watu wenye njaa. Nadhani hilo ni la muhimu sana.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Mchungaji Israel ajiandae.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti na hotuba inayohusu Mpango wa Serikali kama ulivyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwanza nianze kabisa kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini ambao wamenipigia kura na kunipa fursa ya kuingia katika chombo hiki muhimu katika mihimili yetu ya nchi. Lakini nianze tu kwa kumpa pongezi Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo - Waziri wa Fedha ambaye amewasilisha bajeti inayokidhi matakwa halisi ya Mtanzania kwa hivi sasa.

Pia napenda nimpe pole Mheshimiwa Stephen Massatu Wassira - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) ambaye katika majumuisho ya hotuba yake alizungumza mengi sana mazuri, lakini wale ambao hawataki kusikia hawakuyasikia na hawakuyaelewa. Pole sana Mheshimiwa, lakini nakupongeza. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, pole yako ipitie kwenye Kiti na isiende moja kwa moja kwa Mbunge. Utaratibu unaki-*address* Kiti na sio Mbunge aliyepo ndani.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda nimpe pongezi Mheshimiwa Abdallah Kigoda - Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa hotuba yake nzuri ambayo ilitoa mapendekezo yanayoainisha ni jinsi gani ambavyo Serikali inaweza kuboresha bajeti husika. Ninayo michango mingi tu, lakini naomba nizungumzie machache kutokana na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchangia katika eneo la kilimo. Tuimarishe kilimo kwa kuwapa wananchi zana bora. Bajeti yetu ya kilimo bado inabidi tuangalie uwezekano wa kuipatia kima zaidi kwa sababu huu mpango wa matrekta madogo, yaani *power tillers,* baadaye hapo nitaungana na Wizara husika kama tutakuwa na mpango wa kuboresha na kuwapatia wananchi zana bora zaidi. Lakini katika eneo hili, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, yapo maeneo ambayo naona kidogo inabidi wataalamu na Waziri mwenyewe waangalie. Wananchi haswa wa Jimbo la Kilwa Kaskazini wanafanya jitihada zao, lakini kwenye uwajibikaji kuna mapungufu. Nitatoa mfano katika eneo moja. Kwa mujibu wa *Finance Act, 2006* kipengele cha 10(a) *subsection (1) and (2); Subsection (1)* inasema kwamba: "Asilimia 10 ya *export levy* kwenye korosho inabidi irudishwe katika maeneo ya Wilaya husika." Katika mgawanyo ule, asilimia 6.5 zitagawanywa katika Halmashauri zote zinazolima korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha, aidha kwa makusudi ama kwa kutokuzingatia, fedha hizi hazijawahi kufika kwenye Halmashauri yoyote inayolima korosho. Pia, lipo eneo linguine, hivi sasa ni wakati wa mavuno, tukiangalia katika maeneo ya *export*, hakuna mapato ambayo yanaonyesha ni rejeshi kwa wakulima zaidi ya kupewa zile pembejeo. Kwa hiyo, naishauri Serikali, kama jinsi ambavyo sheria inatamka, basi itekelezwe ili kuweza kupunguza dimbwi la umasikini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uvuvi, maana yake Jimbo ambalo nimechaguliwa, tuna sehemu ya bahari na tuna sehemu ya nchi kavu. Nimeangalia mapato ya Serikali kutokana na mazao yanayotokana na uvuvi ni dola bilioni 41. Lakini tukigawanya, sisi kule hatuna madini kama maeneo mengine ya wanzetu kule kama maeneo ya ukanda wa Ziwa ama maeneo ya Shinyanga, Tabora, na kadhalika, hatuna madini. Wenzetu hawa wananufaika kupata *royalty*. Basi katika mfumo huu, tuangalie fedha zinazopatikana tuwapelekee wananchi nao vile vile watumie katika shughuli nyingine za maendeleo badala ya fedha hizi kuingia katika mfuko moja kwa moja Serikalini ambapo sisi hatuna kitu kingine cha ku-*substitute*. Katika hilo, naamini kabisa Serikali italiangalia na kulizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukizungumzia hapa katika bajeti hii, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumzia suala la Serikali kukopa katika Taasisi binafsi za fedha. Mimi naona ipo haja ya Serikali kuangalia kwa umakini zaidi eneo hili kwa sababu wanapokwenda kukopa kwenye Taasisi za fedha, ina maana wao wana-*dominate* ile *market*, matokeo yake mabenki yale hayawezi kukimbilia kumkopesha mtu wa chini, wanakimbilia kuikopesha Serikali kwa sababu wao ndio ambao wanaaminika zaidi kuliko wananchi. Kwa hiyo, katika hili tupunguze mikopo ambayo inahusu Taasisi binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia, Serikali imeridhia, sio mara moja, ni mara kadhaa kuondoa kodi na tozo mbalimbali ili kuweza kupunguza gharama zile zinazotozwa katika bidhaa. Lakini mwitikio unakuwa ni mdogo sana, Serikali inapunguza kodi ambayo tunaamini kabisa inapotoa kodi au tozo, hizi bidhaa zinashuka bei. Lakini bidhaa hazishuki bei na bado tunaendelea, Serikali inakosa mapato, lakini vile vile mlaji ambaye ni mwananchi wa kawaida hana fursa ya kupata punguzo au unafuu wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ipo haja ya kuangalia huu mfumo. Soko huria kwa mujibu wa wenzetu, nchi zote duniani wana soko huria. Lakini lazima kuwe kuna kitu ambacho kina-*control*. Amerika yenyewe ambayo ndiyo mabingwa wa soko huria, lakini kuna *bureau* ambayo inasimamia *price control*. Haiwezekani leo uende kwenye duka hili ukaambiwa mchele kilo moja Sh. 1,000/=, ukienda katika duka lingine mchele unaowiana vile vile unauzwa Sh. 1,500/=. Tume ya Bei tuirudishe tuangalie upya, haya masuala sio tukubali kila tunachoambiwa. Tume ya Bei inaweza ikafanya kazi na isingiliane kabisa na matakwa ya masharti ya soko huria ili tuweze kumlinda mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kwenye suala la maji. Lakini suala la maji kutokana na mfumo wa bajeti hii naomba nilizungumzie kwa ujumla na suala la elimu na afya. Kwa mujibu wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, fedha nyingi sana inaonesha zimekwenda mijini. Ukiangalia bajeti ya maji kwa maeneo ya mijini, ni shilingi bilioni 291.5 na maeneo ya vijijini ni shilingi bilioni 37.4. Namna hii ndiyo inayopelekea wananchi wote sasa kutaka kutoka vijijini kwenda mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la afya, hiyo *basket fund,* Mkoa mmoja ambao sitaki kuutaja unapokea fedha ambazo zinazidi zaidi ya Mikoa 10. Sasa wananchi wengi wako vijijini, kwa nini tusipeleke huduma bora za afya, maji na elimu katika maeneo ya vijijini tunakimbilia kulundika fedha zote katika maeneo ya miji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie deni la Taifa. Serikali kwa mujibu wa bajeti hii iliyowasilishwa hapa, imepanga kiasi cha fedha kama sikosei kwa takwimu ni shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya kulipa madeni ya ndani. Naomba katika madeni haya ya ndani tuangalie zaidi madeni yanayohusu watumishi. Kuna walimu, Wauguzi, Wahudumu wengine wa Afya, Askari Polisi, Wanajeshi na kadhalika wanadai mafao yao kwa miaka. Sasa kama tunakusudia kutumia fedha hizi kwa ajili ya deni la ndani, basi tumalize ili kwenye kamusi yetu matatizo haya yasiwepo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo la umeme, lakini kwa sisi watu wa Kilwa tatizo hili sio kubwa sana. Kwa sababu umeme tunao Somanga unazalishwa, lakini fedha ambazo zimetengwa mara zote zinahusu umeme kusafirishwa kutoka Kilwa kwenda katika maeneo mengine wakati kuna vijiji vya jirani kabisa kama Somanga yenyewe ambapo umeme unazalishwa, umeme bado haujafika. Maeneo ya Tingi, Mtandango, Miteja ambako ndio nyumbani, hakuna umeme na umeme umepita pale. Sasa katika upangaji huu wa bajeti ni lazima tuangalie jinsi gani ambavyo tunaweza tukafanya kusaidia maeneo ya vijijini kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ningependa nichangie ni kuhusiana na suala la wanafunzi. Hivi sasa tumekaa tunazungumza hapa Bungeni wanafunzi wengi wamerudishwa kutokana na kugoma na kuanza maandamano ambayo kwao wanaamini yanawasaidia. Mimi nawashauri wanafunzi wenzangu, tukubaliane wakati mwingine na jinsi mambo yalivyo. Serikali inafanya jitihada, na moja kati ya jitihada hizo hata hiyo UDOM ambayo tunaizungumzia sasa hivi, watu ndio kimbilio lao kwenda ku-*propagate* huko, imejengwa na Serikali hii hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuiomba Serikali ifikirie upya uamuzi wa kuwarudisha wanafunzi hawa na wazazi vile vile tukubali kuwashauri watoto wetu tujue kwamba Serikali inafanya vyema zaidi kwa kile tulichonacho. Hatuwezi kujitanua kwa kiasi hicho. Lakini na Serikali mwangalie mtoto anapokosa siyo tukimbilie kumwadhibu tu, lakini ipo haja ya kuangalia namna ya kuwaelimisha kwa sababu mtoto anapokuwa mwanafunzi ndiyo anajifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kushukuru kwa kunipa nafasi na mchango wangu ni huo, naomba nizingatie hili kwa sababu wenzangu wanaweza wakawa na maoni na mchango mzuri zaidi ya ule ambao nimeutoa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Murtaza. Tunaendelea na mchangiaji anayefuata, nadhani hata mchango wako wewe pia una umuhimu mahali pake. Nimesema atakayefuata ni Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Mchungaji Israel ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama hapa leo nikiwa mwingi wa afya, nashukuru sana. Pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza, naomba kwa moyo wa dhati kabisa niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kalambo, nawaahidi sitawaangusha na kauli mbiu yetu ya kwamba: "Nuru Mpya ya Kalambo, kwa Pamoja Tunaweza," na naamini tutaitekeleza.

Bila kupoteza muda, naomba nianze kwa kuiunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa sababu nina uhakika bajeti iliyoandaliwa imeandaliwa kwa umakini sana na inajibu kilio cha muda mrefu kuhusiana na ukosefu wa ajira na hasa kwa vijana walio wengi. Safari hii bajeti hii imewakumbuka. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yote, maana imeandaliwa kwa umakini mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naomba nijielekeze katika kuchangia kuhusiana na suala la bei ya mafuta. Naipongeza sana bajeti hii kwa sababu imelenga katika kutoa majibu kwa wananchi kuhusiana na ukali wa maisha ambao umekuwa ukisababishwa na kupanda kwa mafuta kila siku. Lakini pia niiombe Serikali baada ya kupunguza tozo hizi, iendane sambamba na kutoa majibu. Kwa sababu tunavyojua ingekuwa tunaambiwa kwamba Serikali imeongeza kodi, basi siku inayofuata tayari bei za mafuta zingepanda wakisema kwamba ili waje kuagiza mafuta mengine. Tafsiri hii iende, hali kadhalika pale ambapo tozo zinapungua, basi na wao washushe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusiana na matumizi ya mafuta, naomba niishauri Serikali ijitahidi kupunguza matumizi ya mafuta kwa maana ya kwamba tutafute *substitute*. Ni vizuri tukajielekeza katika matumizi ya gesi katika vyombo vya usafiri, wenzetu wanafanya hivyo. Ukienda Malyasia gari moja inakuwa ina sehemu ya kuweka *diesel* au *petrol*, lakini wakati huo huo kuna mtungi wa gesi ambao hata katika uendeshaji wake ni rahisi sana na katika *environment* ile ni rahisi na haina taabu, lakini matumizi yake kwa maana ya kuchafua hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa umeme, ni tatizo la muda mrefu sana. Lakini naomba niipongeze Serikali kwa kuliona hili na kwamba sasa hivi tunataka kwa mujibu wa Mpango uliopo, suala la upungu wa umeme ibaki ni historia. Naipongeza sana Serikali kwa kuliona hili kwa sababu bila umeme hatuwezi kuendelea. Tutakuwa tunajidanganya tukidhani tutaendelea bila kutumia nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naiomba Serikali kwa zile sehemu ambazo tayari zimeunganishwa na gridi ya Taifa, watoke huko waanze kufikiria sehemu nyingine ambazo bado hazijaunganishwa na gridi ya Taifa. Pia katika mpango uliopo, tuwe na utaratibu wa kuji-*stretch*, tusije tukadhani katika miradi iliyobuniwa ndiyo ya mwisho. Iko miradi mingi ambayo inaweza ikapatikana kwa bei nafuu, tusije tukang'ang'ania ile tu ambayo iko kwenye mipango. Kwa mfano, namwomba Waziri mwenye dhamana ajaribu kupita Tanzania hii kubwa, aende mpaka Kalambo aone ni namna gani tunaweza tukapata vyanzo ambavyo ni rahisi zaidi kuliko hata hivyo vingine ambavyo anavitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Serikali katika kuhakikisha kwamba wanaongeza chakula kupitia *NFRA*, kwa upande wangu ambaye natokea Mkoa wa Rukwa, nisipoongelea kilimo, nitakuwa kama vile sikuingia Bungeni. Kwa bahati nzuri sisi tumekwenda *step* mbele kabla ya Serikali, wao wanafikiria suala la kuanzisha kilimo cha umwagiliaji, lakini sisi tuna *step* nyingine, tunalima kuanzia mwezi wa tisa kukiwa kukavu kabisa, na hilo somo sijui wananchi wamepata wapi! Baada ya muda unyevu unapanda. Kwa hiyo, mwezi wa Kumi tunapanda sisi. Kwa hiyo, sasa hivi naomba Serikali ijue kwamba tuna mavuno ya aina mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* wajielekeze katika kununua kwa misimu miwili badala ya msimu mmoja uliozoeleka, pesa nyingi zitengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni aibu sana wananchi wetu wanapopeleka mazao tunaambiwa eti Serikali imeishiwa pesa. Inaishiwa pesa vipi na mipango hii inakuwa imeandaliwa, kwamba tunajua sasa hivi tunataka kununua kiasi gani cha chakula? Naiomba Serikali isirudie makosa kwamba eti tumeishiwa pesa njiani wakati mahitaji ya chakula ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia imekuwa ikijitokeza hali inafikia mahali wanasema mara mizani hakuna, siyo busara Serikali kuendelea kutoa majibu kama hayo, hayapendezi hata kidogo kwa Serikali makini inayoongozwa chini ya Chama cha Mapinduzi, haipendezi kutoa majibu ya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naiombe Serikali, kwa sababu lengo ni kumpunguzia adha mwananchi, wasogeze vituo vya kununulia mazao na watoe bei yenye tija. Kwetu sisi dhahabu tunayo, tumeweka *spare*, lakini sasa hivi kwa sababu dhahabu iliyopo, mahindi hayo, tunaomba mtuongezee bei ili kilimo kiwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu unaweza *investment* sehemu ambayo una hakika ya *return* ni vizuri katika Mpango huu mkajielekeza katika kuhakikisha kwamba tunapata matrekta ya kutosha kwa sababu *power tiller* kwetu sisi zime-*prove failure*, hazifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mpango wake wa kuongeza ajira kwa kupitia *SAGCOT*. Ni wazo jema sana na tunalisubiri kwa hamu sana. Serikali itenge pesa ya kutosha kuhakikisha kwamba isije ikawa kama hadithi, tufanye kweli. Ile habari ya hadithi ilishapitwa na wakati sisi tunataka tufanye kweli. Bahati nzuri wakati

mwingine nimekuwa nikishangaa hata pale ambapo wanasema chakula kisiende nje ya nchi kama Kenya, na sisi tunataka tuwe na soko la uhakika maana kila muda tunakuja kulalamikia Serikali imeshindwa kununua. Waacheni Wakenya watutegemee, sisi tunao uwezo mkubwa wa kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itafute utaratibu ilimradi tuwe na uhakika wa ku-*monitor* kipi kinatoka kituletee *forex*. Tungekuwa tunapata *forex* ya kutosha, leo tusingekuwa tunalalamikia juu ya ushukaji wa shilingi yetu.

Kushuka kwa shilingi yetu kumesababishwa na ile *scarcity* ambayo inakuwepo na *speculators* wanadhani kwamba unaweza uka-*trade* kwa shilingi tu. Kwa sababu sera iliyopo unafika hotelini unakuta kwamba mtu ame-*pledge* kwa dola, nadhani Waziri mwenye dhamana atatoa kauli kuhusiana na huu mtindo uliozuka wa kwenda unakuta *quotation* kwenye mahoteli kwenye dola na unaambiwa kwamba bei zinaweza zikabadilika hata baada ya nusu saa, wanakuwa wanafanya kazi ya kuulizia Benki Kuu wamefanya shilingi ngapi na wao wanapandisha bei *as if* ukienda Kariakoo baada ya nusu saa utakuta bei za vyakula zimepanda. Naomba Waziri mwenye dhamana atolee kauli kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango kuhusiana na ardhi, ni kwamba sisi Wakulima, ardhi ndiyo mtaji wetu na asikudangaye mtu haijawahi kutokea mtu akaendelea kama hajawekeza kwenye ardhi, na hii ipo tangu uumbwaji wa dunia. Vizuri vyote vinapatikana kwenye ardhi. Tunaomba Serikali iharakishe kuhakikisha kwamba ardhi inapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati Naibu Waziri anajibu swali alisema wapima ardhi walikwenda wakaishia Wilaya ya Mbozi, hasa wakishafika Mbozi kufika Rukwa *hardly is one hour or two hours* umeshafika. Mpango huo uende kwa Tanzania nzima na ili tuweze kumilikishwa kwa kupata hati tusitumie katika kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati napitia mpango wa Waziri Mkuu, taarifa yake inaonesha kwamba katika Mikoa iliyokopa na kurejesha vizuri sisi Mkoa wa Rukwa ni wa tatu unaongoza Lindi ikafuata Manyara. Sisi Rukwa ni wa tatu. Kwa hiyo, tunaomba mtufikirie, mtuwezeshe kwa sababu sisi ni walipaji wazuri, tunaogopa cha mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda haujaniishia, nadhani siyo busara kama sijaongelea Mikoa ya pembezoni. Mikoa ya pembezoni tuna shida kweli! Mikoa ya Kigoma Rukwa, Katavi, kila adha ambayo anai-*face* Mtumishi ni Mikoa ya pembezoni. Maana ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba ukitafuta walimu, ukipangiwa walimu themanini wakaripoti, watakwenda kuripoti 20 na wengine wataishi miaka miwili wamejitahidi kweli baada ya muda ni lazima wakwambie kwamba ana matatizo ya kiafya anaomba awe karibu na hospitali. Ataomba apelekwe Mbeya au arudi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika nakwenda mpaka upande wa afya, hali ni mbaya kweli. maji ndiyo sisemi. Kwa bahati mbaya sana katika Halmashauri ninayotoka mimi hata ule mradi wa maji kupitia *World Bank* hakuna hata kisima kimoja ninavyoongea leo ambacho kimepatikana. Leo hii unaambiwa imeongezwa *almost* bilioni 300 kwenye Wizara ya Maji, lakini tunanufaika nini kama hata kile kilichotengwa mwanzo hatukupata hata kimoja? Ukiulizia unaambiwa kwamba ni pamoja na matatizo ya kutokuwepo Wahandisi. Sasa anapokosekana Mhandisi, mimi mwananchi shida yangu ni nini? Dhambi yangu ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itizame kwa jicho la huruma. Namshukuru sana Rais wa kipindi hiki Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, maana katika uongozi wake ndiyo tumeanza kuona neema, barabara zimeanza kufunguka, kwa kiwango cha lami. Ilikuwa hadithi, lakini naamini Mungu akijalia baada ya muda siyo mrefu, hili tutakuwa tumeondokana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la uvuvi limeongelewa ili watu wengi hasa vijana waweze kujiingiza katika shughuli za uvuvi. Sisi katika upanuzi wa bandari ya Kasanga ambayo ndiyo bandari inayotegemewa sana kusafirisha simenti kupeleka Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika historia, nadhani ziwa Tanganyika ndiyo utakuta samaki anaitwa *English Fish,* humpati sehemu nyingine. Wazungu mpaka wakamwita hivyo. Natamani Bunge hili lingemwonja huyo samaki. Lakini tunamvua vipi? Hatuna dhana za kumvua huyu? Leo nashukuru Serikali wamepunguza angalau kodi kwenye nyuzi za kutengeneza *net*. Lakini *net* peke yake inatusaidia nini kama tutaendelea kukata miti ili tutengeneze maboti? Naomba Serikali itazame pia *fibre boat* pamoja na injini zile ili tuvue samaki na sasa hivi tuna ujenzi wa soko la samaki la Kimataifa, naishukuru sana MVIWATA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Waziri wa Nishati... *(Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE.JOSEPHAT S. KANDEGE:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaunga hoja mkono tangu mwanzo, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Naomba nimwite Mchungaji Israel, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo.

**MHE. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha, ya Mipango na Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Karatu kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, binafsi sina matatizo na mipango hii pamoja na Bajeti. Maana tatizo siyo ku-*address* umaskini, bali tatizo ni utekelezaji kwa jinsi gani umaskini uondokane na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya siasa safi, uongozi bora, ardhi na watu kwa Tanzania kama tangu mwanzo wa uhuru wetu ni dhana nzuri. Tanzania Mungu ametubariki na utajiri wa kila aina. Tatizo langu kwa Tanzania ni Serikali na watu wake, ni ukiri wa neno umaskini. Sisi ni maskini, sisi ni maskini! Tukianza kwa neno hili na tukaendelea nalo wakati wote, basi itakuwa ndiyo namna yetu ya kuishi na ndiyo maana maneno yanaumba na tutakuwa maskini. Naomba Serikali tukatae umaskini kwa namna zote na tukishakubali kukataa umaskini na raslimali tulizonazo katika nchi hii, hakika Tanzania ni tajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kama nilivyosema kwenye ardhi, ardhi tuliyonayo haitusaidii Watanzania kujikomboa kiuchumi kwa sababu siyo wengi wanaoweza kutumia ardhi waliyonayo kuweza kwenda kwenye vyombo vya fedha na kukopa fedha kwa sababu ardhi ile hawana miliki nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara husika, Waziri mwenye dhamana katika Mpango huu, imeoneshwa wazi na hilo litiliwe maanani ili wananchi wale wa vijijini waweze kutumia ardhi yao kukopa kwenye vyombo vya fedha na kujiendeleza katika uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tangu mwanzo tumesema ni nchi ya wakulima na wafanyakazi na ndiyo dhana iliyotembea sana na baadaye wafanyabiashara. Ukiangalia katika kilimo ambacho tunakisema wakati wote na tunakipigia debe wakati wote, tumkomboe Mtanzania, kimekuwa cha kinyonge sana. Napenda kuiangaliza Serikali, kilimo kama uti wa mgongo kama sehemu ambayo wengi wameajiriwa kwayo, tuondoke kwenye kilimo cha kutegemea hali ya hewa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Karatu, hali ya hewa ikitupiga chenga ambayo hatuna *control* nayo, basi tutapata shida ya chakula wakati wote, na Waswahili wana usemi unaosema: “Shibe mwana malevya na njaa mwana malegeza.” Haiwezekani huyu Mtanzania akafikiri juu ya maendeleo kama ana njaa. Atawaza tu ni jinsi gani apate chakula, lakini habari ya maendeleo itakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, tukiondokana na dhana ya kusubiri hali ya hewa tu tukahamisha kilimo chetu katika neema ambayo Mungu ametujalia, tunayo mabonde mengi ya umwagiliaji katika nchi hii, na katika taarifa ya Waziri naomba aongeze bonde la Eyasi linalozalisha mpunga, vitunguu, mahindi kwa awamu mbili kwa mwaka, halikuoneshwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuondoke katika dhana ya kusubiri hali ya hewa tuwekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji, na taarifa inasema tuna hekta karibu milioni 29.4 inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini tunatumia hekta 381,000 pekee. Tuongeze nguvu kule ili tuondokane na njaa Tanzania na hii inawezekana tukimaanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika vipaumbele suala la nishati ya umeme ni ya lazima, siyo jambo la starehe au jambo la kufikiri. Maendeleo ni lazima yaendane na nishati hii ya umeme.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali katika Mpango wa umeme vijijini, tutaona kwenye bajeti ya Wizara kisekta kupeleka umeme kule Mang'ola ambako kuna uzalishaji mkubwa, kupeleka umeme kule Mbulumbulu ambako tunahitaji pia kuendeleza shule za *A-level* kwani bila umeme ni matatizo. Maeneo mengine umeme umepita juu, vijiji ulikopita hakuna umeme. Kama kijiji cha Basogawishi, Ndamararie, tupeleke umeme maana umeme ni moja ya kitu ambacho kitasukuma maendeleo kwenda kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuzungumzia jambo la raslimali watu kwa maendeleo. Ni kweli tunahitaji kusukuma maendeleo ya Watanzania waachane na umaskini. Lakini jambo moja kubwa ambalo ninaliona kwa Serikali na katika Mpango huu ambao unapaswa kutiliwa maanani ni raslimali watu. Watu waelimishwe, wataalam wapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina *resources* nyingi sana na mimi ningeweza kusema tungeliweza kuangalia mapato yanayotokana na hifadhi zetu za Taifa, madini, inatosha kabisa kuondoa sehemu kubwa ya umaskini wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Karatu tuna hifadhi ya Ngorongoro na milango ya kuingia kwenda Serengeti, tuna utalii wa kitamaduni katika bonde la Eyasi, fedha zinaingia nyingi za kigeni kwa raslimali tulizonazo.

Ni kwa jinsi gani Serikali inadhibiti mapato yanayotokana na hifadhi zetu, yanayotokana na madini, yanayotokana na utalii, bado tuna tatizo kubwa. Upande wa sekta ya madini, hatuna wataalam wazawa wa kutosha ambao watashirikiana katika makampuni yaliyowekeza hapa nchini kuchimba madini na kuhakikisha kwamba uchumi unabaki hapa nchini na siyo unaondoka nje kama ambavyo inafanyika sasa kwa makampuni fulani kwa sababu hatuna wataalam. Ni kweli tangu mwanzo Baba wa Taifa alisema madini yakae mpaka wakati utakapofika, Watanzania wawe na elimu, wachimbe wenyewe kwa faida yao. Sasa tuwekeze kwa vijana wetu, waweze kuwa wataalam na washiriki katika kuchimba madini kwa faida ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie pia sekta ya afya na elimu. Katika afya, bajeti iliyowekwa kuna ongezeko la 3.3%. Tunalo tatizo kubwa kwa Wizara hii ya Afya, moja ya matatizo makubwa ni maradhi na tunahitaji kupambana na maradhi. Hatuna wataalam wa kutosha, Waganga, Wauguzi na Watendaji wote wa sekta hii ya afya hawatoshi. Serikali katika mpango wa *PPP*, naomba mpango huu uboreshwe zaidi ili kuhakikisha sekta hii ya afya inafanya kazi yake sawasawa. Zaidi sana kuanzisha Vyuo vya Taaluma hii kwa ajili ya watumishi hawa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Umepigiwa kengele ya pili.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mchungaji, naona dakika za mwisho kasi ndio ilikuwa inaongezeka zaidi lakini tunakushukuru kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, nadhani msemaji wetu wa mwisho kwa mujibu wa muda tulionao atakuwa Mheshimiwa Mussa Haji Kombo halafu baadaye nitawataja wachangiaji watakaoanza mchana.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pia nachukua nafasi hii kushukuru bajeti hii na bajeti ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda huko, naomba kidogo kukumbusha kitu cha msingi sana katika Bunge letu hili. Kwa muda mrefu Chama kilikuwa kimoja tu cha CCM lakini baada ya kutafakari na kuona watawezaje kukusanya michango ya pande zote kwa raia wake wa Tanzania, wakaamua kuunda Tume ya kupokea maoni juu ya suala hili kwa sababu watu walikuwa wakiritimba, walikuwa wameshachoka. Chama cha CCM bado kikapata asilimia 80 kibakie na asilimia 20 maskini ikapata watu wanaosema tunataka mabadiliko. Bado Chama cha CCM na Serikali yake kikaamua kuleta Mfumo huu wa Vyama Vingi kwa asilimia 20. Maana yake nini? Maana yake unaposhirikisha watu wote watatoa mawazo mazuri kwa nchi yetu. Maana yake tutaondoa majungu, tutaondoa fitina na choyo ili tujenge nchi yetu kwa nguvu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna Vyama 5, 6, 20, ndio nia ya Chama cha Mapinduzi wakati ule kufanya hivyo lakini kwa nia ya kuleta maendeleo kwa nchi yetu na makubaliano lakini ndani ya Bunge hili halionekani kama ni Bunge la watu waliokua. Tunatupiana maneno kama ni maadui wa Palestina na Israel. Tunatupiana matusi na matope mpaka nje kwa wapiga kura wetu na raia wema. Haijulikani sababu ni nini, Watanzania wana uwezo, wanajua nani anaweza kuongoza nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sababu za kutia fitina, mishahara milioni 12, mambo kama haya ni mambo ya kupaka matope Wabunge wazuri kama sisi tuliomo humu. Tujitahidi kuchukua mfumo ambao Chama cha Mapinduzi, kile ambacho mimi nilikuwa mwanachama basi tutekeleze, uwe mfumo mzuri. Napenda sana kuwaambia Wabunge wenzangu tushindane kwa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameshachangia sana kwenye vipaumbele vingi. Mimi sitaki nizungumzie sijui kilimo, uvuvi, umeme kwa sababu nina hakika wanaolengwa yamewatosha. Nataka kuzungumzia jambo moja kubwa sana ambalo inaonekana Serikali ya Muungano haifahamu. Njia moja au *source* moja ya uchumi duniani sasa ni mchezo wa mpira. Dakika 90 ya mchezo ule, watu wanaokuja kununua mchezo ule 50,000 au 100,000 wakati wa dakika 90 na kila mmoja anakaa pale amefurahi. Wachezaji wenyewe wananunuliwa *pounds* milioni nne, milioni 10, milioni

20. Sasa tunahitaji Serikali na bahati nzuri Rais wa Tanzania amejitahidi sana kujenga uwanja mzuri kama ule tulionao Dar es Salaam Uwanja wa Taifa, tunahitaji kufanya mchezo wa mpira kuwa ni mchezo wa uchumi lakini tunahitaji kuvitayarisha vipaji. Tunahitaji kufungua shule za mchezo huu. Tunaweza tukaanzisha kwa Kanda au kwa Mikoa Maalum, tukaweka shule ambazo zina wataalam ili tupate watu wenye vipaji vya kuuza nje na Timu yetu ya Taifa ikafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi kubwa sana lakini leo kwa sababu hatuna njia ya kuwafanya wale wenye vipaji wakaendelea, hivi vilabu vyetu vikubwa wananunua watu kutoka nje, huyu kanunuliwa shilingi milioni 50, huyu milioni 100, kwa sababu hatujawa tayari. Naiomba sana Serikali katika mipango yetu na bajeti yetu iangalie uchumi huu ambao hauna hasara, hauna utapeli wala haitakuwa huu mpira tulionao sasa wa kucheza kwa kisiasa. Sijui naipenda Yanga kwa vile sijui yuko Rais, sijui naipenda Simba na ndio sababu wenzetu wakafanya makampuni ya timu zao. Nalipendekeza sana suala hili, inawezekana sina utaalam mzuri wa kuliezea lakini kwa sababu ni wazo zuri naomba lichukuliwe na Serikali. Hii pia itatoa ajira kwa vijana wetu. Kijana anayecheza vizuri pato lake halitapungua shilingi milioni kwenda juu, nafikiri hiyo itasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni hili suala la kupunguza matumizi kwa Serikali. Awamu ya Pili iliyokuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alifanya *reform* na walikubaliana katika awamu hii kuanzia mwaka 1987 mpaka mwaka 1988 kuchukua hatua ya kukopesha magari kwa Makatibu Wakuu na Wakuu wa Idara. Hii imeendelea na ina faida zake. Faida mojawapo hawa wakubwa ni uteuzi, Rais kafurahi au Rais kaona unafaa anakuteua, unakaa miaka miwili, mitatu umeshazoea starehe ya nchi, unaondoka pale hata baiskeli huna kwa sababu ulikuwa na gari tano zote za Serikali, bahati nzuri Mawaziri nao ni Wabunge wanapata hii mikopo tunayokopeshwa sisi lakini nao wanaweza kuondoka hivyo hivyo. Faida moja ni kwamba unapoondoka kwenye nafasi ile unapata nafasi ya kuondoka na gari lako ulilokopa, bado ukienda nyumbani utaheshimika. Utakaa muda mrefu watu hawajajua kama umefukuzwa. Faida nyingine ni kupunguza matumizi ya magari na matumizi ya gari ni mafuta. Suala hili lilikuwa limeondolewa, tuelezwe ni sababu gani zilifanya hatukufanya hivyo, ni utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni Bima ya Afya. Bima ya Afya iko kwa Wafanyakazi tu lakini wazalishaji wa nchi hii ni wakulima, ni wavuvi na wafugaji. Ni vizuri Serikali ikatafuta njia ikaanzisha bima ya afya kwa wananchi hawa itapunguza vifo vya wazazi, vifo vya watoto ambavyo vinaweza vikazuilika. Kwa utaratibu huu wa kumpeleka mtoto Muhimbili, analipa shilingi laki mbili, tutazika kila siku na maneno haya sijui amekufa, wanapungua uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu dakika zimebakia ndogo sana, lengo la zamani kabisa baada ya uhuru wa nchi hii, sisi kule kwetu Zanzibar kulikuwa hakuna habari hiyo, wanasema kuondoa umaskini, maradhi na ujinga. Awamu ile imekwisha, ya Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, ilikuwa Awamu wanasema ya 'Ruksa'. Imekuja Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne, inatuletea *program* hii ya Miaka Mitano tuna-*discuss* leo. Nachowaomba kwanza tufanye tathmini, Awamu ya Nne, haidhuru Rais

amezungumza matatizo, utekelezaji wa Awamu nyingine lakini tutathmini ujinga umepungua kiasi gani tangu Awamu ya Kwanza mpaka leo, maradhi yamepungua kwa kiasi gani tangu Awamu ya Kwanza mpaka leo na umaskini umepungua kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana ilikuwa ni Siku ya Watoto Duniani. Nini *cause* watoto wale wanaishi maisha ya taabu, ni umaskini, akina mama wale si kama hawataki kulea watoto wao, hawana *means*, utamaduni na nia njema haipo. Sasa tutazame kiwango gani cha umaskini, haidhuru kuna *data* tunasema umepungua lakini tutazame kama Mussa Haji na wenzake umaskini wao umepungua vipi. Naomba sana, tukilitazama hilo tutaliona vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabla kengele ya mwisho haijalia, zile shilingi milioni 12 ambazo tuliahidiwa kama zitakuweko kwenye mshahara na bahati hazipo na matusi mengi tuliyopata, aibu nyingi kwa wananchi wetu, basi naomba zirudishwe, tupate sasa hivi. Tutajifutia angalau kuona kwamba kile kitu baada ya matusi imekuwa dua, tumepewa na ndio sababu ya kuwa na ushirikiano wa Vyama Vingi, sasa *policy* ya Vyama vingine labda ikianza hivi itakuja hiki. Nakuomba hizi shilingi milioni 12 basi turejeshewe badala ya shilingi milioni mbili tunazopata sasa kabla ya kodi zikija hizi shilingi milioni 12, wananchi wetu wanaotupigia kura, vyama vyetu vitafurahi sana, vitaona hii Serikali nzuri kwelikweli. Nakuomba hilo, ahsante. Nitaunga mkono hoja hii nikipewa majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kombo amenikumbusha msemo wa Kiswahili usemao wakati mwingine wazee ni dawa, naomba niishie hapo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe matangazo na Miongozo ifuatayo:-

Kwanza kabisa, labda ningewataja wachangiaji 10 ambao wataanza kipindi cha mchana. Tutaanza na Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Yusuph Nassir, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Christowaja Mtinda na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. Hiyo itakuwa ni orodha yangu ya wachangiaji 10 wa mwanzo tutakapoingia kwenye mchezo wa jioni.

Baada ya hapo, nimepokea tangazo kwamba wale Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, walioambiwa kutakuwa na kikao chao leo chumba namba 106, saa saba mchana, kikao kile kimeahirishwa lakini watapewa taarifa kitafanyika saa ngapi, lini na wapi. Kwa hiyo, utatumika utaratibu mwingine wa kuwatangazia kikao hicho kitafanyika saa ngapi, lini na wapi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nirudi kwenye Kanuni, inaonekana hapa ndani sasa kumekuwa na mitazamo ya aina tofauti lakini mtazamo mkubwa kwa Wabunge wengi ni uvunjaji wa Kanuni ya 64 na vile vipengele vyake vyote. Kanuni ya 64 inagusa masuala yote ambayo ni makatazo kwetu Wabunge tunapokuwa ndani na tunapochangia hoja

mbalimbali. Imeorodheshwa pale kutoa taarifa ambazo hazina ukweli, kuzungumza jambo ambalo haliko kwenye mjadala, kuzungumza jambo lolote linalosubiri maamuzi, kutotaja jina la Rais, kutozungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia na mambo ya utoaji wa haki isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahsusi katika jambo ama shughuli mahususi, hatasema vibaya wala kutumia matusi, hatatumia lugha ya kuudhi ama inayodhalilisha Bunge. Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli nakemea tabia hii kwa Wabunge wote ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe sana, tutakaporudi katika kipindi cha jioni, hakika sitafumba macho na wala sitasubiri Mwongozo wala Taarifa kwa Mbunge mwingine. Hebu turudishe heshima ya Bunge, toa hoja za kimsingi, Watanzania wanatusikia badala yake tunatumia muda mrefu. Nilikuwa nahesabu kutoka juzi katika kipindi kimoja tunapoteza takribani dakika 45 kwa Miongozo na kubishana, dakika ambazo zingeweza kutumiwa na Wabunge wasiopungua wanne kuwasilisha maoni ya Watanzania hapa ndani. Kwa hiyo, naomba kabisa Waheshimiwa Wabunge hebu tuheshimu Kanuni hiyo na tujielekeze katika wajibu wetu wa Kikatiba wa kuwawakilisha wananchi hapa ndani na siyo kupoteza muda kwa sababu ambazo hazina msingi.

Hapa nimeulizwa kwa nini nimekuwa na tabia ya kuwakatisha Wabunge wanapoongea. Kanuni ya 67 inasema:-

*"Spika anaweza kulihutubia Bunge wakati wowote na kwa ajili hiyo, anaweza kumkatiza Mbunge yeyote anayezungumza."*

Kwa hiyo, ninapoona mwenendo wa Kanuni humu ndani haujakaa vizuri, Kanuni inaniruhusu kusimama wakati wowote na kumkatiza Mbunge yeyote anapozungumza. *(Makofi)*

Kwa lililojiri leo, nitatumia Kanuni ya 68(4) ambayo inasema:-

*"Spika anaweza, ama papo hapo kutoa uamuzi wake juu ya jambo la utaratibu lililotajwa au kuahirisha uamuzi ili alifikirie zaidi jambo hilo na kutoa uamuzi baadaye au kutoa uamuzi na baadaye kutoa sababu za uamuzi huo, vyovyote atakavyoamua."*

Kwa hiyo, kutokana na jambo la utaratibu lililoombwa na mimi naamua kwamba suala hili nitaendelea kulifikiria, tunaposema Spika, ni Mwenyekiti wa Bunge, Naibu Spika, ama Kiongozi yeyote anayekaa hapa kwenye Kiti, ndio maamuzi yangu.

Baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge, tutakutana saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, habari za jioni.

**WABUNGE FULANI:** Nzuri.

**MWENYEKITI:** Sasa tunaendelea na ajenda ya jioni ya leo. Kama nilivyokuwa nimeitanguliza orodha yangu pale mchana nilisema tutaanza na Mheshimiwa Tundu Lissu, atafuatia Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye mjadala huu wa bajeti ya nchi yetu kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mwanahistoria wa Kimarekani alifariki mwaka jana, anaitwa Howard Zin, aliyeandika kitabu kinaitwa *'A people's History of the United States'*, aliwahi kusema maneno yafuatayo:-

*"Those who do not learn from their history are destined to repeat past mistakes"*, wale wasiojifunza kutokana na historia yao ni lazima watarudia makosa ya zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti ambayo imesomwa mbele ya Bungeni hili Tukufu inaonesha kwamba sisi kama Taifa pamoja na Serikali yetu hatujajifunza hata kidogo kutokana na historia yetu ya miaka hamsini mwaka huu kama nchi huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka hamsini ya uhuru wetu, kila mwaka kuanzia mwaka 1961 tumekuwa tunapanga bajeti na katika miaka yote hiyo, ni miaka miwili tu ambayo Taifa hili liliwahi kuandaa bajeti iliyokuwa na bajeti ya maendeleo kubwa kuliko bajeti ya matumizi ya kawaida. Miaka miwili hiyo, ni mwaka 1964/1965 ambapo bajeti yetu ya maendeleo ilikuwa ni asilimia sitini na nne ya bajeti ya Taifa na mwaka 1981/1982 ambapo bajeti yetu ya maendeleo ilikuwa ni asilimia sitini na moja ya bajeti yote. Miaka mingine yote hii, Taifa limeandaa bajeti za matumizi ya Serikali ya kuendesha shughuli za utawala badala ya kutenga mafungu makubwa ya maendeleo. Sasa hii ni moja ya sababu muhimu ambazo zimefanya safari yetu ya kupata maendeleo kuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1969, wakati Kitabu cha yule ambaye namdhania mimi ni Msomi Maarufu, Msomi Bora kuliko mwingine yeyote aliyewahi kuzalishwa na nchi, Marehemu Profesa Justin Rweyemamu, alipochapisha kitabu chake juu ya utaratibu wa ujenzi wa uchumi wa viwanda wa Tanzania, alisema kwamba moja ya sababu kubwa zilizosababisha mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano ushindikane ni kwa sababu ya Serikali kutenga mafungu madogo kwa ajili ya miradi ya maendeleo badala ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti ya mwaka huu ya shilingi trilioni 13 na bilioni 525 na ushee imetenga kwa matumizi ya maendeleo shilingi trilioni 4.9, shilingi trilioni 8.6 zilizobaki ni bajeti ya matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, tunaendelea na utamaduni huohuo wa kula tunachokivuna leo badala ya kuweka mbegu kwa ajili ya

kesho na kesho kutwa na hii si kujifunza kutokana na historia yetu ya miaka hamsini kama Taifa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ninalotaka kuonesha kwamba hatujajifunza kutokana na historia yetu kama nchi huru, ni eneo la misamaha ya kodi. Katika Mpango wa Maendeleo tuliosomewa hapa wiki iliyopita na katika Kitabu cha Hali ya Uchumi ambacho tumeletewa hapa Bungeni, inaonesha kwamba sekta ya madini kwa mwaka 2010 ilichangia zaidi ya asilimia 36 ya mauzo yote ya fedha za kigeni kwa nchi hii, ilichangia asilimia 97 ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia, bidhaa zisizo za kilimo, sekta ni moja ya sekta ambazo zimekuwa kwa kasi kubwa sana katika kipindi cha karibu miaka kumi na tano iliyopita. Sekta hiyo ya madini ambayo ndiyo inasemekana inaingiza fedha za kigeni kuliko nyingine yoyote, mchango wake kwa pato la Taifa ni asilimia tatu. Mchango wake kwa mapato ya Serikali kama kodi, mirabaha na vinginevyo, haujawahi kufikia dola milioni 30 kwa mwaka, mchango wa sekta unaoongoza kwa mauzo kuliko sekta nyingine yoyote inaingiza fedha kidogo zaidi Serikalini kuliko mauzo ya maua, sasa badala ya kujifunza na historia hii ya hovyo, yote haya yanatokea kwa sababu ya misamaha ya kodi ambayo tuliiwekea makampuni ya madini mwaka 1997 na mwaka 1998.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya mabadiliko makubwa katika mfumo wa kisheria wa fedha unaohusu makampuni ya madini maana yake ni kwamba mabilioni yote yanayotokana na madini sio ya Tanzania, tunachoambiwa inaingiza kwenye nchi, hizi fedha hizi si za nchi hii, sasa badala ya kujifunza kutokana na makosa hayo, badala ya kujifunza kutokana na historia yetu tunaiendeleza na tunaiendelezaje? Tumeletewa Muswada wa Sheria ya Fedha ambao unapendekeza misamaha mikubwa ya kodi kwa makampuni yatakayowekeza katika maeneo maalum ya kiuchumi. Kodi zilezile ambazo tulizisamehe kwa makampuni ya madini, leo tunazisamehe kwa makampuni yatakayowekeza kwenye *Special Economic Zones* na misamaha ya kodi hii inapendekezwa kwenye bajeti hii na kwenye Muswada huu wa Sheria ya Fedha kwa miaka kumi. Kwa hiyo, kwa miaka kumi iwapo bajeti hii itapita na Muswada huu utapitishwa, kwa miaka kumi, tusahau kupata mapato yoyote ya maana kutokana na hizi *Special Economic Zones, we have not learned from our history, we are repeating past mistakes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kilimo na maeneo ya vijijini Tanzania. Sekta ya kilimo kufuatana na nyaraka ambazo zimeletwa katika Bunge hili inaajiri asilimia 75 ya Watanzania, lakini uchangiaji wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka. Mwaka huu kufuatana na nyaraka hizi, tunaambiwa kwamba mchango wa sekta ya kilimo umepungua hadi kufikia asilimia 25.3 kwa sekta inayoajiri asilimia 75 ya Watanzania, mchango wake kwa pato la Taifa ni asilimia 25.3 ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu tumeacha kuwekeza katika vijiji vyetu, tumeacha kuwekeza katika kilimo. Serikali hii imekuwa inatenga fedha nyingi kwa ajili ya kupeleka vijijini, fedha hizi zimekuwa hazifiki vijijini, naomba nitoe takwimu chache zinazothibitisha hili na hii naisoma kutoka ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, shilingi bilioni 99 na milioni 114 zilizoidhinishwa kwa ajili ya Halmashauri za Mitaa 111 kwa mwaka huo wa fedha 2008 hazikupelekwa vijijini. Kwa mwaka 2009 zilikuwa shilingi bilioni 88 na milioni 720 na hizo zilitakiwa zipelekwe kwenye Halmashauri 133 za nchi yetu. Sasa kwa takwimu hizo, kwa miaka miwili shilingi bilioni 187 na milioni 834 na ushee ambazo zilitakiwa zipelekwe vijijini zikasaidie miradi ya maendeleo hazikupelekwa. Hizi ni fedha ambazo ziliidhinishwa na Bunge hili badala ya kupeleka fedha ambazo zimeidhinishwa na Bunge, Serikali yetu imeruhusu Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tarafa na Watendaji wa Kata kuchangisha wananchi wetu michango ya nguvu, michango ya mazao, michango ya mifugo, michango ya nyumba za bati na michango hii haijawahi kutungiwa sheria yoyote nchi hii, michango haramu, wananchi wanachangishwa kwa nguvu, wanafungwa, wanapigwa si kwa sababu hakuna hela ni kwa sababu fedha ambazo zimetengwa na Serikali kwa ajili yao zimekwenda kwenye mambo mengine ambayo hayakuidhinishwa na Bunge hili. Hii ndiyo sababu ya umaskini wa vijijini, Mungu hakusema wanavijiji wetu wawe maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpango wa bajeti hii unazungumzia suala la utawala bora na kwenye Ripoti ya Hali ya Uchumi imezungumzia vilevile haja ya kuwa na utawala bora, haki za binaadamu na vitu kama hivi. Nchi hii haina utawala bora, uwajibikaji, haitii haki za binadamu. Inakuwaje Watanzania wamekufa Mbagala, Gongo la Mboto mpaka leo hatujaambiwa kwa nini Watanzania wamekufa kwenye maeneo hayo. Nchi hii Mawaziri wamepatikana na wizi wa mabilioni ya fedha za Benki Kuu, mpaka leo hatujaambiwa hawa waliohusika na wizi mkubwa huu wamefanywa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii kwa Ripoti ya Haki za Binadamu ya Tanzania ya mwaka jana, nchi hii kwa Ripoti ya Haki za Binadamu ya *State Department* ya Marekani, Jeshi la Polisi limehusika na mauaji ya Watanzania 72 katika miaka miwili iliyopita, hakuna hatua hata moja iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna yeyote ambaye amehojiwa, hakuna *inquest* yoyote kinyume na sheria zetu, hakuna mtu yeyote …

**TAARIFA**

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI**: Taarifa utaitoa baadaye, naomba umwache, Mheshimiwa endelea.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, hakuna haki za binadamu na kwa sababu hakuna haki za binadamu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili, tunaendelea na mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Juma Njwayo atafuatia na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu kutoa mchango kwenye mapendekezo ya bajeti yaliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuipongeza Serikali na hasa Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake ya bajeti, lakini pia kujali vipaumbele kadhaa vilivyo muhimu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wanaobedha, Mheshimiwa Mkulo ni vitu vya kawaida hivyo, ukishakuwa Kiongozi usitegemee *positivity* na *negativity* utarajie pia na kwa sababu ni ushauri, ule wa manufaa tuuchukue, ndiyo namna inavyoendeshwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii kwangu mimi ni nzuri, lakini tuna tatizo la nchi yetu la utendaji, tuliowapa nafasi ya kutekeleza mipango, sera, kufuatilia bajeti na sheria zote, mara nyingi hawafanyi kama tunavyowaagiza kufanya. Kwa hiyo, naishauri Serikali sasa iamue kwa makusudi kabisa kuwabana Watendaji wetu na ikiwezekana wale wanaopewa nafasi za Ukurugenzi na Ukuu wa Idara tu-*revisit* namna tunavyowapata kwa sababu wakati mwingine tunachukuachukua watu wa hovyohovyo tu, athari yake ni kutotenda yale tunayowaagiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili nina mifano mingi. Kwa haraka haraka nitataja mifano mitatu tu hapa. Mwezi wa nne wakati Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma ilipokuwa inatoa ushauri wake kwa Serikali kwamba tumegundua *PSRC* katika uwekezaji ule wa kuuza mali za Serikali kulikuwa na upungufu fulani *CHC* ipewe nafasi iendelee, jambo hili hadi leo halijafanyika, *CHC* inamaliza muda wake tarehe 30 Juni, 2011, wiki mbili tu zijazo, sina hakika kama linaweza kufanywa haraka likaletwa hapa, inaonekana kama kuna *personal interest* badala ya *public interest*. Ndugu zangu tu-*concentrate* kwenye masuala ya *public interest* kwa ajili ya maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninao mfano mwingine hapa, mwaka 2006 wakati tunapitisha *Finance Act*, Na.6 kama sikosei na labda kwa ajili ya kurejea vizuri, tulipitisha hapa, tukabadilisha sehemu fulani ya namna ya kugawa hela ya *export levy* zinazotokana na korosho, Waziri alipewa mamlaka, Hazina wapeleke kwenye Halmashauri zetu za Wilaya, hadi hapa ninavyoongea Halmashauri hizo hazijapata pesa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena anatokea mtu tu huko anaitwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, anaandika barua kwa Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho, anasema nakupa wewe hiyo pesa, jambo tulilokubaliana hapa Bungeni yeye ana *mandate* gani ya

kutoa uamuzi tofauti na ule wa Bunge? Serikali wala haijaja kutuuliza hapa, kwamba kuna mawazo mengine tunadhani na hasa wadau tunaotokana na maeneo ya korosho yale, lakini leo imesababisha *audit query* nyingi sana kwenye Halmashauri zetu. Baadhi ya Halmashauri zimepata Hati Chafu kutokana na hili, lakini pia imeleta mzunguko mrefu, unatoa pesa unapeleka kilimo, unapeleka Bodi ya Korosho baadaye Bodi ya Korosho inafanyafanya ujanja wa kununua hizo pembejeo inapeleka kule, kwa nini kunakuwa na *redtape procedure* ya namna hii? Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kugawa pesa kule, sheria ilisema mkishakusanya mnapeleka kule, hakuna la kusema kupitia kwenye Bodi ya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuliweka sawasawa hapa, naomba noisome, *Finance Act*, Na. 4 ya mwaka 2006, *section four*, ili kupunguza maneno nitasoma sehemu chache tu, inasema:-

*"The rate of ten percent collected under subsection (1) shall be divided as follows: 6.5% shall be divided amongst District Councils which are cashnut producers and 3.5% shall be limited to the Consolidated Fund."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya Katibu Mkuu kuzichukua pesa hizo akazipeleka kule, tukasababisha matatizo, tena leo hakuna pembejeo tunapigiwa kelele kweli. Wabunge wa maeneo ya korosho tunapigiwa simu hakuna pembejeo, hakuna nini, tumalize jambo hili. Ndugu yangu Mheshimiwa Mkulo, wewe kaka yangu maana umezaliwa *zone* ileile ya kwetu tunakolima korosho hebu maliza suala hili. Kwa kweli nisipopata majibu ya kutosha, tutatofautiana sana ingawaje natoka kwenye Serikali huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mawazo katika hili, watu wanajaribu kujenga hoja ya kutafuta ulaji tu, wanasema eti *Finance Act, 2010* ilizuia jambo hilo lisiende kwenye Halmashauri. Ni kweli kwa kiasi fulani na labda niisome kwa nia nzuri ya kuliweka jambo hili sawasawa. *Section four* hiyohiyo, *subsection three* ya *Finance Act* inasema, mkishakusanya korosho zile, *Minister responsible* na mambo ya korosho *in consultation with stakeholders make regulations describe a mechanism for distribution and use of levy collected in terms in subparagraph (a) amongst cash nut stakeholders*. Sasa jambo hili halijawa tayari *established* kwani kuna *Cash Nut Industry Development Trust Fund* ambayo tayari inafanya kazi hapa nchini? Kwa hiyo, wakati huu kwenye mchakato wa kujenga hili, tuendelee kupeleka kwenye Halmashauri mpaka itakapoanza kufanya kazi, tusianze kutafuta mchawi, tunakosea wenyewe hapa, tumalize jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kutoa tu baadhi ya mifano ya yanayotokea kwenye maeneo yetu ya utendaji lakini wanafanya hivyo kinyume. Kwa sababu nilisomasoma haya, mimi nataka kuwaambia kwanza hizo hela zinazoenda huko wala haziingizwi kwenye vitabu. Zaidi ya shilingi bilioni tatu na ushee, haziingizwi kwenye vitabu vya Bodi ya Korosho pale na ushahidi ninao hapa, naomba vijana wakuchukulie haya mambo yote ninayoyasoma, ninazo hapa *Performance and Financial Review* ya miaka mitatu kwenye Bodi ya Korosho. *Export Levy zero, zero, zero,* zinafanywaje na wakati zinakwenda kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni la umeme. Nimeona kipaumbele kimewekwa pale na kwa kweli kwa hali ya sasa umeme unatuangusha. Mimi nataka kurudi kulekule Kanda ya Kusini yaani kuanzia mwaka 2008/2009 mpaka 2010 wakati tuko kwenye kampeni tulikuwa tunawaambia wananchi kwamba umeme wa *Artumas*, wa gesi asilia, ule unatakiwa kupatikana kwa bei nafuu kuweka kwenye vijiji vyetu lakini sasa hapa *EWURA* nao wamefanyafanya ujanja wao hela tulilipa Holand kutengeneza tu mkataba pale na kusaini imechukua zaidi ya mwaka mzima watu wanasema eeh hawa hawataki hela, wameondoa kule. Matokeo yake kule Mtwara na Lindi wananchi wengi walio vijijini ambao wangepata umeme wameshindwa kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mkoa wa Mtwara na Lindi ndiyo Mikoa pekee ambayo haina mgao, ina umeme wa kutosha. Jamani katika muda mfupi ujao tumalize tatizo hili, tupeleke umeme kwa wananchi kule na mwaka 2015 siyo mbali, tusije tukarudi kule wakatusuta kwamba tuliwadanganya na Ndugu yangu Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Mwenyekiti samahani namtaja Mheshimiwa Ngeleja, rafiki yangu ugangamale na wale watu, umeme tupate kule, leo wanakushinda nini bwana, uwasukume, tumalize mambo kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 15 tu ya Watanzania ndio wanaopata umeme, kati yake asilimia 14 na 15 ya Watanzania wengi wako vijijini. Tutengeneze mazingira sasa, tukianza na kule ambako umeme upo na baadaye tukamalizia kwingine tutakapotoa umeme ule wa kutosha kuleta kwenye Gridi ya Taifa, utakuwa wa manufaa kwa Watanzania na wataendelea ku-*generate income* ya nchi hii kwa manufaa ya wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo pia, kipaumbele chetu namba nne ni kilimo, lakini tunawavunja moyo sana wakulima wale. Kwa mtindo huu hatutaweza kuwashawishi wakafanya uzalishaji wa kutosha kwenye mazao ya chakula na ya biashara. Maana kuna maamuzi tunayafanya ya makato yasiyo na msingi, kuwakopa kusiko na msingi, kuwapandishia ushuru na matozo yasiyo na msingi. Matokeo yake tunawavunja moyo, tunawa-*discourage* sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tuwawekee mazingira mazuri ya kupunguza hayo matozo, makato, michango ili wazalishe zaidi na zaidi Taifa linufaike na uzalishaji wa wakulima hao. Nalisema hili kwa sababu kule kwetu ukanda wa kwetu kule, wananchi wamewahi kukatwa hela zao za malipo ya korosho bila ridhaa yao. Kwani ukiwaita hawa ukawaelimisha, kuna tatizo gani kwenye mambo ya muhimu kwa mfano madawati si wangekubali tu lakini unawakata kinyemela, halafu hakuna hata ripoti ya kutosha namna gani mmefanya kwenye jambo hili. Mimi naomba tupate *consent*, mambo yote makubwa yanayowahusu wananchi, namna gani wanataka wawe na kwa kweli kwenye mambo muhimu watakuridhia tu, hakuna sababu ya kuwakatakata kinyemela na kuwaongezea makato makubwa yasiyo na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti pia nimeona jambo lingine la maji kama kipaumbele namba mbili. Maeneo ninayotoka mimi, maji ni tatizo hasa Tandahimba,

Newala na Mtwara Vijijini. Nimeona kwenye bajeti hapa ya maendeleo kuna karibu shilingi bilioni 21. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ilisema kwamba itafanya marekebisho ya kutosha, marekebisho makubwa kwenye miradi sita ile ya kitaifa ikiwemo na mradi wa Makonde *Water Supply Authority.* Mimi naomba tuanze sasa, kila aina ya mkakati na jitihada zifanywe kwa hela hizi tusingoje wananchi kuendelea kusononeka, haitatupendeza sana na wala haitawapendeza wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya Mikoa au Kanda kuna matatizo ya huduma ya afya, Madaktari wachache, Wauguzi wachache, vifaa vya tiba vichache ni pamoja na Kanda ya Kusini kwa maana ya Mkoa wa Mtwara, Lindi na Ruvuma, hatuna hata Hospitali ya Rufaa. Tuliambiwa hapa kwenye miaka mitatu, minne, mitano iliyopita kwamba sasa wanaenda kule kutujengea Hospitali ya Rufaa, tumejenga *fence* tu tumeiacha, hakuna kinachoendelea pale. Naomba hapa tutoke na pesa angalau za kuanza majengo. Wananchi hawawezi kuendelea kupata shida, wanakwenda Dar es Salaam mbali kutafuta huduma za kiafya wakati kule ingewezekana tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uliponitangaza kwamba nitaongea mchana huu, wazee wa Mtwara wamenipigia simu wakiniambia niiambie Serikali, hawataki wakimbizi kupelekwa kule kwenye Wilaya yoyote. Wana sababu nyingi tu, lakini moja ya sababu kubwa wanasema, walikuwa na wakimbizi wa Msumbiji, wamekaa kule na wamechangia kweli kuwaweka kwenye hali ngumu. Vidonda walivyovipata wakati ule mpaka leo hawajavimaliza. Sasa mnawaongezea mzigo tena wa vidonda, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi pamoja na mambo mengine nakubaliana nao kwa sababu, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anajibu swali hapa la Mheshimiwa Faith Mitambo, Mbunge wa Liwale, alisema kuna mpango wa kuwapa uraia wale na baadaye wawagawe, ingawa alisema baadaye linatafakariwa kidogo. Mimi nataka kusema, ukishampa mtu uraia si ana haki ya kuishi mahali popote kwani lazima aende kuishi Mtwara? Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 17(1), naomba nisome:-

*"Kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiwapa uraia tunawapelekaje…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu akubariki sana. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Njwayo. Kuna mtu aliniletea *message* hapa alikuwa ananiambia, anakuomba usimame lakini nimemwambia ulikwishasimama muda mrefu sana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji anayefuata, ni Mheshimiwa Ahmed Shabiby, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Nchambi.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mmoja wa wachangiaji.

Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake wawili, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara na Wasaidizi wake wote, kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo inatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida yangu na wananchi wa Jimbo langu, wananifahamu kwamba huwa nachangia vile vitu ambavyo najua vinawezekana. Huwa sichangii vile vitu ambavyo hata nikipiga kelele kwa sauti, nipige meza lakini haviwezekani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana pale Gairo sasa hivi kuna miradi ya maji inaendelea ya shilingi bilioni nane ambayo hawajawahi kupata toka dunia ianze. Sasa hivi wameshakuwa Wilaya ambayo itaanza hivi karibuni na ile barabara ya kwenda kule Nongwe na Iyogwe, pesa za kutosha tayari zipo. Kwa hiyo, tuchangie kwenye yale masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwa kutumia hiki Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 63(1) hapa anazungumzia kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vipuri vya zana za kilimo. Amevitaja hapa pamoja na ma-*power tiller*, vitakavyotumika kwenye kilimo cha mkataba, makundi yaliyosajiliwa na vyama vya ushirika. Hapa mimi bado sijaelewa. Kama tumeamua kuingia kwenye mpango wa Kilimo Kwanza, halafu tayari tunasamehe ongezeko ya Kodi ya Thamani kwa vikundi tu, kwa watu watakaojiunga na vikundi vya ushirika, kuna baadhi ya maeneo hakuna vikundi vya ushirika wala hakuna kilimo cha mkataba. Kwa ushauri wangu, kama imeamuliwa kuwa hivyo, isamehewe tu kwa Mtanzania yeyote ili mradi lile trekta la *power tiller* litakuwepo ndani ya nchi hii na itahudumia Watanzania lakini kusema kwamba mpaka ajiunge na vyama vya ushirika au awe na kilimo cha mkataba, unampa masharti mengine magumu. Ataingia na mtu mkataba, atasamehewa ushuru wa *spare parts* lakini huyo mtu aliyempa kilimo cha mkataba atamwambia mimi labda nitanunua haya mahindi kwa shilingi 100, atauza tu, hiki ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ukiangalia ukurasa wa 10 kwenye hotuba hii, kuimarisha hifadhi ya chakula katika Wakala wa Hifadhi ya Serikali *(NFRA)* kwa ajili ya ule wakati wa uhaba wa chakula. Hifadhi hii itatumika kutoa haya mazao kwenye masoko ili kushusha makali ya maisha, yaani maana yake kushusha bei ya vyakula. Ukiangalia mwaka huu tu, hawa wenyewe wamenunua kwa wakulima kilo shilingi 300, mwanzoni wakaanza kuyatoa yale mahindi pale Dar es Salaam kwa bei ya shilingi 380.

Watu wakalalamika yakashuka bei ikawa shilingi 350, wakalalamika ikawa shilingi 300. Nataka niseme lazima ifahamike kitu kimoja hii shilingi 300 unayemuuzia ni yule dalali au mnunuzi mkubwa ambaye na yeye akienda kuuza bado tena itakuja kwenye shilingi 400 mpaka 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, mkiamua kuuza haya mahindi basi yawe chini ya bei hii kwa sababu maana ya Serikali ni kuwasaidia watu kwenye matatizo. Kama mnaamua kupunguza bei basi iwe shilingi 200 au shilingi 150. Ukifanya hivyo kwa Dar es Salaam peke yake haya mahindi yakijaa kwenye masoko ya Tandale, Temeke, Tandika, Kawe na sehemu nyingine zote, kwa maana hiyo haya mahindi ambayo watu wameyaficha huko Mikoani *automatically* yatashuka bei kwa sababu watakuwa hawana mahali pa kuyapeleka kwa sababu wakipeleka Dar es Salaam tayari kule bei iko chini. Kwa hiyo, ule unafuu utakuwa wa karibia sehemu zote. Kwa sababu lazima tukubaliane kwamba Mkoa unaotumia vyakula kwa wingi ni Dar es Salaam, kwa hiyo, Dar es Salaam bei ikishuka na sehemu nyingine zote bei inashuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unamsubiri mtu unamuuzia shilingi 300, anashindwa kununua hayo mahindi baadaye tena anapata njaa huku kijijini unayasafirisha tena kutoka Dar es Salaam mpaka Kishapu, unaenda kuuza shilingi 50 na nauli, sasa umesaidia nini. Kwa hiyo, umetengeneza hasara zaidi ya mara tatu, mara nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kwenye masuala ya sukari, mwaka huu sukari imeleta shida sana kwenye nchi hii baada ya kufungwa hivi viwanda. Ukifuatilia utaambiwa kwamba baada ya kufungwa viwanda kuna wafanyabiashara wasiozidi wawili, watatu, wamepewa vibali vya kuleta sukari na wanapewa msamaha wa kodi lakini bado sukari imekuwa ya bei ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi najiuliza hivi hii Bodi ya Sukari ina kazi gani? Hii nchi kila siku tunaanzisha Bodi, Bodi, Bodi, halafu Bodi zenyewe hazina msaada wa aina yoyote. Hivi kweli kwa nini tusifanye kama nchi jirani, mfano Kenya, kwenye *shortage* ya sukari kama hii wao wanatangaza tu, mtu yeyote anayetaka kuleta, analeta na wao wanaweka kiwango kwamba labda kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu isizidi kiasi fulani. Mtu wa Mbeya, Songea, Rukwa na Iringa, mfanyabiashara wa kule ungempa kibali, angechukua pale Malawi karibu tu, ni kilomita 240 tu kutoka pale Kyela, angewauzia wale pale, lakini tena atoke mfanyabiashara mdogo Rukwa aende mpaka Dar es Salaam tena aisafirishe ile sukari ailete mpaka Rukwa halafu unategemea hiyo sukari itashuka bei, haiwezekani kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wa Rwanda wanachukua sukari Malawi, inapita Mbeya, inapita Iringa, inapita Morogoro lakini mpaka Rwanda bado bei rahisi. Sasa hatuelewi kuna kitu gani? Au kama inashindikana basi wapewe wenye viwanda wenyewe vibali, wanajua upungufu wa sukari ni kiasi gani, watajua walete tani ngapi, watajipangia ili ikidhi mahitaji ya sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tunazungumza sana mambo ya Kilimo Kwanza. Tunawapamba wakulima kwa kila aina ya stahili na tunabadilisha *slogan* kila siku mara kilimo ni Uti wa Mgongo, Kilimo Kwanza, itakuja nyingine tena lakini hakuna kinachotekelezeka, kwa sababu hatujamlenga mkulima wa chini, wakulima wetu hawakopesheki. Watu wengi wamezungumza suala hili lakini hawajafafanua kwa nini. Sasa hivi kuna matrekta hata ukipita hapo njiani hapo, kuna trekta zaidi ya 300 zinauzwa, njia kama unakwenda Kisasa utaziangalia hapo. Hawa Suma JKT nao wana matrekta na mafomu tumeyaona hapa mengine wameyaleta humu. Tutakopa Wabunge tu na wafanyakazi wa Serikali na matajiri wengine basi lakini mwananchi wa kawaida hawezi kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sharti la kwanza, ni lazima awe na nyumba yenye hati. Sasa mkulima wa Gairo pale, nyumba zenye hati ziko tisa tu, Gairo nzima, hakuna hata mkulima mmoja mwenye hati. Haiwezekani, mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe, ni pamoja na kummilikisha hati yake ya nyumba, ardhi pamoja na mashamba. Tumekuwa tukizungumzia hapa habari za hati za mila, hazieleweki zimefia wapi na sijui zimetoka wapi. Hawa *TIB* tunaosema kwamba watawakopesha wakulima hawawezi kutoa mkopo bila hati, haiwezekani. Cha msingi tuhakikishe kwamba wananchi wetu ni lazima wamiliki ardhi yao na ni lazima wawe na hati za nyumba zao, ndiyo tutaweza sasa hapo kuangalia mambo mengine la sivyo watakuja wawekezaji wa mashamba watamaliza yale mashamba yote, watauza mwishowe itakuja kuwa kama Zimbabwe hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema ahadi za Mheshimiwa Rais ni lazima ziheshimiwe. Kiongozi Mkuu wa nchi anapotoa ahadi, ni lazima iheshimike. Kwa mfano, pale kwangu Chakwale na Lubeho, amekuja, ameahidi kabisa kwamba jamani hapa mtapata umeme na hata kwenye hii Semina Elekezi anasema jamani nimeenda sehemu wakati anaenda Kilindi, watu wana simu hawana umeme.

Amekuja Waziri, amewaambia mtapata umeme, lakini mpaka sasa hivi nikiangalia kwenye vitabu hakuna! Sasa hii sijui, mambo mengine hata sielewi! Itabidi tumwone sasa Rais mwenyewe, tutamfuata Ikulu huko huko, tukamwambie kwamba, bwana hawa watu wana matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 mwezi wa Sita, wakati Rais alipokuwa anafanya mkutano wa hadhara pale Gairo, alimsimamisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye mkutano na akasema kwamba, achangie milioni 200 kwa ajili ya barabara ya Nongwe. Kwa sababu, bosi wake alizungumza hivyo, aliitikia haraka sana kwamba nitaleta hii milioni 200. Lakini toka mwaka 2008 mpaka leo, ile pesa haijafika. Naomba kama pale chini kuna matatizo kwa wasaidizi wake, ile barabara ya Nongwe, toka dunia hii ianze haijawahi kutengenezwa mpaka leo! Kwa hiyo, naomba ile ahadi itimizwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho, ni kuhusu habari ya uletaji mafuta kwa *Bulky Procurement.* Huu mpango unatakiwa haraka mno. Hawa watu wanaopiga vita hawaelewi maana yake, mimi ni mfanyabashara wa mafuta. Yaani makampuni ya nje

ndio yanayopiga vita, hawataki mzawa yeyote aingie kwenye biashara ya mafuta. Kwa sababu, ukijiingiza wewe na vilita vyako vichache pale, wao wako tayari kupata hasara hata 50/= ili utoke pale wabaki wao. Lakini kwa mpango huu, watakuwa wengi wanaoleta mafuta, wazawa wengi, ushindani utakuwa wa kweli, kwa hiyo na bei itakuwa nafuu. Lakini hii habari ya kwenye kodi sijui za tozo, *SUMATRA*, *EWURA*, nini, hata ipunguzwe vipi, haizidi 50/=. Hicho ni kitu cha ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi hii tena ukisema utoe kwenye mambo ya *road toll* 200/=, utoe tena kwenye *custom*, nchi tena haiendi, tusidanganyane hapa. Dawa ya kushusha mafuta ni kuagiza uagizaji wa pamoja wa mafuta. Nataka nione hayo makampuni makubwa yanagomea kuleta mafuta, yaambieni yaache. Mafuta ni *hot cake* hapa, kila mtu atataka kuleta mafuta hapa! Watu kibao wanataka kuleta mafuta, lakini kazi ya kuwabembeleza tu wakija huyu mzungu huyu, kaja sijui Mwarabu yule sijui, kaja nani. Unakuta watu walichosema ni cha kweli, mafuta yana matatizo. Kuna haja gani ya kukaa na kazi ya kubembeleza watu? Fanyeni huu mpango haraka sana au kuna mambo mambo ya ulaji ulaji hapa, ndio maana huu mpango unachelewa? Maana nchi hii nayo kwa 10% hii, ila siku hizi kidogo inapungua. Fanyeni mambo haya haraka, mtaona bei itashuka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kupoteza muda na kugongewa kengele. Naona bado dakika moja, huwa naongea lakini naangalia saa pale. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa hii na mimi niweze kuchangia. Lakini awali ya yote ikiwa ni mara yangu ya kwanza kupata muda mrefu wa kuweza kuchangia, si vibaya nikachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa imani yao waliyoamua kuwekeza kwangu kwa kipindi cha miaka mitano. Naomba kwa ruhusa yako niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Kishapu, tuko pamoja na mimi ni kijana waliyenituma ambaye nitafanya kazi ya uwakilishi, kuleta maendeleo na kutatua kero kwa kipindi cha miaka mitano na wao wakae mkao wa kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia si vibaya nikawashukuru shemeji zangu kule Kigoma, baada tu ya kutwaa Ubunge, wao waliamua kunipatia mke, waliniamini, wakaona pia dada yao naweza kumtunza Kishapu. Nashukuru sana shemeji zangu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba sasa nimshukuru sana Waziri wa Fedha na timu yake yote. Utamaduni wa kushukuru ni wa kwetu sisi Watanzania, Waafrika na wanadamu. Mwenyezi Mungu anapokupa jambo, ni wajibu kumshukuru ili siku nyingine akuongezee ziada ya kile alichokupa, ama akupe kile kile asikupunguzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri wa Fedha na timu yake yote, kwa kuwasilisha hotuba nzuri iliyojaa matumaini, lakini yenye mwelekeo wa kuleta

misingi ya maendeleo, kutatua kero na kuinua uchumi wa Taifa letu. Hongera sana Mheshimiwa Mkulo na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijikite katika kuchangia masuala hasa yanayohusu Jimbo langu. Nikianza na kilimo, naomba niungane na Wabunge wenzangu, tunapoongelea kilimo, kwa maono yangu, kama tutaongelea kilimo bila kuongelea maji, bado tunazunguka katika *round about* ambayo haitatupeleka au kutupa mwelekeo sahihi wa kuleta ule usemi wa kilimo ni kiini au ni uti wa mgongo na sasa tunasema Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kishapu ni miongoni mwa Majimbo ambayo kwa kweli yanaongoza kwa ukame. Lakini Mwenyezi Mungu, alitupa neema kubwa sana pale Mwanza ya Ziwa Victoria. Nadhani ni wakati muafaka sasa, kama tunaamua kufikiria kilimo, tufikirie kuyaleta maji yale na tuyatumie kwa ajili ya umwagiliaji kwa Jimbo langu la Kishapu na maeneo ya karibu ya ziwa lile. Lakini la pili, tunapoongelea kilimo, naomba sana tuongelee suala la kilimo tulichonacho sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee wetu Mwinyi alisema, kila zama na kitabu chake. Wakati mimi nikiwa mdogo, nakumbuka mvua zilikuwa zikianza kunyesha katika kijiji cha Mwamashere nilikozaliwa mimi, mwezi wa Tisa na zinakatika mwezi wa Tano kwenda wa Sita. Zilikuwa mvua nyingi, lakini hivi leo mvua zikinyesha mnapigiana simu na kwako kumenyesha leo?  Kwa hivyo, nakiri kabisa yale maneno aliyoyasema Mzee Mwinyi, kila zama na kitabu chake na tuangale kitabu tulichonacho sasa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati anajikita kwenye kutengeneza bajeti, kama kweli tunafikiria kilimo, tukifikirie kwa mtazamo wa aina yake. Tufikirie maji, tufikirie vitu vinavyowezesha kurahisisha kilimo, kama wachangiaji wenzangu walivyosema matrekta, mbegu bora ambazo zinakidhi maeneo yale, dawa za kutosha, mbolea na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka kwenye kilimo naomba nirejee kwenye maji. Kwanza naomba niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa jibu lake zuri lililojibiwa na Wizara ya Maji na kuwatia matumaini makubwa, ambayo ndio iliyokuwa kiu na hamu ya wananchi wa Jimbo la Kishapu, kuona iwapo iko siku wapo hai watakunywa na kuoga maji ya Ziwa Viktoria.  Sasa nawahakikishia, Serikali yao imeliona hilo na imewaahidi mwaka 2012, mradi ule utaingia katika Jimbo la Kishapu na hatimaye watakunywa na kuoga maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si vibaya kwa sababu kazi hiyo inafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, naomba niishukuru sana. Lakini nijikite pia kwenye tatizo la muda mfupi, kwa sababu lile litakuwa la muda wa kati ama muda mrefu, hivi sasa Jimbo la Kishapu, ni miongoni mwa Majimbo ambayo yanahangaika sana na suala zima la maji. Nilidhani kwa kutumia fursa ya bajeti hii tuangalie uwezekano, aidha, wa kupata visima katika vijiji vyetu ama kupata mabwawa ambayo tutaweza kuzuia maji yanayotiririka wakati wa masika na wakati wa mvua nyingi ili wananchi wa Jimbo la Kishapu, wasipate tabu wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie usemi mmoja wa Kisukuma. Wenzangu wanatumia wa Kichina, Kijerumani, Kingereza, lakini mimi naomba nitumie usemi wa Kisukuma kwa ruhusa yako. Wasukuma wana usemi wanasema, "*Omasala adawuna gwan'nigo,*" yaani mtu mwenye akili, huwa habebeshwi mzigo. Atatumia kila njia, ile akili yake atacheza na vichwa vya watu, watabeba wengine, yeye atatia mikono mfukoni atawasindikiza wakiwa wamebeba mzigo kichwani. Sisi sasa, imefika wakati Watanzania, tutumie akili zetu, tucheze na akili zetu, tuweze kuona tunayatatua vipi masuala ya muda mfupi, ya muda wa kati na ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Kishapu wana matumaini sana na Mbunge wao. Wana imani sana na Serikali yao. Lakini wapo tayari kuonesha ushirikiano, umoja, kwa lolote lile ambalo wanadhani litasaidia jamii yao. Kwa hiyo, ni wakati wetu sasa Waheshimiwa Wabunge, kupitia Bunge hili Tukufu, kuchangamsha vichwa vyetu. Tunaongelea maji tangu uhuru, Serikali imejitahidi kwa kiasi kikubwa, lakini ni wajibu wetu sasa sisi kuumiza akili zetu tuone ni namna gani mama zetu hawa, wanaota vipara, wanapata tabu, akichelewa nyumbani Mheshimiwa Mwenyekiti kama wewe, anapata bakora, ulikuwa wapi? Ni mateso ya hali ya juu kweli kweli. Nadhani ifike mahali sasa tufikiri, kwa sababu tukiongelea suala la maji sio tu lina athiri afya zetu na linatuumiza ama kutupotezea muda, lakini linasababisha mambo mengi, ndoa zinavunjika! Kwa hiyo, ni lazima tuliangalie kwa upana kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirejee kwenye suala la Hospitali ya Wilaya. Tangu mwaka 2003, nashukuru kwamba katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, suala zima la afya pia limeangaliwa kwa ukaribu zaidi. Lakini Wilaya ya Kishapu, ilianza mwaka 2003, mpaka leo hii 2011 hatuna Hospitali ya Wilaya na hatuna mgawo wa dawa kwa ajili ya Wilaya! Yaani dawa zinazokuja Jimboni na Wilaya ya Kishapu, ni mgawo wa kituo cha afya. Tunao Madaktari wanne, kwa bahati mbaya ama nzuri mmoja alifariki kwa ajali ya pikipiki, walikuwa watano, wanao uwezo kabisa wa kuwa Madaktari wa hospitali ya Wilaya, hatuna Hospitali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la kusikitisha sana na kitu ambacho kinanishangaza na kunitia machungu ni kuona, Wizara hii ya Fedha kupitia bajeti zake, bado inaruhusu fedha hizo ziende kwenye kujenga jengo kubwa na la thamani la Halmashauri! Wakati hatuna Hospitali ya Wilaya mpaka hivi leo! Nilidhani hata Mheshimiwa Mkulo, angekuwa hana afya njema, asingeweza kutengeneza bajeti hii. Kwa hiyo, suala zima la afya ni lazima tulipe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ile inahitaji bilioni 1.3 tofauti na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, alisema Wilaya inahitaji bilioni 9.0! Kwa hiyo, Hospitali yangu inahitaji bilioni 1.3 ili iweze kukamilika, akinamama kama wewe wasipate tabu. Wanatembea kilometa 150, kutoka Kata ya Mwamalasa na Gunambiu kwenda Shinyanga Mjini, bado wakifika wanaambiwa umetoka Wilaya gani? Akijibu Kishapu, anaambiwa, hii ni Hospitali ya Mkoa, subiri foleni, kama ni ya Wilaya, nyie hamna hopsitali kule? Ni mateso na ni aibu kweli kweli na tuko kwa ajili yao, lazima tulisimamie kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umeme. Tunalo tatizo kubwa la umeme, lakini ifike mahali Waheshimiwa Mawaziri kwa niaba ya Serikali, waheshimu na kutii ahadi za Viongozi Wakuu wa Nchi. Mheshimiwa Sumaye, akiwa Waziri Mkuu, alifika katika Kata ya Shagihiru, akawaambia wananchi pale, mtapata umeme hapa; nitakaporudi Dar-es-Salaam, nitaagiza mpate umeme. Lakini ametoka Mheshimiwa Sumaye, ametoka Mheshimiwa Lowassa, sasa ni Mheshimiwa Pinda, umeme ule haujafika! Sasa hawa Mawaziri kama hawaheshimu kauli za Viongozi Wakuu wa Nchi, watatuheshimu sisi Wabunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali, kauli za Viongozi Wakuu wa Nchi wanapotamka, wana mambo mengi; kuna *session* ambazo zinahitaji kufuatilia, ni lazima wao wafuatilie na kutii na kuheshimu. Unakuta hivi sasa hata Wakurugenzi wa Halmashauri, wako juu ya Wabunge, wako juu ya Wakuu wa Mikoa, wako juu ya Mawaziri, ni kutokana na utaratibu wa kutoheshimiana. Kwa hiyo, tuheshimu kauli zile, wananchi wawe na imani, wajenge imani vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutoka Kata ya Songwa Mji wa Maganzo kwenda Mondo, kwenda Bubiki, kwenda Segebugoro, kwenda Nyasamba njiapanda ya Mwanza, ni barabara ya lami. Watu walihamasishwa kujenga majumba ya kisasa, wakapata ahadi ya kuletewa umeme na Wabunge waliopita wengi, hakuna lililotekelezeka! Sisi wakati tunakaa kijijini, tukibebwa na mzee kwenye *Land Rover, Pick Up* nyuma, tukiingia karibu na Shinyanga Mjini tunapanda lami, tunaona mataa. Kwa hiyo, ni imani yangu tangu udogo, mjini ni sehemu ya kuja kujifunza. Lakini leo mtu anatoka kijijini, anafika mjini anakuta barabara ndio mbovu, mataa hakuna, umeme hakuna, watajifunza wapi? *Where are we going to learn? We don’t need to learn through mistakes, we better learn through others achievements.* Sasa wapi sisi tunakwenda kusoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye suala lingine la barabara ya lami. Tunapoongelea kukuza uchumi wa nchi yetu, yako mambo ambayo yataharakisha ukuaji wa uchumi. Tuna Meatu, tuna Ngorongoro, tuna Igunga, tuna Majimbo mengi ya Iramba kule, ambapo hayana barabara! Tunahitaji kupata barabara ya lami itakayotoka Kolandoto, iende Ngorongoro kupitia Meatu. Lakini itoke Ukenyenge itokeze Igunga, nia yetu ni nini? Watu wataweza kusafiri kwa urahisi, watu wataweza kusafirisha mtama wao, mahindi yao, mpunga wao kwa bei nafuu ili waulete mjini. Leo watu wanalima mpunga vijijini kule, mahindi, usafiri ni ghali kuliko kitu chochote! Kwa hiyo, uchumi wetu hatuwezi kuuwezesha. Naomba Mawaziri wako hapa, waweze kutuangalia katika suala la barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shinyanga Mjini leo, Mikoa ya Kanda ya Ziwa tuna dhahabu ambayo inatembea juu. Mwenyezi Mungu ametupa neema ya kuwa na dhahabu inatembea juu ya ardhi, lakini tunajikita kuchimba dhahabu iliyokuwa chini ya ardhi! Dhahabu iliyokuwa juu ya ardhi ni mifugo. Leo Kiwanda cha Nyama tangu uhuru, mpaka hivi leo nasimama, hatuna kabisa Kanda ya Ziwa. Wafugaji wana ng’ombe 1,000, wana ng’ombe 2,000, leo ng’ombe anauzwa shilingi 200,000, analetwa Dar-es-Salaam

anauzwa 700,000/=. Lakini angekuwa na kiwanda yule mtu pale, Serikali ingewezesha... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Lakini kwa sababu, mimi ni Mbunge *Form One,* ungeniongezea dakika tano, nikaweza kumalizia. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nakushukuru kwa mchango wako. Uzuri wa shughuli za Bunge, hakuna *Form One* wala *Form Six. (Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Charles Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Serikali yangu. Awali ya yote nichukue fursa hii kuwashukuru wote ambao wananiombea afya na ujasiri katika kufanya kazi hii ngumu, lakini ninayoipenda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijakwenda mbali sana ningependa niwasilishe mambo ambayo nimetumwa na wapiga kura wangu. Wananchi wa Kata ya Muhutwe, Kisiwa cha Bumbile na Kata ya Kishulo, wanaiomba Serikali katika mipango yake mizuri ya safari hii, wawajengee Vituo vya Polisi. Vilivyopo vimechakaa au ni mahanga, majumba ya mabati. Lakini kwa utaratibu tuliojipangia wako tayari kutoa vionwa, mawe na matofali, kusudi Serikali ichangie vifaa vya viwandani, twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kagera na Muleba, wamenituma nishukuru kwa mtindo huu wa Viongozi wa Kitaifa, kututembelea. Alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunashukuru sana. Akafuata Waziri katika Ofisi ya Rais, Mzee Wassira, wanashukuru sana. Wanasema wote muige mfano, karibuni Nyegera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nalizungumzia nimetumwa na Waheshimiwa Madiwani wa Wilaya ya Muleba, Waheshimiwa Madiwani kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Muleba wanaomba Waziri wa TAMISEMI na Naibu wake waende kwenye Halmashauri ya Muleba, wana neno wanataka kunena nao, wanasema kwa kikwetu ukitaka kumuokoa ndege umuokoe wakati bado anaruka "*ati ajuna akanyonyi ajuna kyakyaharara,*' TAMISEMI mnahitajiwa Muleba, kuna jambo la haraka mtaambiwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotumwa, tunajitahidi kujenga zahanati na vituo vya afya, lakini tunajua bajeti ya Serikali haitoshi lakini nia ipo na uwezo wa wananchi kuchangia kwa kasi, siyo mzuri. Wamenituma nimwombe Waziri wa Afya, niiombe Serikali katika hospitali zetu za Ndorange, Kagondo, na Rwantege,

ambazo ni za *mission* mtusaidie, mpeleke madawa kwa wingi na mchangie gharama za Madaktari ili wananchi wetu wasiendelee kufa kwa magonjwa madogo madogo ya kawaida, chonde chonde mtusaidie lakini na sisi tunakuja kwa kasi tutengeneze Vituo vya Afya vya kila Kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni nzuri sana, naanza kuiunga mkono bajeti hii ya Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha, aliyowasilisha nianzie upande wa elimu, bajeti imekuja kututoa kimasomaso sisi ambao tumekuwa tukihubiri suala la elimu tulianzisha sekondari za Kata, wakatupiga madongo, lakini nimeona bajeti kubwa iliyopangwa katika sekta ya elimu, nina uhakika miundombinu itajengwa, Walimu watapewa marupurupu mazuri, kwa hiyo, watafundisha vizuri. Nachukua fursa hii kuwaombea walimu posho wale wanaokwenda kufundisha Kagera na Mikoa mingine ya pembezoni kwa sababu mikoa ya kwetu Walimu wakipangwa hawaendi, sasa nawaombea posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ombi lingine, sisi Wilaya ya Muleba tulipangiwa walimu 56 wa sekondari walioripoti ni 40. Sasa kwa kuwa hao watu wengine kumi na sita hawajaripoti, tunaomba ile kasma iliyopangwa kuwahudumia basi mumruhusu Mwenyekiti wa Halmashauri yangu na Halmashauri itangaze kazi, wale wanaotaka kwenda kufanya Kagera, wanaokwenda kufanya Muleba waende na ningeomba mikoa mingine ya pembezoni tupewe utaratibu huo, mtu akipangiwa kwenda pembezoni Singida, aah, Singida siyo pembezoni, akitaka kwenda Lindi akakataliwa basi Mkurugenzi wa kule atangaze, anayetaka kwenda kufanya kazi kule kusudi tuweze kusukuma gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naomba ni tatizo la mawasiliano, Walimu wangu wanaopenda kufundisha visiwani, mimi ndiyo Mbunge mwenye visiwa vingi, nina visiwa tisa katika Ziwa Victoria, kuna walimu na wafanyakazi wanaokwenda kufanya kazi Kisiwa cha Goziba, Goziba hakuna mawasiliano, naomba muisaidie muweke mnara wa mawasiliano, nimewaomba *VODACOM* hawajanijibu. Naomba mniwekee mawasiliano lakini mbali na mawasiliano ule mnara utatusaidia katika kuongoza mitumbwi na majahazi yanayokwenda sehemu zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni nzuri sana, ni bajeti ya ukombozi, ukisoma vitabu hivi kuna mambo yamefichika, nilitaka kulaumu lakini Mwenyezi Mungu kanijalia nikasoma, ukisoma mpango wa umwagiliaji na sisi Kagera tumekumbukwa, nashukuru ni bajeti nzuri. Mradi wa umwagiliaji wa Muleba mwaka huu umetengewa fungu, nadhani na sisi tutatumia sehemu hiyo kama darasa kusudi mtakapokuwa mmekuja awamu yetu na sisi mtugeuze sijui itakuwa *SAGCOT*, au *NOGAT*, kwa hiyo nashukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala lingine, suala la mafuta, suala la mafuta daah! Nasita kuhusu tozo, tozo hazitatupa nafuu lakini mimi badala ya kulaumu naishauri Serikali iondoe vikwazo katika kuondoa mizigo bandarini ili nchi za jirani zipitishe mizigo yao Dar es Salaam, mizigo ile ikienda kwa wingi hata kama mtapunguza

ule ushuru mdogo acha *road levy* kwa sababu watu wanasema *road levy* iendelee na mimi naafiki, ile shilingi inayobaki kama magari yakipita kwa wingi kwenda Kongo, kwenda Burundi, *volume* ya mafuta itakayotumika ikiwa nyingi tutaweza kupata pesa nyingi sana za kuendesha shughuli zetu. Kwa upande wa mafuta nashauri hilo lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoke upande wa mafuta, niende katika suala la umeme. Waheshimiwa Wabunge nawa-*address* kupitia kwa Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu liliwahi kufanya maamuzi likaweka kitu kinaitwa *road levy,* ndiyo imejenga barabara hizo mnazoziona. Tukitaka kupata umeme huo tunaouomba hapa tutengeneze *energy fund,* tujifunge kibwebwe, tutengeneze *energy fund*, tukijua kwamba *energy fund*, tutakuwa tunaiona, tutaanza kugawana, kabajeti kenyewe mnakaona, kasungura kenyewe mnakaona, hatuwezi kutoa umeme kwa watu wote, nazungumzia ule umeme wa vijijini, kwa sababu ule umeme wa kuzalisha kwa *generator* sina wasiwasi, huo utapatikana, nimeyaona makabrasha, nimekesha nikiyasoma, tumezungumza sana, huo utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa vijijini inabidi tujifunge mikanda, Watanzania tunaweza tukakubaliana kwamba kwenye simu tutakazopiga basi kila ukipiga dakika 10 au dakika sita uchangie shilingi tatu au shilingi nne, hiyo pesa iingie kwenye *energy fund,* sisi Wabunge tuisimamie, halafu tuipeleke kwenye vijijini, tutatumia miaka mitatu lakini tutavuka. Mnajua Watanzania wenzangu hatuna mjomba, hatuna shangazi, tujifunge sisi wenyewe tuchangie *energy fund* tutaweza kutengeneza umeme bila kumlaumu yeyote. Hatuna nafasi ya kulaumu, sisi ndiyo Serikali tutamlaumu nani, kasungura kenyewe kadogo. Kwa hiyo, ndugu zangu naomba mlizingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye suala la uvuvi. Suala la uvuvi lina utata, Jimboni kwangu kuna watu wanapigwa viboko, wanaambiwa ni wavuvi haramu, nimeiona sera ya Serikali, nimeiona bajeti, nimeiona mipango naipongeza bajeti hii. Ninachoomba pamoja na kupunguza ushuru katika nyavu, ongezeni kupunguza ushuru katika *engine* lakini nyavu ambazo ni mbovu tengenezeni utaratibu wa kuzi-*withdraw* kwa kuwapa wavuvi nyavu nzuri, halafu tuwasimamie. Naomba twende kwa namna hiyo, wananchi wetu wataweza kuvua na wataweza kupata manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushe ahadi za Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais alipokuja kwetu aliahidi kutengeneza barabara ya lami kutoka Muhutwe kwenda Kamachumu, naikumbushia na nashukuru, lakini ikifika Kamachumu iende Nshamba ifike Muleba kusudi tuweze kuunganisha. Nashukuru ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Bukoba lakini Mheshimiwa Rais alisema mtakapokuwa mmemaliza Bukoba na pesa nimeziona atakwenda Kajunguti, tuna mpango wa kulima bonde la Mto Ngono kusudi tuweze kupeleka mazao Ulaya, soko letu tunalolilenga ni soko la Ulaya, kwa hiyo nashukuru sana. Lakini Mheshimiwa Rais alitamka mwenyewe na nilikuwepo, akasema atatuwezesha ili tuweze kulima mpunga katika bonde la Burigi, hiyo ni ahadi ya Rais na nitaomba na yenyewe tuitekeleze. Ni mradi mdogo haulingani na ule mkubwa sana, lakini ahadi ya baba ni ahadi, ningeomba itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapojiandaa kumalizia naomba nichukue nafasi hii kuipongeza bajeti hii na nieleze msimamo wangu kuhusu misamaha ya kodi. Wametoa tafsiri nyingi kwamba historia itawafundisha watu na kuna Mswahili alisema, usilolijua usiliseme. Nawaombea wachimbaji wa mafuta tuwape msamaha, kwa sababu gani? Uchimbaji wa mafuta nchi hii ulianza kwenye miaka ya 50, tumechoronga visima zaidi ya 39, visima hivyo vinaonekana vitupu lakini tumeanza kwenda kwenye maeneo ambayo kasi ya upatikanaji wa mafuta na gesi ni kubwa, kila kisima kilichochimbwa, visima vitatu vilivyopita vyote vinaonyesha gesi na gesi kubwa. Sasa tuna mashindano ya kieneo, *regional competition,* tunataka tuwavutie wachimbaji, kinachotakiwa katika msamaha huu ni usimamizi pale ambako misamaha ilitumika vibaya watu walifanya uzembe, ningependekeza anayefanya uzembe katika kusimamia msamaha apewe adhabu kubwa, aende jela miaka 20, lakini hao Wazungu tuwape misamaha *statutory,* ili waje wachimbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba siku moja Mheshimiwa Rais aje hapa na *brass band,* aende kwenye kiti karibu na hapo ulipokaa, atangaze kwamba nchi hii imepata mafuta, ningependa kabla sijafa niyaone mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, mwisho wa kuchangia, naunga mkono bajeti ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, sijasema kidumu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage kwa kweli leo umetuacha hoi, lakini hapa nimeambiwa kwa nini hukumalizia kusema maana ya kasungura kadogo kwa Kihaya wanasemaje, ila utatwambia baadaye. Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Amina Abdallah Amour atafuatiwa na Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyokuwepo mbele yetu. Naanza kwa kusema ukikisoma kitabu hiki cha bajeti na ukakimaliza vizuri, maelezo yaliyoko humo ndani ya hii bajeti yanatosha kujiona Watanzania tunaagana na umaskini, lakini tatizo liko kwenye utekelezaji na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kupunguza umaskini yote ilishaelezwa hiyo hapa, sina haja ya kurejea kuchangia kwa kirefu ila nitapitia baadhi ya maeneo na kutoa msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwenye ajira, Serikali imeahidi itapanua ajira kwa kila maeneo ikiwa pamoja na kilimo. Ukiangalia kilimo huwa kinafanyika vijijini siyo mjini na ukiangalia tatizo lililokuweko hivi sasa, vijana vijijini wakishabalehe tu hawataki tena kubakia vijijini na wanakuja mijini na wakifika mijini huwa hawapati kazi, wanapita wakiranda barabarani na hao vijana ndiyo hawa vijana waliotupa kura zao na hivi leo siye sote tukawa hapa ni Wabunge, chama chochote bila kupata *support* ya vijana hakiwezi kushinda. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwatupie macho hawa vijana na iweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye misamaha ya wawekezaji. Misamaha ya wawekezaji ni mingi mno, ijapokuwa Serikali imesema itapunguza lakini mimi nasema bado ifuatilie kutokana na kwamba, kuna wawekezaji wengine ambao wamekuja hapa kuwekeza kwa majengo kama hoteli ambazo ni hoteli mbili tu, lakini misamaha ya ujenzi waliyochukua ni ya hoteli mpaka kumi, wakatumia zile hoteli mbili wakajengea hoteli na vifaa vingine wakapita wakiviuza mtaani. Kwa hiyo, tunapunguza mapato yetu ya nchi, itabidi ifuatiliwe vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye sekta ya uvuvi, ni kweli uvuvi umetajwa, lakini haujapewa kipaumbele, bahari yetu ni kubwa, ina samaki wengi na samaki wakubwa. Juzi nilipita nikienda feri, kuna vijana wengi wanataka kwenda kuvua lakini hawana dhana za kuvulia, wamebakia pale wanakaa wakipara samaki, miaka nenda, miaka rudi, kazi yao kupara samaki. Kwa hiyo, naomba Serikali iwawezeshe hao vijana kwa kuwakopesha nyenzo za kuweza kuvulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitagusia kidogo kwenye bajeti tegemezi, sisi hapa Tanzania tuna bajeti tegemezi na bajeti tegemezi imetokana kwa kuwa matumizi ni makubwa mno kuliko mapato. Lakini hii tusiishabikie tukasema kwa kuwa kila nchi wana bajeti tegemezi sisi Watanzania tuvinjari, ijapokuwa baada ya miaka mitano tuhakikishe na sisi tunaondokana na bajeti tegemezi, tunakusanya mapato ya kutosha, tunayafuatilia mapato, tunayadhibiti mapato na kwa wale wote waharibifu na wezi wa nchi hii tunawafukuza sehemu walizokuwepo ukianzia *TRA*, Shirika la Meli na Halmashauri zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye mikopo na nitagusia riba ya mikopo. Riba ni kubwa mno, naiomba Serikali ikae na mabenki, izungumze nao ili waweze kupunguza hii riba na ikiwa Benki Kuu wanachukua *percentage* kubwa katika hii mikopo nayo ipunguze ili na huku hii riba iweze kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja kidogo kwenye sheria ya *PPP*. Sheria iko tayari, naomba Serikali iitangaze ili watu waanze kuifanyia kazi na naomba Serikali ifuatilie yasije yakajitokeza yale yaliyojitokeza, sina haja ya kuyataja na sote tunaijua, kwa hiyo, naomba Serikali ifuatilie vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuchangia katika mfumko wa bei. Nitakwenda moja kwa moja kwenye bidhaa hizi zinazozalishwa hapa ndani ya nchi kwani mchele na sembe umepanda bei mno, mwananchi mwenye kipato cha chini hamudu kununua mchele na sembe na hivi vitu tunavizalisha hapa hapa. Serikali imesema tayari itapunguza bei ya mafuta, lakini hata ikipunguza bei ya mafuta, lakini bei bado itakuwa kubwa, naiomba Serikali iingilie kati na ipange bei ya mazao haya ili mwananchi amudu kununua mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kukaa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Amina kwa mchango wako. Sasa nitamwita Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir na Mheshimiwa Sabreena Sungura ajiandae.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kabisa nasema naiunga mkono hoja hii ya bajeti yetu kwa nguvu zote. Vile vile nitumie fursa hii adimu kabisa kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Waziri wa Fedha; Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda, niwapongeze pia na wajumbe wao, nimpongeze Mzee Wasira, nimpongeze pia na ndugu Mpango wa Tume ya Mpango kwa kuandaa mpango huu thabiti. Baada ya hayo, niwapongeze pia wana Korogwe Mjini kwa maamuzi waliyoyafanya na hatimaye nikasimama hapa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeiona bajeti pamoja na vipaumbele vyake, ikianzia umeme, ikazungumzia maji, ikazungumzia viwanda, ikazungumzia miundombinu na hatimaye elimu na afya. Ni ukweli usiopingika kwamba bila umeme Taifa letu litaingia gizani, bila umeme hatutakuwa na maendeleo endelevu na hatimaye tutakuja kujikuta kama nchi tumeingia katika mfumo unaoitwa *stagnation flow chart* ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme kwa nchi hii limekuwa ni tatizo kwa takriban mwaka mmoja na nusu, lilianza kidogo kidogo lakini kadri nchi inavyokua na mahitaji yake na ongezeko la viwanda, tatizo hili limeendelea kuwa kubwa. Niipongeze bajeti kwa kutenga kwa makusudi kabisa kwamba sasa tunaangalia mtazamo wa kuwa na *megawatt* 260 kwa ajili ya *emergence power crisis*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na utekelezaji wa kadhia hii ya umeme, sasa Serikali imejiwekeza katika kutengeneza bajeti ya kununua mitambo itakayozalisha *megawatt* 260, lakini ni suala la kujiuliza sasa nishati itakayotumika kwenye uzalishaji wa umeme huu ni ipi? Inawezekana kabisa, kwa sababu suala hili ni la dharura, kwa sababu suala hili limekuja kwa wakati ambao tunaona mafanikio mbele, lakini tuna kadhia ya haraka, tukajikita kutumia nishati ya mafuta. Lakini ni ukweli pia usiopingika kwa maana sababu ile ile iliyotufanya tubadilishe Ubungo kutoka Jeti kwenda Gesi Asilia na kurudi tena kwenye Gesi kwa *megawatt 260* kutalitumbukiza Taifa katika mzigo mkubwa kwa maana bei ya Jeti sasa hivi imepanda na hata bei ya *fuel oil* nayo pia imepanda. Inawezekana kabisa, piga hesabu za haraka haraka kwa *megawatt* hizi 260, tutajikuta kwa bajeti yetu ya mwaka mmoja kwa ajili ya mafuta haya ya uzalishaji umeme wa dharura, tutajikuta tumetumia pesa ambazo tungeweza kuwekeza kwenye bomba la gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono bajeti lakini ni lazima tathmini ya kina ifanyike. Ni kweli tunahitaji umeme lakini tuone ni mahali gani tunaweza kutumia nguvu za haraka. Au hata kukopa mahali ili angalau lile bomba linalotoka Kusini kuja Dar es Salaam na hatimaye kuelekea Tanga liweze kutengemaa. Tufanye *costs benefit analysis* ya kwamba gharama za Jeti za mwaka mmoja zinaweza zikatosheleza kujenga lile bomba kutoka Mtwara kuelekea Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hayo, labda nijaribu kwenda kwenye suala la miundombinu. Naikumbatia sana bajeti hii na nitaiunga mkono kwa nguvu zote huku tukijielekeza na kujikita katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu imegusia bandari na reli. Kule tunakotoka sisi imepita reli, barabara na bandari haiko mbali. Lakini pia ilitoka katika sehemu ya Mpango kwamba, sasa tunazungumzia kutengeneza bandari kubwa Mbegani. Napenda niishauri Serikali na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Uchumi kuweka bandari Mbegani mahali ambapo ni kilomita 30 kutoka Bandari ya Dar es Salaam kama nina hesabu za sawasawa au kilomita 35. Meli ambazo zitakuwa zina *dock* Dar es Salaam na zile ambazo zitakuwa zina *dock* Mbegani zitakuwa zina share *outer acrage* moja. Maana *outer acrage* kwa maana zitakuwa zina-*pack* nje ya bahari karibu sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tusisahau kutoka Mbegani kuelekea Saadan ambapo ni eneo la Hifadhi ya Mbuga za Wanyama na mahali ambapo kunazaliwa *Tortoise* au Kasa, ni eneo hilo hilo la karibu. Sasa athari za kuingia kwa meli nyingi hapa zinafahamika. *Water pollution* tutaua wanyama baharini, tutaua na mali hali zilizopo ndani ya bahari zetu. Kwa nini basi tusiliangalie kwa kina na katika mfumo ule ule wa kutawanya uwekezaji wa Kitaifa badala ya kuiweka Mbegani tukaipeleka Mwambani? Siwezi kusema imetoka Mkoa gani na si kwamba hapa nita-*declare interest*, hapana! Ni suala la *logic* tu. Meli zitakazokuwa Mbegani *outer acrage* yake itakuwa ni karibu na Mbegani. Kwa hiyo, tuiombe bajeti hii angalau basi kama kutakuwa na suala la kuhamisha uwekezaji huu wa Kitaifa, tufikirie eneo lingine, si lazima iwe Mwambani, tunaweza tukasogeza hata Kilwa kule alikotoka Mheshimiwa Mangungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la elimu. Ni ukweli usiopingika matokeo ya shule zetu za Kata hayakuwa mazuri hususan mwaka huu na si ajabu hata Mwenyezi Mungu akayajaalia kidogo kidogo kwa mwakani. Lakini sasa tuseme tumewekeza bajeti hii nzuri kabisa kwa ajili ya Walimu wa Sekondari. Labda nitoe ushauri tena kwa Wizara husika pamoja na Serikali yetu kwamba, pia sasa tuongeze bajeti kidogo ambayo itahusisha shule za *VETA* kwa maana kimbilio la watoto hawa waliopata *division IV* na *zero* waweze kwenda kule angalau wakapate stadi za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika vitongoji mbalimbali vya kule nilikotoka nikianzia Mahenge, Kitifu, Ngombezi na hata nikisogea karibu kidogo maeneo ya Mzeri nikiteremka Mswaha, nikiongeza Kilole na Bagamoyo. Ukiangalia idadi ya vijana ambao wamemaliza shule za Kata na kazi wanazozifanya watu wote tunasimama stendi. Idadi ya watu wanaosafiri kwenye stendi ya Mji wa Korogwe ni takriban 5% lakini *population* iliyopo, 95% ni vijana ambao aidha, wameshindwa kuendelea baada ya kumaliza darasa la saba au wamemaliza Shule za Sekondari za Kata na wameshindwa kuendelea na masomo. Sasa tutafanya nini sisi kama Serikali au kama viongozi tunaopanga mipango ya nchi hii leo? Tuwatafutie namna bora ya kuweza kuwapa stadi za kuingia nazo mitaani. Kwa hiyo basi, naishauri Serikali tuongeze kidogo kwenye bajeti inayohusiana na Vyuo vya Ufundi Stadi, tuongeze wigo kama viko vya Kanda, sasa

tuangalie kila Mkoa na kama viko vya Mkoa kutegemea na *population* basi tuongeze hata ikiwezekana vya kila Wilaya mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la afya. Bajeti yetu imegusa na imegusa vizuri tu. Lakini pia niseme kuna baadhi ya maeneo ambayo yanakua kwa haraka sana na hasa Korogwe Mjini. Hospitali yetu ya Magunga pale ambapo inatokea dharura yoyote tunashindwa kuhudumia wagonjwa wengi. Barabara ya kutoka Chalinze mpaka ufike Mkomazi hakuna hospitali ya maana pale katikati isipokuwa Hospitali ya Wilaya ya Korogwe. Idadi ya watu ni wengi, idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa ni wengi na dharura zozote za ajali za mabasi, watu wote hukimbizwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuiboresha kidogo bajeti ya Wizara ya Afya na angalau basi tuangalie na maeneo haya yanayokua kwa haraka kama Korogwe Mjini yakipewa kipaumbele katika kuwahudumia watu. Tuongezewe Madaktari ambao wana ujuzi hasa ule wa Uganga wa mifupa kwa sababu ajali zinazotokea kwenye eneo la Korogwe hapo katikati ni nyingi na uwezo wa hospitali ile ni mdogo. Tuongezewe pia na sehemu hata za kuhifadhi miili kwa sababu hata ile tuliyokuwa nayo pia kuna wakati inakuwa haitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudie tena kwenye sakata la maji. Naiunga mkono bajeti hii sana, hasa pale ilipotoa kipaumbele cha maji. Maeneo yetu yanayokua haraka, maeneo ambayo yana mfumo uliokuwa sawa na mfumo wa kikoloni wa kusambaza maji yanahitaji bajeti ambayo imeandikwa vizuri. Yanahitaji sisi tuweze kuyasimamia, yanahitaji Serikali iweze kuwahurumia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na magari mengi yaliyoandikwa programu ya maji tangu mwaka 2008 pale eneo la Korogwe Mjini. Ukipiga hesabu ya magari yale matatu au manne yanaweza kutupeleka kwenye takriban milioni 700 au 800. Tungeweza kuuza mawili, tungeweza kupata visima kumi pale mjini. Sasa tuone kama mipango ile mikubwa kabisa ambayo ilikuwa ikilenga ufadhili hasa ule wa Benki ya Dunia imeshindikana, basi tutoe kipaumbele kwa maeneo ambayo sisi tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru pia bajeti hii kwenye eneo la kilimo na msamaha uliotoka, sasa nikiangalia kadhia hii ya maji, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie pia kutoa msamaha kwa gari ambazo zitakuwa zina *drilling rakes* kwa ajili ya kuchimba visima ili kuweza kutoa tahafifu inayokusudiwa. Tuangalie kwamba, kodi za magari ya kuchimbia visima ni kubwa mno, unalipa kama ambavyo mtu anaagiza gari nyingine yoyote na kila *accessories* iliyomo kule ndani huwa inapigiwa kodi pia kwa sababu nyingine siyo *truck mountain* zinakuja kwenye vipande vipande. Kwa hiyo, ukileta *generator* mle ndani utapigiwa kodi, ukileta *machine* au *mud pumps* utapigiwa kodi, ukileta *drilling bits* pia zitapigiwa kodi, ukileta *drilling roads* utapigiwa kodi. Sasa tunaomba msamaha utolewe kwa gari ambazo zitafanya *projects* maalum ambazo zitawasaidia wananchi wetu kupunguza shida ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana jamii ya wana Korogwe Mjini, niseme mmenituma kazi na nitaifanya kwa umakini, nitagonga kila mlango tutaangalia yale

tunayoyaweza, tutasimamia kwa msingi yale tunayoyajua na yale ambayo Serikali ina uwezo nayo kwa sasa. Bajeti hii imeelekeza nguvu nyingi katika kuwekeza kwenye viwanda na hatimaye tuna maeneo mazuri, tuna mazao ya kutosha, tutaangalia mfumo uliowekwa kupitia Benki yetu ya Raslimali. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuweka dirisha maalum litakalohusisha suala la uwekezaji kupitia viwanda na hatimaye kutoa ajira kwa vijana.

*(Hapa Kengele Ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yusuph Nassir, tunaendelea na Mbunge anayefuatia ni Mheshimiwa Sabreena Sungura, halafu Mheshimiwa Grace S. Kiwelu ajiandae.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu wangu kwa kunijaalia leo hii kuwepo miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza aliyekuwa mgombea urais kwa tiketi ya CHADEMA Dokta Peter Wilbrod Slaa kwa umahiri wake aliouonyesha katika kutafuta kura na uvumilivu wa kisiasa aliouonyesha baada ya matokeo mpaka leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kuupongeza uongozi wa Kambi ya Upinzani na wapiganaji wetu wote waliotujalia kura nyingi na kutufanya leo hii tukawa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitachukua fursa hii kuwapongeza wanawake wa Kigoma walioniwezesha leo hii kuwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia naomba kuchukua fursa hii kuwaombea wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao wamefukuzwa hapa juzi kwamba, Serikali iweze kuwaangalia kwa jicho la huruma na kuhakikisha vijana hawa wanarudi chuoni kwani wengi wao wanazagaa mitaani na wengine wakikosa nauli za kurudi nyumbani. Sasa hali hii inaweza kuwa ni athari kubwa hasa kwa wanafunzi wa kike, wanaweza wakaanza biashara mbaya ya kujiuza, hivyo ikawapelekea kupata magonjwa hatarishi. Naomba Serikali isikie kilio cha wanafunzi hawa na iweze kuwa-*consider* ili waweze kurudi chuoni na kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, napenda kuchukua fursa hii kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii, naomba nianze na upande wa kilimo. Upande wa kilimo tumeona umetengewa *almost 1.9* ya bajeti yote. Kwa dhana ya Kilimo Kwanza kiwango hiki ni kidogo sana kuweza kufanya mapinduzi ya kilimo ambayo tunayatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanasumbuliwa na jambo moja kuu ambalo limegawanyika katika vipengele viwili, jambo hilo ni njaa. Watanzania wana njaa ya tumbo na kichwa.  Ninaposema njaa ya kichwa namaanisha elimu na ninaposema njaa ya tumbo namaanisha kilimo. Fedha hii ni ndogo, hivyo, tunaiomba Serikali hapo mbeleni iweze kuangalia sekta ya kilimo kwa sababu ni sekta mama na ni sekta ambayo inatoa *almost 70%* ya ajira za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza mipango mingi ambayo imepangwa na Serikali ya kuweza kuiinua nchi yetu. Lakini kama tunarudi mitaani na kusema tukae na wanavijiji wetu au na wananchi wetu kuweza kuangalia ni jinsi gani na wao watashiriki katika mipango hii, lakini kama wananchi hawa wana njaa hawawezi kukaa na waka *participate* vizuri katika mipango hii ya kuondoa janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie upande wa pili, yaani upande wa matumizi ya Serikali. Yalikuwa ni matarajio makubwa ya Watanzania kwamba bajeti hii ya Serikali ingeweza kupunguza matumizi ya Serikali na hiki kimekuwa ni kilio kikubwa. Ni vema Serikali ikakumbuka kwamba, ni kubwa sana hivyo gharama nyingi zinakuwa zinapotea kwa uendeshaji wa shughuli za Serikali. Kwa hiyo, napenda kuchukua fursa hii kuiomba Serikali iweze kupunguza ukubwa wake, hivyo basi, fedha ambazo zingeweza kuhudumia gharama nyingine zikaweza kutumika katika matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikumbuke kwamba fedha hizi ni fedha ambazo tunakopa, ni fedha ambazo pia zina riba hivyo basi zinaongeza deni kwa Taifa na si busara ya kawaida kufanya sherehe na maadhimisho mbalimbali kwa fedha za mikopo. Watanzania walitegemea bajeti hii si kwamba tu Serikali ingesema inapunguza matumizi ya namna hiyo bali ingekuwa ni kufuta kabisa ili kuondoa mianya ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niguse katika sekta nzima ya madini. Ongezeko la kodi katika suala zima la vileo ikiwemo sigara, pombe na mvinyo sidhani kama ni vitu ambavyo vingeweza kusaidia kutusukuma mbele kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwa ni matumaini ya Watanzania kwamba bajeti hii Serikali ingeweza kupitia upya mikataba na kodi za madini ili kuongeza kipato cha nchi yetu. Lakini kuongeza kasi ya mfumuko wa bei katika vitu hivi ni aidha, Serikali ilitaka Watanzania wapunguze kunywa pombe na kuvuta sigara ama Serikali inataka watu hawa waingie kwenye kunywa gongo na kutumia sigara za kienyeji ambazo zinajulikana kama bangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nirukie suala lingine la nne ambalo ni faini za barabarani. Sentensi zimekuwa tata kwani Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, faini zinapandishwa mpaka shilingi 50,000/= lakini kwenye vitabu tunaona zimepanda mpaka kufika shilingi 300,000/=. Wananchi wengi matumbo yamekuwa joto kwamba faini hizi kweli wataweza na makosa yameumbiwa binadamu hakuna mkamilifu. Kiwango hiki ni kikubwa, tunaomba Waziri atoe tamko kwamba ile shilingi 50,000/= aliyoitamka yeye ama ni zile shilingi 300,000/= zilizopo kwenye vitabu ili hata wale *Traffic* wetu waliokaa mkao wa kula waweze kujua ni nini kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hapo tukija kwenye bajeti yetu tukiangalia katika ukurasa wa 39 kuna *welfare of civil servants*. Kutokana na bajeti yetu kuwa ndogo na kiwango tulichotarajia kutumia kuwa kikubwa, napenda kuchukua fursa hii hasa katika Wizara ya Sheria na Katiba kwamba Wanasheria wetu wamekuwa wanapata mshahara mdogo sana. Hapa juzi juzi mishahara imeongezwa lakini ilikuwa ni kwa Wanasheria wanaofanya Bunge na Wanasheria walio chini ya *Attorney General.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kwamba na Wanasheria wetu waliopo katika *Local Government* na Wizarani waweze kuongezewa mishahara kwani kwa kutokufanya hivyo kunawafanya Wanasheria wetu wazuri kwenye *Local Government* wanakuwa wakipata kazi katika sekta nyingine ambazo wenyewe wanasema zinalipa, wanaondoka kwenye *Local Government*, hivyo kufanya Wanasheria wazuri kwenda kwenye sekta binafsi na kuacha Halmashauri zetu zikiwa si kwamba na Wanasheria wabaya lakini Wanasheria ambao wanakuwa si *competent* kihivyo, jambo ambalo linapelekea sasa kesi nyingi za Halmashauri zinakuwa zinapoteza na kulipa mabilioni ya fedha kama gharama. Kwa hiyo, tuhakikishe vijana hawa tunawaongezea mishahara ili waweze kubaki kwenye taasisi hizi muhimu na waweze kufanya kazi ya kuendeleza Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye ukurasa wa 43 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tumeona hapa *VAT* imekuwa *exempted* katika kuingiza vifaa vya uvuvi. Kule kwetu Kigoma watu wengi wanategemea biashara na sekta ya uvuvi. Lakini katika sekta ya uvuvi kama tunavyofahamu Ziwa Tanganyika ni ziwa lenye kina kirefu, kwa hiyo, wavuvi wetu kwa kutokuwa na utaalam wa kutosha na vifaa vya uvuvi wa kutosha ni hali ambayo inaweza ikawaweka katika mashaka. Lakini mbali na hapo wavuvi wale wamekuwa wakipambana na changamoto nyingi wanapokuwa katika uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ni wafanyabiashara kutoka nchi za jirani ikiwepo Kongo, Burundi na Zambia, wamekuwa wakikutana nao katikati ya maji na biashara yote ikiishia hapo na wakirudi nyumbani na samaki kidogo sana hali ambayo inafanya Halmashauri zetu zinakosa mapato kutoka kwa wanunuzi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hapo wavuvi hawa wamekuwa wakinyang'anywa mitumbwi yao na Maharamia wanaotoka Kongo na baadhi yao baada ya uvamizi na kunyang'anywa vifaa vyao, wakisharudi nyumbani wanapata taarifa kwamba Mitumbwi yao iko upande wa pili wa Kongo na hivyo wanachukua barua za

utambulisho kwa Mkuu wa Wilaya na kwenda Kongo kugomboa mitumbwi yao hiyo ambapo wakifika kule wanatakiwa walipe takriban kati ya dola 700 hadi 1000 ili kupata mitumbwi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali iweze kushughulikia tatizo hili kwani linapelekea tunakosa mapato ya kutosha kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kugusia ni suala la Mkoa wa Kigoma katika dhana nzima ya miundombinu. Mkoa wa Kigoma umekuwa ni Mkoa wenye neema lakini ndiyo Mkoa ambapo umesahaulika kwa muda mrefu toka Uhuru. Mheshimiwa Mbunge hapa juzi juzi kasema na sisi tunataka kuunganishwa na Tanzania, na alivyoulizwa hata kwa mara ya pili alisema tunataka kuunganishwa na Tanzania, hakumaanisha kwamba amekosea lakini hii ni kauli ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Rais kwamba Kigoma sasa nitawaunganisha na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuiomba Serikali kama ina nia thabiti ya kutuunganisha na Tanzania, basi zoezi la barabara hizi liweze kupewa kipaumbele hivyo basi mara moja tuweze kuwa *connected* na wafanyabiashara wanaotoka Mkoa wa Kigoma na wao waweze kuendelea. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 68(8) nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge ambaye anaongea sasa. Hii ni mara ya pili, alianza mwingine juzi na huyu sasa anarudia. Mimi nadhani huu ni udhalilishaji kwa watu wa Kigoma. Kigoma ni sehemu ya Tanzania, ukiniambia leo tuna nchi inaitwa Tanzania ambayo haina Kigoma mimi siijui hiyo Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa maana ya maendeleo, maendeleo ni mchakato, miaka mitano iliyopita Kigoma zimejengwa barabara za lami za kilomita 96, leo hii sasa hivi kuna barabara ya lami imeanza na mkandarasi yupo kilomita 76. Leo hii linajengwa daraja la Malagarasi na kilomita 48, tulikuwa na tatizo la umeme leo mji wa Kigoma hauna tatizo la umeme, Kasulu na Kibondo nako baada ya mwezi mmoja watakuwa wamewasha umeme, kusema sasa Kigoma siyo Tanzania huu ni udhalilishaji, ningeomba Mheshimiwa Mbunge ayafute maneno haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge unapotumia kifungu hicho kuomba Taarifa huombi Mwongozo wa kumtaka mzungumzaji akanushe maneno yake kama ni ya ukweli ama uongo. Kwa hiyo, umempa taarifa hiyo umemsaidia kujua yale yanayoendelea kule Kigoma, kwa maana hiyo umesahihisha kile ambacho kilikuwa

kinaongelewa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge endelea ukizingatia taarifa iliyotolewa. *(Makofi)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa yake siitaki kwa sababu Mbunge huyu hana uchungu na watu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea kama ifuatavyo, Mkoa wa Kigoma tumekuwa na umeme lakini umeme huo ni wa jenereta, umeme wa jenereta vikipatikana viwanda vizito viwili tu umeme ule haufanyikazi. Kwa hiyo, tunahitaji umeme wa Mto Malagarasi, tumepiga kelele na Mheshimiwa Rais akasema atakuja kulitekeleza hilo, hivi karibuni tunasikia mto ule una vyura wa ajabu duniani.

Kwa hiyo, suala hilo linaweza likazuia utekelezaji wa mradi wa umeme ukashindikana. Sasa wakazi wa Kigoma wanahoji; vyura na binadamu nani ana thamani? Kama tunaamua kusema vyura wale wana thamani, basi tuanzishe *center* ya utalii ili mkoa uingize pesa ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudi tena kwenye suala zima la usafiri wa majini katika Ziwa Tanganyika. Mkoa wa Kigoma tuna meli ambazo tuliachiwa na wakoloni toka enzi hizo; meli hizo ni *MV Mwongozo* na *MV. Liemba.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni kengele ya pili, pamoja na kuongezewa muda ulibakiza dakika chache. *(Makofi)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Grace Kiwelu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo**…**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mchangiaji anayefuata, Mheshimiwa Grace Kiwelu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo, Mheshimiwa Mbunge anasema meli ya Mwongozo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed, Mheshimiwa Grace Kiwelu naomba uketi. Mheshimiwa Kessy naomba uheshimu kiti, tunapoteza muda wa kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge wawakilishe mawazo ya wananchi.

Naomba Mheshimiwa Grace aendelee na kama kuna taarifa ya msingi kama alivyofanya Mheshimiwa Peter Serukamba, inatolewa na nimemwambia Mheshimiwa Sabreena azingatie maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma na aendelee. Mjadala

umekwisha, Mheshimiwa Grace endelea, Waheshimiwa Wabunge tutumie muda wetu vizuri.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache katika Bajeti hii ya mwaka 2011/2012. Kabla ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kunipa nguvu ya kuweza kusimama katika ukumbi huu na kuweza kuzungumza machache kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na mwenzangu kumpongeza aliyekuwa Mgombea wa Urais wa CHADEMA, kwa kazi kubwa sana aliyoifanya kuzunguka nchi hii na kuwezesha kupata Wabunge 48 kutoka Wabunge 11 tuliokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeliti, pili nichukue nafasi hii kuwapongeza akinamama wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa imani yao kubwa waliyoonesha kwangu na kuweza kunirudisha tena Bungeni kwa kipindi cha tatu, nawashukuruni sana. Niwapongeze wanachama na wapenzi na Watanzania wote wenye nia njema kwa kuendelea kukiunga chama chetu mkono, tunawashukuru na hatutawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia Bajeti napenda niseme maneno ya utangulizi. Wabunge wamekuwa wana hofu kubwa sana kuhusu maandamano, wengi wamekuwa wakidai kwamba mpango wa miaka mitano na Bajeti hii haitaweza kutekelezeka kama maandamano ya CHADEMA yataendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace, naomba ujikite kwenye ajenda na ajenda ni Mpango wa Bajeti na kwenye Bajeti hakuna maandamano. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa mwongozo wako, ila tu niwatake Watanzania kwamba waendelee kutuunga mkono na tutaendelea kuja huko kwenye mikoa yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na gharama za maisha. Wewe ni shahidi gharama za maisha na upandaji wa bei unazidi katika nchi yetu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema kwamba gharama hizi zinapanda kutokana na kodi kubwa ya mafuta, lakini katika Bajeti yake hajatuonesha atapunguza kodi hiyo kwa kiasi gani. Tunajua kipato cha chini cha Mtanzania ni kati ya shilingi 1,500/= mpaka shilingi 1,600/= lakini leo unga wa sembe kilo ni shilingi 1,000/= kwa kilo, sukari pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa tamko kwamba ishuke bei, lakini mpaka leo Dar es Salaam kilo moja ya sukari ni shilingi 2,000/=, kopo la mkaa leo ni shilingi 1,500/=, leo Mtanzania huyu wa kima cha chini sijui ni vipi anaweza kumudu maisha yake ya kila siku na gharama hizi zinazidi kuendelea. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha basi tujue kwamba kodi hii ya mafuta inapunguzwa kwa kiasi gani ili Watanzania wale maskini nao waweze kuishi kwa amani katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la nidhamu ya fedha. Katika nchi yetu tumekuwa tunapitisha fedha nyingi sana kwenda katika Halmashauri zetu na pia katika Wizara zetu, lakini kumekuwa na matumizi mabaya sana ya fedha. Fedha hazina msimamizi, zimekuwa zinatumika kama vile hazina mwenyewe na hivyo wameendelea kutumia kwa sababu hakuna hatua kali zinazochukuliwa kwa wale wahusika wote wanaotumia fedha hizi vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni mashahidi, nilikuwa kwenye Kamati ya *LAAC* kipindi kilichopita tulijionea katika Halmashauri zetu jinsi ambavyo miradi inatekelezwa kwa kiwango cha chini, wakati fedha nyingi zimepelekwa katika Halmashauri zetu. Lakini pia katika Wizara *furniture* zinazonunuliwa nikienda mimi leo dukani bei ninayoipata ni tofauti na nitakapokwenda Wizara *either* ya Fedha au Madini. Huu ni wizi unaofanywa na Watanzania ambao hawana uchungu na nchi yetu. Tuitake Serikali sasa tukomeshe matumizi haya mabaya, tuwe na nidhamu ya fedha ili tuhakikishe tunatunza rasilimali zetu vizuri na fedha hizi ambazo zinatokana na walipa kodi maskini wa nchi hii ziweze kuwafikia na kuondoa kero walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Sheria ya Usalama Barabarani. Juzi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyoisoma hapa Bungeni, alituambia kwamba wanaweka tozo ya faini ya shilingi 300,000/= katika kitabu chake kinasomeka hivyo, katika *finance bill* tuliyogaiwa juzi nayo inaonesha shilingi 300,000/= lakini yeye alitamka shilingi 50,000/= sasa tunachotaka kujua ipi ni sahihi, kwa sababu tunachokuja kupitisha hapa ni *finance bill* ambayo inaonesha shilingi 300,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo tunajua sekta hii ya usafiri imewasaidia vijana wengi sana, wamekopa hela, wamenunua pikipiki, bajaji, wengine wana *hiace* lakini tutakapowaingizia tozo hii ambayo sijui usahihi wake ni upi, ni shilingi 50,000/= au shilingi 300,000/= lakini zote ni nyingi, tunataka Serikali iangalie mara mbili vijana hawa ambao tunawatoza faini hii ni kwa ajili ya kupunguza ajali au kuongeza mapato ya Serikali? *(Makofi)*

Mimi nina amini kwamba kama ni kupunguza ajali ni wajibu wetu sisi Serikali kutoa elimu kwa vijana hawa, waelewe Sheria za Usalama Barabarani na ndipo waweze kuzifuata, lakini kwa tozo hizi tunazidi kuwaweka vijana vijiweni. Tunawanufaisha matrafiki, siyo siri tunajua wanachukua rushwa ndogo ndogo barabarani, shilingi 20,000/= zenyewe zilikuwa hazifiki leo ni shilingi 50,000/= hii tunazidi kuwanufaisha wachache, tunawaumiza vijana ambao ndio wengi wameingia kwenye ajira hii, tuna tatizo kubwa la ajira katika nchi hii kwa upande wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie suala hili mara mbili kwa sababu tunawategemea vijana, vijana ni nguvu ya Taifa hili kwa hiyo tuwawezeshe wenyewe wameweza kubuni miradi hiyo ya usafiri tusiwavunje moyo, tuwatie moyo. Mheshimiwa Waziri, tozo hii muiangalie na muweze kuipunguza ili vijana wetu waweze kufanyakazi, wasirudi tena vijiweni wakaendelea kuzurura barabarani na kuvuta bangi, hatupendi watoto wetu wafike huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la magari ya viongozi. Juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amepongezwa na mimi nampongeza kwa kuweza kukataa *VX* na kuchukua *GX*, ingawa sijui tofauti za bei ni kiasi gani kwa sababu mie siyo mtaalamu wa magari. Ningependa basi Waziri Mkuu ameonesha njia, yeye ana *GX* lakini kuna *VX* kwenye misafara yake, sasa sijui ni kwa nini hawa wanaokuwa kwenye msafara wake bosi wao amekataa *VX*, wao wana ma-*V8* wanakwenda kwenye msafara wa Waziri Mkuu. Tunapenda kuwe na nidhamu, kama Waziri Mkuu amekataa basi na wengine wafuate nyayo zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo huwezi kutofautisha kama huyu ni Mkurugenzi wa Halmashauri, huyu ni Naibu Waziri, huyu ni Waziri kwani magari yote ni ya thamani kubwa, vipuli bei ni ya juu, sasa tunataka kuwe na aina za magari zitakazotumika. Kama tukiamua ni Pajero basi ziwe hivyo, wale wenye nyadhifa za juu angalau tunaweza kuvumilia, lakini Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakurugenzi kwenye Wizara, Halmashauri sasa ufike wakati tuwe na uchungu na fedha za walipa kodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari haya yanauzwa aghali sana, vipuli vyake kama nilivyosema ni vya aghali sana, kwa hiyo, sasa tujifunze ndugu zangu Mawaziri na kama alivyotoa ushauri Mbunge wa Ilala juzi kama inawezekana wakopeshwe magari wapatiwe hela ya mafuta watumie magari hayo kufanyia kazi na baada ya muda na watakapomaliza wajibu wao magari yatakuwa ni ya kwao tuache kutumia fedha hizi vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalopenda kulisema kuhusu magari haya, tumeyaona magari haya baada ya muda wa kazi yanazurura mitaani. Tunawataka wanaotumia magari haya baada ya muda wa kazi waya-*park* na watumie magari yao. Tunayakuta kwenye baa, sasa huu si mfano mzuri wa matumizi ya magari haya na ndiyo maana tunapendekeza ni vizuri wakakopeshwa ili hata wakitoka kazini basi kama wanaamua kwenda kujipumzisha waende kwa magari yao na waache kutumia magari ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la leseni za biashara. Nimesikitika kusikia kwamba leseni hizi zinarudishwa tena, tulizifuta leseni hizi za biashara mwaka 2003 na hii iliwasaidia sana akinamama na vijana kuanzisha biashara ndogo ndogo, lakini cha kustaajabisha tena leo zinarudishwa. Hivi mama huyu ambaye mtaji wake haufiki shilingi 10,000/= kule kijijini mnamwambia akachangie shilingi 10,000/= kwa mwaka atazitoa wapi wakati mtaji wenyewe hata shilingi 10,000/= haufiki? *(Makofi)*

Tunajua wakati ule wa kodi ya maendeleo akinamama na akina baba walikuwa wanakimbia nyumbani kwa kushindwa kulipa kodi hizi, sasa leo tunazirejesha tena, tunataka kurejesha machafuko ndani ya nyumba kwa sababu biashara hizi ndogo akinamama walipokuwa wanazifanya zilikuwa zinasaidia kunyanyua kipato, kuwezesha mama kupata hela ya mboga na kupikia familia, leo anarudi kwa baba kumdai hela ya mboga. Naiomba sana Serikali ada hii ya leseni tuiondoe na tuwawezeshe akinamama

hawa ambao waliweza kufanya biashara hizi kwa manufaa ya familia zao na waendelee kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi wanaokusanya kodi hizi ni Watendaji wa Kata na Vijiji, tunawajua wanavyojifanya Miungu watu huko vijijini, wanavyowanyanyasa wananchi. Niombe sana Serikali tunawahitaji sana akinamama na tunajua ndiyo nguzo ya familia, kwa hiyo, nawaomba muondoe kodi hiyo ili tuwawezeshe akinamama hawa waishi kwa amani katika nchi yao pamoja na vijana ambao ni nguvu ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee juu ya afya. Najua afya imeongezewa 0.3% katika Bajeti hii, lakini tunajua katika maeneo tunayotoka huduma za afya bado ni duni, hatuna wafanyakazi wa kutosha, hatuna vyombo muhimu vya kupimia kama vile darubini. Jana nimeona kwenye taarifa za habari kwamba hata wale wanaokwenda kupima *HIV* wamekosa kupimwa kwa sababu hakuna vipimo. Sasa itakuwa ni aibu kwa Taifa lenye wagonjwa wanaokosa kupata matibabu. Litakuwa ni Taifa la ajabu sana, watu wake watakuwa ni wagonjwa wanaokosa matibabu na watashindwa kufanya kazi za kuendeleza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Tunaiomba Serikali iongeze Bajeti, tumeona hospitali hazina dawa, watu wakienda kumuona daktari wakishapimwa wanaandikiwa kwenda kununua dawa. Nimesema toka mwanzo kwamba kipato cha Mtanzania ni kidogo, tunajua gharama za dawa zilivyo aghali kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie Wizara hii ya afya ili Watanzania waweze kupata huduma bora katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hospitali za Serikali zinavyofungwa kutokana na wakaguzi waliotoka Wizara ya Afya, hazina wahudumu, ni chafu na zinatia aibu. Tumuombe Waziri anayehusika kusimamia sekta hii ili iwe mfano. Tulikuwa tunasema hospitali za watu binafsi ndizo chafu, lakini tumeona kutoka kwa wakaguzi wetu tuliowatuma wenyewe, hospitali za Serikali ndizo zinaongoza kwa uchafu, ni aibu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie hospitali zetu na watakapotimiza wajibu wao nina amini Watanzania watakuwa na afya njema, wataweza kufanya kazi vizuri za kuongeza uchumi kwa Taifa na kwa familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itapunguza hata ile hali ya watu wanaokimbilia kwa babu, ulisema wanakwenda hata wanaotoka nchi za nje lakini sisi tuoneshe mfano kwamba watu wetu hawakimbilii kwa babu kwa sababu wanapata dawa nzuri kutoka katika hospitali zetu, wanapata huduma nzuri za afya, hawatakwenda kwa babu watakimbilia hospitali ambako tunaamini ndiko kwenye matibabu ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, naomba nimuite sasa Mheshimiwa Christowaja Mtinda na Mheshimiwa Mtutura Mtutura naye ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyoko mezani kwetu. Kwanza kabisa nami niungane na wenzangu kwa dhati kabisa kuwaombea wanafunzi waliofukuzwa wa Chuo Kikuu cha Dodoma waweze kurudi masomoni ili waweze kumalizia mitihani yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu mtoto akikosea dawa si kumchapa au kumfukuza nyumbani, dawa ni kumkalisha na kumfundisha aweze kufuata maadili mema. Lakini sijui niseme nini inapotokea pia kama mzazi ukikosea hiyo sasa inatakiwa busara itumike. Kwa hiyo hili naliomba tuungane wote tuweze kuwasaidia wanafunzi wetu ambao tunawategemea sana kuwa wataalamu wetu wa baadae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nami nichangie katika hoja hii ya Bajeti. Mimi sina matatizo na vipaumbele ambavyo vimewekwa kwenye Bajeti. Lakini nimepata mashaka baada ya kuona kwamba kuna maneno yanafuatia baada ya vipaumbele, yanasema hivi naomba ninukuu; "Bajeti itahakikisha pia kuwa mafanikio yaliyopatikana katika sekta za elimu na afya yanalindwa pamoja na kuimarishwa ubora wa huduma zinazotolewa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia hapo kwa nini nimepata wasiwasi, naomba nimnukuu mwanazuoni mmoja aliyepata kusema maneno yafuatayo; "Ukifikiria mwaka mmoja ujao, panda mbegu, ukifikiria miaka kumi ijayo, panda mti na ukifikiria miaka 100 ijayo elimisha watu." Maana ya mfano huu ni kwamba ukipanda mbegu utavuna mara moja, ukipanda mti utavuna mara kumi na ukipanda kwa miaka 100 utavuna mara 100. Maana yake ni nini? Vipaumbele vilivyowekwa nimesema ni vizuri, lakini nilitegemea kwamba tusingeacha kipaumbele cha elimu. Bila elimu mambo tunayozungumzia umeme, miundombinu na vyote ambavyo tunavizungumzia haviwezi kufanyika sawa sawa kama hatuna wataalamu wetu wa ndani. Nimeshtuka pia kuona kwamba Bajeti itaendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana katika elimu na mimi nasema elimu kwanza. Sasa najiuliza je, tufurahie au tulinde mafanikio yaliyopatikana kwa kuangalia kwa mfano matokeo ya mwaka jana ya kidato cha nne wanafunzi wetu kufeli kwa asilimia 88 kwa *division zero* na *four* ndio tuyalinde mafanikio hayo Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, tujivunie shule zetu za sekondari za Kata ambazo kwa kweli kabisa na ndani ya mioyo yetu tunashuhudia kabisa si shule za sekondari ambazo zinakidhi mahitaji ya kuitwa sekondari kwa sababu sekondari hizi zimeonesha upungufu mkubwa, wote tu mashahidi, hazina walimu wa kutosha, hazina vitendea kazi, hazina maabara, hazina maktaba na hazina mabweni, je, tujivunie haya mafanikio ambayo yanazipata shule zetu za sekondari za Kata tutayaita hayo ndio mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tulinde mafanikio ambayo yamesemwa kwa shule kadhaa za sekondari za Kata kukimbiwa na wanafunzi kwa kutokuwa na walimu hata mmoja mfano ninao shule nyingi hasa katika mkoa wangu ninaotoka mkoa wa Singida,

Mawaziri wa TAMISEMI ni mashahidi walikwenda kutembelea shule moja inaitwa Wembele walikuta hali halisi ilivyokuwa, haina walimu, yamebaki magofu na wanafunzi wamekimbia, je, tujivunie hayo mafanikio? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulinde idadi kubwa ya watoto wanaojiunga na shule zetu za sekondari za Kata ambao nadhani ndio tunajivunia, lakini baada ya kumaliza shule hawajui kusoma wala kuandika na matokeo yake wanarudi majumbani wanaanza kuokota chupa mitaani na wengine kukaa kwenye vijiwe na kuwa wapiga debe wa daladala hayo ndiyo mafanikio ambayo tujivunie? Lingine tujivunie mafanikio ya walimu wetu kupata matatizo mara wanapofuata stahiki zao hususan madeni wanayoidai Serikali na mishahara yao duni na mazingira yao duni ya kufundishia na nyumba wanazokaa ambazo hazistahili kabisa kwa binadamu kuishi, je, hayo ni mafanikio ambayo tujivunie na kuyalinda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatukubaliani na hayo naomba sasa tuwe wakweli, tuchukue hatua kama Taifa ili tufanye chini/juu tuweze kuinua kiwango cha elimu za shule zetu za sekondari. Bila hivyo tutabaki kuwa Taifa la watu mbumbumbu na Taifa la watu wenye matabaka. Tunafahamu kabisa kuna shule binafsi zinafanya vizuri, zina matokeo mazuri, tutaweka matabaka kati ya watoto wa maskini na watoto ambao wana uwezo mkubwa. Matokeo yake tutaanzisha ukoloni ndani ya nchi yetu. Hilo tuliogope wote kwa pamoja na tushirikiane ili tuweze kuinua kiwango cha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kwenye suala hilo la elimu lakini sasa niende kwenye elimu ya juu. Katika mpango wa miaka mitano tumeonyeshwa kwamba kutakuwa na malengo ya kupanua Vyuo Vikuu na kuanzisha Vyuo Vikuu vipya na pia tutawafundisha wataalamu hasa wa masomo ya sayansi na vinginevyo. Swali langu kuna mikakati gani ya muda mfupi ambayo imeandaliwa ili kuweza kuwapata hao wahadhiri ambao watakwenda kufundisha Vyuo Vikuu. Ninavyofahamu nichukulie mfano wa chuo kimoja tu Chuo cha Mkwawa, walimu au wahadhiri walikuwa wanazidiwa na wanafunzi mpaka wanafundisha *session* tatu somo lile lile moja na wanafunzi jinsi walivyo wengi mpaka wanasomea *cafeteria.* Sasa sijui tuna mpango gani ili kuweza kuzalisha wataalamu ambao watakwenda kufanya kazi katika nchi yetu.

Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuweza kuongeza asilimia nne ya tozo ya kuendeleza ufundi stadi kwa Bodi ya Mikopo, mimi nina tatizo la Bodi ya Mikopo, tunafahamu Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya kuchunguza Bodi ya Mikopo, hiyo ripoti ipo wapi? Kwa nini hatujaambiwa kitu gani kilibainika kwenye Bodi ya Mikopo? Tunachotaka kufahamu ni kitu gani kiliipata Bodi ya Mikopo na kupelekea migomo mingi vyuoni na wanafunzi kufukuzwa kila mwaka? Mimi nadhani suala si kuongeza tu pesa, suala ni kuifumua hiyo Bodi ya Mikopo ikiwezekana chombo kingine kianzishwe ambacho kitasimamia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi na ili kupunguza matatizo ya wataalamu mbalimbali hususani walimu…

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Taarifa

**MWENYEKITI:** Eeeh! Kuna Taarifa?

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia Kifungu 98(8). Nimeshindwa kuvumilia ni kiasi gani watu wanashindwa kupata muunganiko wa kisekta. Mzungumzaji anaposema vipaumbele havisaidii elimu, mimi nasema haifahamu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea suala la elimu kwa mfano Singida katika kipindi hiki tunavyoongea bila maji elimu haiwezekani, watoto wanaondoka saa sita mchana wanarudi jioni kwenye saa tatu usiku, wazazi wanaondoka saa tatu usiku wanarudi saa nane usiku. Walimu wanatafuta maji, bila maji walimu hawakai kwenye zile shule. *(Makofi)*

Lakini vile vile bila barabara walimu wanakimbia zile shule, lakini vile vile bila umeme walimu hawawezi wakakubali zile shule. Lakini vile vile bila chakula, tumekuwa tukilia mara zote, bila chakula watoto hawasomi. Unaposema elimu kwanza unaongelea nini, yaani unajiangalia uliye shiba na unasema unaweza ukasoma, kule hawasomi bila hivi vipaumbele. Kwa hiyo, tunapotatua hili kwenye elimu tunakuwa tunasawazisha tu. Kwa hiyo, ni muunganiko wa sekta na hatujafuta kabisa elimu na umeona ongezeko napo lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ulichokifanya hapa ni kuongeza tu, yeye amesisitiza msisitizo huo huo. Shule ile haina walimu ndio maana watoto hawapo. Lakini wewe umesisitiza kwamba na ndio maana mpango umewekwa ili walimu wapatikane ili watoto warudi kwenye ile shule. Kwa hiyo, wote mko sahihi, Taarifa hizo zote zinakwenda sambamba katika ku-*address* suala moja na nia njema ya Serikali yetu ilioonyeshwa kwenye mpango na kwenye Bajeti ili kukidhi tatizo ambalo liko mbele yetu.

Mheshimiwa Mbunge naomba uendelee na *Hansard* inukuu hayo mambo yote mawili ni mambo ya kimsingi ya kufanya watoto wetu na elimu yetu iwe bora. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunisaidia kumuelimisha Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nimeshamaliza ku-*rule* na wewe una haja tena ya kuongeza neno baada ya mimi kumaliza *agenda* yangu, hebu naomba ukae. Nimeshamaliza wewe endelea na mchango wako.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa katika suala lingine la ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Suala hili limezungumziwa katika ukurasa wa 55 na mimi nitazungumzia kipengele kimoja tu katika *paragraph* ya 65 kifungu kidogo cha (4) ukurasa wa 56 ambacho kinasema kwamba; “Ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma

itasaidia kuibua miradi mbalimbali.” Kipengele cha nne kinasema; “Kuipunguzia au kuiondolea mzigo Serikali wa kubeba mashirika yasiyo na ufanisi na kuelekeza nguvu katika vipaumbele vingine.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu moja, katika ripoti iliyoletwa kwetu na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma ilipendekeza katika Bunge hili kwamba Shirika hodhi ya yaliyokuwa Mashirika ya Umma yaani *Consolidated Holding Corporation (CHC)* liliongezewa muda wake kwa sababu ilionekana kwamba muda wake unaisha mwezi Juni, 2011. Kutokana na ripoti hiyo imeonekana kwamba Shirika hili limefanya kazi kubwa na kwa ufanisi mkubwa na katika mwaka 2008 peke yake liliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.2 na katika mwaka 2009 liliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 2.6 kama matunda ya ubinafsishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuishia hapo ndipo Shirika hili liliweza kukusanya shilingi bilioni 14.3 kama gawio na kwenye hisa mbalimbali. Sasa hivi tunapozungumza mpaka mwezi Februari, 2011 bado Serikali inadai madeni yanayofikia jumla ya shilingi bilioni 23.6. Shirika hili ndilo ambalo linajua wadaiwa ni akina nani na ni wa jinsi gani ya kukusanya madeni haya. Mimi ningependekeza kwamba Wizara ya Fedha iangalie hili kwa uzito wake ili Shirika hili liweze kuongezwa muda ili Taifa lisiweze kuingia hasara kwa wadaiwa kuweza kukimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukusanya madeni itasaidia pia Serikali kuweza kulipa madeni mengine ambayo inadaiwa hasa na Taasisi zetu za ndani hususan Mifuko ya Pensheni ya Uzeeni. Tumesikia kwamba Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma yaani *PSPF* mpaka sasa inaidai Serikali shilingi trilioni tatu. Kama Serikali haitalipa mfuko huo hizo shilingi trilioni tatu ina maana sisi watumishi ambao muda wowote tunategemea kustaafu sijui tutakimbilia wapi maana hatutapata mafao yetu. Kwa hiyo, niiombe Wizara ya Fedha itilie maanani katika kulipa hii Mifuko ya Pensheni ambayo ni msaada mkubwa sana kwa watumishi ambao wanamaliza muda wao kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili tunaendelea na mchangiaji anayefuata na mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na muda ukituruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini, kwa namna walivyojikita kukichagua Chama cha Mapinduzi kikashika madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumelelewa katika maadili ya kushukuru hata kwa kidogo unachopewa. Kwa niaba ya wananchi wa Tunduru wote tunaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa namna walivyojikita katika kutuletea maendeleo. Mwenzangu Mheshimiwa Vita Kawawa asubuhi alisema kwamba barabara yetu ya

kutoka Tunduru hadi Namtumbo inajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa hivi usanifu wa kina na upembuzi unafanyika katika barabara ya kutoka Mangaka kwenda Tunduru. Hii ni ahadi kiporo, tunaamini kabisa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi anafahamu hilo na atalitengea fedha katika Bajeti ijayo ili nayo iweze kujengwa hasa kwa kuzingatia kwamba ni ahadi kiporo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalazimika kuwapongeza wachangiaji wawili wa kutoka Chama cha Upinzani. Wachangiaji hawa ni Mchungaji Mustapha Akunaay na Mchungaji Israel Natse kwa namna walivyochangia na kuonyesha ukomavu wa kisiasa na Mungu atawalinda Wabunge hawa. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi siku moja kukaa na Sheikh wangu Imam, anaitwa Sheikh Chilakweche alinipa maneno mazito. Aliniambia Mtutura mara zote unapotaka kufanya jambo lolote hata kama likiwa zuri kiasi gani basi jambo hilo ulifanye inavyotakiwa kwa uzuri zaidi, lakini ulifanye kimya kimya, sio kwa vishindo. Lakini vile vile siku nyingine nikakutana na Imam Mohamed Yaka, yeye aliniambia kwa Kiarabu alisema; "*Manibagadhaulama fadikafara, fadikafara finali jahnnam"*. Tafsiri yake kila mwenye kubughudhi viongozi walioteuliwa na Mwenyezi Mungu basi mtu huyo hatapata radhi ya Mwenyezi Mungu na ukikosa radhi ya Mwenyezi Mungu basi adhabu yake ni moto mkali. Mwenyezi Mungu atuepushe na adhabu hiyo wote tuseme *amin.*

**WABUNGE FULANI:** *Amin.*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA**: Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, wote tunafahamu nini kinachoendelea kabla hatujafika hapa na nini kinachoendelea tukiwa hapa. Leo vijana wetu wa *UDOM* wako nje, wamefukuzwa, lakini ni kutokana na ushawishi wa baadhi ya viongozi kutoridhika. Leo viongozi wale wamefunga simu zao na wanadai hapa kwamba wanazurura mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naungana kabisa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu kuwaombea radhi vijana wale warudishwe shuleni na wakirudi waelewe kwamba wale waliokuwa wanawashawishi leo wamewazimia simu na hawana msaada wowote na wakirudi wazingatie kile kilichowapeleka pale, Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi iko hapa kuhakikisha kwamba wanapata elimu ya kutosha ili waitumikie nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono Bajeti hii, ina kila sifa ambayo inatakiwa iungwe mkono na Wabunge wote, siwezi kurejea yale ambayo wenzangu wameyataja, vipaumbele vya umeme, vipaumbele vya kilimo, kodi mbalimbali zimefutwa kwenye zana za kilimo, hivi sasa ndugu zangu tuseme nini tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa umeme, dhamira ya umeme huu ambao tutauzalisha uende kwenye viwanda na uende kwa wananchi wa kawaida ili kuchochea maendeleo, lakini kwa mfumo tulionao sasa hivi kama hautabadilishwa na kwa wale tuliowapa dhamana ambao ni *TANESCO* hii itakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano halisi na nitaukabidhi baada ya kuusoma, hii ni barua iliyoandikwa na Meneja wa *TANESCO* Ruvuma kuwaandikia *Masjid Quba* pale Matogoro Songea Mjini, wanasema rejea barua yako ya tarehe 29 mwezi Aprili, 2011 ukiomba kupewa gharama za kuingiza umeme kwenye jengo lako. Mambo yaliyoorodheshwa hapa kwanza gharama ya kadi ya maombi ni shilingi 5,000, gharama ya *service line* shilingi 385,682, gharama ya kusogeza nguzo mbili shilingi milioni moja laki sita mia tisa sitini na mia tatu sitini na sita na senti ishirini na saba, *VAT* shilingi 375,668 jumla ni shilingi 2,462,000 ni Mtanzania gani atakayemudu kuingiza umeme katika hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake tutazalisha umeme mwingi, utatumika viwandani lakini wananchi wa kawaida hawataweza kuutumia, je, lengo litakuwa limetimia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amezungumza mara kadhaa, amesema waungunishieni wananchi umeme ili mpate mauzo makubwa kufanya marejesho. Matokeo yake tunazalisha umeme mwingi, utakuwa kwenye waya hautumiki na wananchi, matokeo yake maendeleo tunayoyakusudia hayatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye tozo ya mafuta, niungane na Wabunge wenzangu kwamba hata pale wawindaji wanapotaka kumuua nyati wanaangalia wampige sehemu gani, huwezi kumuua nyati kwa risasi kwa kumchana sikio, hawezi kufa. Ukimpiga nyati ukamkata mkia hafi, mpige kifuani atakufa. Kama kweli Serikali imedhamiria kupunguza bei ya mafuta ili kuleta unafuu kwa Watanzania, waangalie maeneo makubwa, siyo tozo, tozo ni asilimia 4.3 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ndugu zangu *SUMATRA*, wao kodi yao ni senti 28 kwa lita moja, hata shilingi moja haijafika leo umpunguzie ili umpunguzie nguvu ya kuweza kufanya kazi ambayo amekabidhiwa na nchi hii atafanyaje hiyo kazi? Tuangalie maeneo ambayo kweli yataleta *impact* katika bei ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee masuala yanayohusu Jimbo langu, ukitaka mwananchi wa Tunduru ujue hasira zake basi mchokoze kwenye korosho ndiyo utajua kwamba huyu mtu ana hasira au hana hasira na ukitaka ujue mahaba ya wananchi wa Tunduru basi hakikisha korosho zinapewa msaada unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Tunduru tulipata ruzuku ya *sulphur* ya shilingi milioni mia moja na ishirini na moja na wananchi wengi wakahamasika kupalilia korosho zao, korosho zingine ambazo zilikuwa misituni wananchi wamezifufua, na wanaendelea kupanda mikorosho mingine mipya. Cha ajabu katika sera ile ile ambayo tunaiimarisha ya Kilimo Kwanza badala ya kuongeza ruzuku kutoka shilingi milioni 121 za mwaka jana angalau tupate shilingi milioni 200 mwaka huu tumepata ruzuku ya shilingi milioni 50. Sielewi na wananchi wa Tunduru hawaelewi, kwa sababu hamasa kubwa zilifanyika za kuwahimiza wafufue mikorosho yao na wamefufua na hasa ukizingatia lile suala la stakabadhi ghalani, wananchi wengi wamehamasika kufufua

mikorosho yao, matokeo yake ruzuku inapungua kutoka shilingi milioni 121 kuja shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru tulilieleza hili kwa Rais tukiwa Mbinga na tunashukuru tumelieleza hili kwa Waziri wa Kilimo hapa Dodoma wamelipokea vizuri, nina imani kabisa Waziri wa Kilimo atalifanyia kazi, asisubiri Rais aingilie kati. Kwa namna alivyolipokea basi alifanyie kazi kwa haraka zaidi kwa sababu muda wa kupulizia korosho ndiyo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yetu ni kwamba Serikali itawahamasisha wafanyabiashara binafsi wawasaidie wananchi katika kupata pembejeo kama ni kwa mkopo au kuwapatia pembejeo za bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye zana za kilimo, tunaipongeza Serikali kwa kukubali yenyewe kuleta matrekta makubwa, tunayo yamekuja mengi tu, lakini je, ni matrekta mangapi mpaka sasa yamenunuliwa na yameenda vijijini, mengi yapo kwenye *show room*.

Tunaiomba Serikali kama ilivyofanya kwenye pembejeo iweke ruzuku kwenye matrekta ili wananchi waweze kununua kwa bei nafuu. Itakuwa haina maana yoyote kama matrekta haya yametoka India, yametoka China na yakaja hapa yakakaa miaka mitatu kwenye *show room* bila kuleta tija yoyote, tunaomba matrekta haya yaende vijijini wananchi walime ndipo tija itaonekana kwa kuweka ruzuku, badala ya kununua kwa shilingi milioni 40 basi wananchi waweze kununua kwa shilingi milioni 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *The Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT),* inazungumziwa *Southern corridor* na unapozungumzia *Southern corridor* huwezi kuiacha Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Lakini cha kushangaza mpango huu ambao unawafadhili wakubwa zaidi ya 18 imechukua Mkoa wa Dar Es Salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya na Mkoa wa Rukwa. Ruvuma, Mtwara na Lindi wameachwa, hivi unapozungumzia *Southern* ya Tanzania bila kuingiza Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Lindi na Mkoa Ruvuma *Southern* hiyo iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa haraka sana ama Dar es Salaam na Morogoro iondolewe na kama haiwezi kuondolewa basi mikoa hii mitatu iingizwe katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mtutura, msemaji wetu wa mwisho naamini atakuwa Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nipate fursa ya kuchangia Bajeti hii ya Makadirio ya fedha ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza kuchangia Bajeti iliyo mbele yetu, naomba kabisa nichukue nafasi hii na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, naomba kuwashukuru Watanzania wote wakiwemo wanawake, vijana na wazee, kukiwezesha Chama cha Mapinduzi kupata ushindi mkubwa kupitia nafasi ya Rais, Wabunge na Madiwani. Hakika kuchaguliwa kwa Chama cha Mapinduzi kunaendelea kudhihirisha jinsi ambavyo chama kina sera nzuri ambazo zitawaondoa wananchi hapa walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Watanzania, Umoja wa akinamama Tanzania, kukishukuru Chama cha Mapinduzi na Tume ya Uchaguzi kwa kuniwezesha mimi Amina Nassor Makilagi kuwa miongoni mwa Wabunge Wanawake wachache tuliyopewa dhamana ya kuwa Wawakilishi katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninashukuru sana kwa sababu natambua wapo wanawake wengi kabisa katika nchi hii, wenye uwezo mkubwa kuliko sisi Wanawake tulio ndani ya ukumbi huu, lakini kitendo cha Chama changu na kitendo cha Tume ya Uchaguzi kuniteua kusema kweli naomba nishukuru kwa Mwenyezi Mungu na vile vile kitu ambacho naweza kusema ni kwamba imani itazaa imani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Anne Makinda kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana za heshima na Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inadhihirisha jinsi Wabunge wa Tanzania walivyo na imani kubwa na Mama Anne Makinda, lakini si hilo tu imedhihirisha kwamba sisi wanawake tukipewa nafasi tunaweza, kinachotakiwa hapa ni kuthubutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri wa Fedha, Katibu Mkuu na wadau wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri, Bajeti inayotoa matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Bajeti hii inawagusa Watanzania wote maana ni ukweli usiofichika kwamba ili maisha bora Watanzania hawawezi wakayapata bila ya kuimarisha miundombinu ya barabara, kama reli hakuna, kama hakuna cha kutosha, kama hakuna maji safi na salama na kama hakuna viwanda na biashara na hata elimu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo naomba nami niungane na Mheshimiwa Mtutura na Wabunge wote waliochangia kuiomba Serikali yetu tukufu ambayo ni Serikali sikivu iangalie kwa macho ya huruma watoto wetu wa Chuo Kikuu ambao wamepewa mapumziko kwa muda, watafakari kwa kina na wawarejeshwe chuoni kwa sababu mimi ninajua kuna vijana wengi na mimi leo nyumbani kwangu nina vijana karibu hamsini hasa watoto wa kike wameonesha kabisa hisia zao kwamba kusema ukweli hata wengine hawakushiriki katika kuleta vurugu katika chuo. Kwa hiyo, na mimi kama mzazi naiomba kabisa Serikali yetu ifanye uchunguzi wa kina ikibainika kwamba wapo vijana wavurugaji na mimi nasema kama mzazi tuwaache, lakini wale ambao wamekwenda kwa mkumbo wasamehewe na warejeshwe chuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba sasa moja kwa moja nijielekeze katika kuchangia katika Bajeti hii ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuunga mkono asilimia mia moja kwamba Bajeti hii ni nzuri, kwa sababu vipaumbele vyake vimelenga kuwakomboa Watanzania na hasa wananwake katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unapozungumzia suala la miundombinu na unapozungumza kuimarisha barabara wanaopata adha kubwa pamoja na Watanzania wote lakini hasa inawagusa wanawake na hasa pale wanapokuwa wajawazito, kutembea katika barabara za vumbi. Unapozungumzia tatizo la maji Watanzania wote wanaguswa lakini wanaoguswa zaidi ni wanawake. Kwa kuwa tumezungumza kuwa tunataka tuimarishe uchumi wetu, ukishapata tatizo la maji wale wazalishaji wakubwa ambao ni wanawake wanaishia kutafuta maji siku nzima na kilimo chetu kinakuwa duni na hata uzalishaji unakuwa duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vilivyowekwa katika Bajeti hii mimi ndivyo vinavyonisukuma niiunge mkono Bajeti hii kwamba kweli ni Bajeti nzuri, haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha na watendaji wote kwa kazi nzuri sana waliyoifanya ya kukusanya mapato, kwa taarifa nilizonazo, mpaka sasa tumeshakusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 93 sawa na ongezeko la asilimia 17. Hiki ni kiwango kikubwa sana na ninawatia moyo na nawaomba muendelee hivyo ili itakapofika mwisho wa mwaka huu tuwe tumeshafikia lengo, na hata kama siyo kufikia lengo, tuwe tumeshapiga hatua fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe ushauri kidogo katika suala zima la ukusanyaji wa mapato. Kama ambavyo wote tunafahamu nchi yetu ina rasilimali nyingi sana, na bahati nzuri Serikali yetu ya CCM imeandaa utaratibu mzuri sana wa kukusanya mapato na imejiandaa vizuri kabisa, lakini lipo tatizo la baadhi ya watendaji wetu wasio wazalendo na wasio waaminifu ambao Serikali hii imewaamini na ikawakabidhi dhamana ya kukusanya mapato, badala ya kukusanya mapato na kuyafikisha katika mamlaka zinazohusika, matokeo yake mapato yale yanaishia mifukoni mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na wachangiaji wenzangu kwamba ni vizuri sasa Serikali ijielekeze kudhibiti mapato hasa katika maeneo ya bandari. Pale mapato yanapotea sana kwenye viwanja vyetu vya ndege, kwenye mipaka yetu kwa wafanyabiashara wadogo na wafanyabiashara wakubwa, ni vizuri tujielekeze sasa kuhakikisha tunadhibiti mianya yote inayosababisha mapato yetu yanapotelea barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kuchangia kwangu leo, natoa wito kwa watendaji wetu wa umma ambao mmekabidhiwa dhamana ya kukusanya mapato, chonde chonde kuweni waadilifu, muiheshimu Serikali iliyowaweka hapo, fanyeni kazi kwa

uadilifu na uaminifu mbadilike ili tuweze kukusanya mapato kama inavyokadiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe ushauri wa pili kwamba ni vizuri wakati tunadhibiti mianya ya kupotea kwa mapato, ni vizuri Serikali yetu sasa ijielekeze katika kudhibiti mapato ili Bajeti hii iliyotengwa, maana ukiangalia kwenye sekta ya miundombinu tumetenga fedha nyingi, sekta ya maji, sekta ya kilimo, ukiangalia hali halisi kule vijijini na ukilinganisha na thamani ya fedha iliyotengwa wakati mwingine vinapishana. Kwa hiyo, naomba sana Madiwani na sisi Wabunge, watendaji wote na viongozi tuliokabidhiwa dhamana tujitahidi sasa kuhakikisha tunafuatilia kwa karibu na siyo sisi Wabunge peke yetu, ni kuanzia Wizara yenyewe Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na watendaji wako wote tuwe na utaratibu wa kufuatilia fedha zinazokwenda hasa katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichokigundua ni kuwa tunapopeleka pesa hakuna ufuatiliaji, matokeo yake tunatuma Kamati ya Mzee Mrema wakati mambo yameshaharibika, lakini kama tungekuwa tuna utaratibu wa kupanga walau hata kila baada ya miezi mitatu kunatokea kikosi fulani cha viongozi au watendaji wa Serikali au vyama vya siasa tunakwenda kuangalia hali halisi nina imani tungeweza kuokoa miradi mingi na fedha nyingi zisingeishia kwenye upotevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la kupotea kwa mapato, pamoja na kwamba kuna baadhi ya maeneo kunafanyika aidha kwa bahati mbaya, lakini mimi ninavyojua ni maeneo mengi watu wanafanya makusudi na uzembe wa upotevu wa mapato katika miradi haufanywi kwa bahati mbaya, hii yote inatokana na uvunjifu wa maadili. Unakuta mradi umepangwa ni mradi wa shilingi bilioni moja, unakuta hapa kuna mlolongo wa *ten percent* wa kugawana mapato, huyu mhandisi anapata chake, huyu mshauri naye ana chake, Mkurugenzi ana chake, pengine Mbunge ana chake kuja kufikia kwenye mradi unakuta mradi kwa kweli hauna tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwaomba watendaji wote kuwa waadilifu kwa sababu wameaminiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie katika harakati za kuongeza mapato, naomba niipongeze Wizara ya Fedha kwa kuandaa mipango mizuri ya kuongeza mapato, kama yalivyoainishwa katika kitabu cha hotuba ya Waziri na kama yalivyoainishwa katika Mpango wa mwaka 2011 wa maendeleo na mwaka 2012 na hata kama ilivyoainishwa katika mpango mkakati wa maendeleo yetu ya Taifa ya mwaka 2011 mpaka mwaka 2016. Kusema ukweli mipango ni mizuri sana, naomba niwapongeze Wizara ya Fedha na watalaamu wote walioshiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri kitu kimoja katika suala la kusimamia hapo. Kuna hii sekta ya madini, kumekuwepo na kilio cha Wabunge kwa muda mrefu na tumekuwa tukisikia maneno ya hapa na pale kwamba nchi za wenzetu za Botswana, Namibia na Afrika Kusini wamenufaika na madini. Lakini wamenufaika kwa sababu kwa maneno tunayoyasikia ni kwamba wenzetu wana sera nzuri. Nilikuwa

nafikiri ifikie wakati sasa tutume watalaam wetu, watalaamu wazalendo maana yake usitume watalaam hivi hivi, tutume wale wazalendo, waende Namibia, Botswana na Afrika Kusini wakazitazame sera zao, kama zitakuwa ni sera nzuri siyo mbaya na sisi tukazitumia katika kurekebisha sera zetu ili madini tuliyonayo yaweze kuongeza pato katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kilimo, naomba nichangie katika hatua hii ya kilimo kwamba tunaishukuru sana Serikali yetu ya CCM na Wizara ya Fedha kwa kutuletea mpango mkakati wa kuimarisha kilimo na hasa katika kuongeza sehemu ya kilimo cha umwagiliaji. Mimi ndiyo maana nimesema Bajeti imenigusa. Naomba nipongeze sana kwa ukanda waliouchagua kuanza na ukanda wa Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuongeza hekta 1,000 za kilimo na kuweza kuzalisha kilimo cha kutosha kwa zaidi ya asilimia 120, mimi natoa ushauri kwamba sekta hii ya kilimo ndiyo inayoweza kutukomboa haraka. Nilipenda niongeze kwamba badala ya kuiangalia sana Kanda ya Kusini peke yake, ilikuwa ni vizuri sasa tuangalie na Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda ya Ziwa yenye mito yenye Ziwa ina Mikoa ya Mwanza ambako kuna Ziwa Victoria na Mto Simiyu, Mkoa wa Mara kuna Ziwa Victoria na kuna Mto Mara. Ule Mto Mara peke yake kama utatumika vizuri unaweza ukaleta tija sana hata ukaongeza pato letu. Lakini Mkoa wa Shinyanga vile vile, Mkoa wa Kagera kuna Mto Kagera na maeneo mengine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza naomba niwapongeze sana kwa shughuli ya siku ya leo, kwa kweli nadhani tunayo kila nia ya kukubali kwamba sasa nafikiri kila mtu ameanza kuzoea Kanuni zetu na tunaanza kwenda vizuri. Kwa hiyo, naomba sana tuendelee kupeana ushirikiano kama alivyoagiza *Madame Speaker*, siku za kuleana na utoto zimeshakaribia kukatika, kwa hiyo, mwendo tunaokwenda nao sasa ni wa kiutu uzima na Spika amelisema sana hilo nami naomba kulisisitiza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukifanya hivyo, mnaona hata afya ya uchangiaji wetu ndani ya Bunge inakuwa ni ya uwakilishi kamili, kwa hiyo, naomba niwashukuru sana kwa jinsi tulivyoendelea nina hakika agizo la Spika litaendelea kutekelezwa vizuri na hivyo tuweze kuwawakilisha Watanzania vizuri kuliko kulumbana katika malumbano ambayo hayana afya kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninayo matangazo machache; kwanza kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba kesho pamoja na kwamba ni Jumamosi, Kamati hiyo itakutana saa nne asubuhi ili kuweza kuendelea na kazi ya kupitia ile *Finance Bill*, tunapoelekea kumaliza mjadala huu wa Bajeti ni lazima pia *Finance Bill* nayo ipate nafasi ya kujadiliwa na kupitishwa Bungeni. Naomba Kamati hiyo na Wajumbe wote mhudhurie bila kukosa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge leo mchana nilitangaza hapa kutakuwa na mkutano wa Wabunge wote katika kuunda uongozi wa *Tanzania Parliamentary Association on Population and Development* yaani Chama cha Wabunge kinachojihusisha na masuala ya idadi ya watu na maendeleo. Mkutano ule umefanyika na mchuano ulikuwa mkubwa kweli kwenye kikao hicho leo. Naomba niwatangazie viongozi waliopatikana baada ya mchuano mkali watakaoongoza Chama hicho kwa miaka mitano. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitaanza na Kamati Tendaji wa kwanza ni *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Lolesia Maselle Bukwimba, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Said Suleiman Said na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mweka Hazina wa chama hicho amechaguliwa Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Katibu wa Chama hicho amechaguliwa Mheshimiwa Ahaji Mtutura Abdallah Mtutura, Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho ni Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu na Mwenyekiti wa Chama hicho ni Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, hapa ndani leo umekuwa na wageni kutoka Chuo Kikuu cha Tiba cha *IMTU* na hao wameoongozwa na ndugu Sebastian Siwale na Mponjoli Mwangosi, kwa hiyo hawa walikuwa ni wageni wetu wengine hapa leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo niwashukuru sana kwa ushirikiano wa siku hii ya leo na naomba sasa niahirishe shughuli hizi za Bunge na tutakutana siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi kwa ajili ya kuanza ratiba zetu rasmi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, asanteni sana.

*(Saa 1.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 20 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)*